# UCHAMBUZI WA MIKAKATI YA UPOLE KAMA INAVYOTUMIWA NA WAHUSIKA WAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *MBAYA WETU*

**NA**

**STEPHEN MACHIRA**

**NAMBARI YA USAJILI**

**C50/69445/2013**

**WASIMAMIZI:**

**PROF. HABWE**

**NA**

**BI. MARY NDUNG'U**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA MASOMO YA KISWAHILI IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**NOVEMBA, 2015**

**UNGAMO**

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kingine chochote, kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili

Sahihi ………………………….. Tarehe ………………………………

**STEPHEN MACHIRA**

**Mtahiniwa (C50/69445/2013)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi …………………………… Tarehe ………………………………..

**PROF. JOHN HABWE**

**(Msimamizi**)

Sahihi …………………………….. Tarehe………………………………….

**BI. MARY NDUNGU**

**(Msimamizi)**

## TABARUKU

Kwenu nyie wazazi wangu wapendwa:

Mamangu Esther Wanjiku na Babangu, Taracisio Machira mlionielea, kunielekeza na kunishauri kuhusu namna za kukabiliana na changamoto za maisha.

## SHUKRANI

Ama kwa hakika kidole kimoja hakivunji chawa, mchakato mzima wa kuikamilisha tasnifu hii si bidii yangu pekee na haungefanikiwa bila msaada wa wengine.Kwanza, kabisa, namshukuru Mungu kwa fadhili zake na kunipatia nguvu za kukabiliana na changamoto mbalimbali wakati nikiitafitia mada hii. Sina budi kukiri bayana kuwa, Mwenyezi Mungu amenipatia kariha na hamu ya kuendelea kuisukuma kazi hii hasa pale nilihisi kulemewe na changamoto za maisha. Kwa msingi huu, natangaza kuwa, shukrani, utukufu na heshima ni zake.

Pili, natoa na kudhihirisha shukrani zangu kwa wasimamizi wangu; Prof. Habwe na Bi.Mary Ndung'u kwa kunishika mkono na kunielekeza katika kuiandaa kazi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa hakika, mmenielekeza na kunifunza mengi kuhusu utafiti ambayo isingekuwa nyinyi ingekuwa vigumu kuyaelewa. Asanteni kwa uvumilivu ambao mmekuwa nao kwangu katika kunikosoa na kunielekeza hadi nikafikia kiwango hiki.Shukrani sana na Mungu awabariki.

Vilevile, shukrani teletele ziwaendee wahadhiri wote katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Idara ya Kiswahili. Mafunzo, maelekezo na ushauri wenu ulinitia motisha na ilhamu ya kuifanya kazi hii na kuikamilisha. Wahadhiri hawa ni pamoja na, Prof. Kithaka, Prof. Wamitila, Dkt. Zaja, Prof. Abdulaziz, Prof.Kineene wa Mutiso, Dkt. Mukhwana, Dkt. Swaleh, Bw.Mungania, Dkt. Mbuthia na Prof. Habwe bila kuwasahau Dkt.Buregeya na Dkt. Rayya Timamy. Nawashukuru nyote na Mungu awabariki kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mwisho, ningetaka kuwashukuru wanafunzi wenzangu ambao tulianza safari hii nao kwa ushauri na uelekezi wao.Wanafunzi hawa wamekuwa mhimili na mwega mkubwa kwangu katika kunipatia motisha na kunipatia mawaidha panapohitajika. Nao ni pamoja na: Indindi Henry, Makhulo Evans, Kamwanza Rosemary, Francisco Gathara, Rose Dama, Otuchi Timothy, Biasha Salim Khamis, Rita  Magara na Gikambi Ezekiel. Nyote nawatambua na kuwavulia kofia kwa uhisani wenu kwangu katika kipindi chote cha miaka miwili ambayo tumekuwa pamoja.

## IKSIRI

Utafiti huu umeshughulikia suala la upole kama linavyobainika katika matumizi ya lugha ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*. Mtafiti ametumia mtazamo wa Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) na kujikita katika kipengele cha mikakati ya upole. Data ya uchunguzi huu ilitokana na uchambuzi wa kauli na matamshi ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.* Lengo la kwanza la utafiti lilikuwa kubainisha iwapo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanaitumia mikakati ya upole katika kuokoa uso wanapoingiliana. Matokeo yanadhihirisha kuwa, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanaitumia mikakati ya upole wanapoingiliana kama njia ya kuyafanikisha mazungumzo yao. Lengo la pili la uchunguzi huu lilikuwa kubainisha jinsi sifa za wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* zinavyobainika kupitia matumizi yao ya mikakati ya upole. Utafiti huu unaonyesha kuwa, sifa mbalimbali za wahusika wakuu zikiwemo hasi na chanya zinabainika kupitia matumzi yao ya mikakati ya upole.Vilevile, uchunguzi huu ulidhamiria kuzichunguza hali zinazoyaathiri matumizi ya mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*. Matokeo yanaonyesha kuwa, matumizi ya mikakati ya upole na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* yanaathiriwa na hali mbalimbali za kijamii kama vile mamlaka na malengo yao. Kwa jumla, utafiti huu umebainisha kuwa, upole una nafasi kubwa katika kuikamilisha kazi nzima ya tamthilia. Kupitia uchunguzi huu, imethibitika kuwa, kufanikiwa kwa maingiliano ya wahusika katika tamthilia kunategemea kiwango chao cha matumizi ya mikakati ya upole.

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA UTAFITI

**Upole**- Katika utafiti huu dhana hii imetumika kurejelea matumizi ya lugha ya mzungumzaji ambayo yanayodhihirisha heshima na hali ya kumjali msikilizaji.

**Mikakati ya upole**- Mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wahusika wanapozungumza ili kuzuia kuvunjika kwa mazungumzo yao.

**Vitendo vinavyotishia uso-** Kauli au matamshi ambayo yanaweza yakamkasirisha msemaji au msikilizaji wakati wa mazungumzo hivyo kusababisha kuvunjika kwa mazungumzo.

**Drama**- Matukio na vitendo vya wahusika katika mchezo wa kuigiza vinayodhamiria kuleta msisimko na mvuto kwa hadhira.

**Isimu matini-** Taaluma inayohakiki matini mbalimbali kwa kujikita katika kuchunguza jinsi vipashio mbalimbali vya kiisimu vuinavyochangia katika kuibua maana katika matini husika.

**Ubadhirifu**- hali ya matumizi mabaya wa mali. Ufujaji wa pesa

**Diskosi**- Usemi au kauli ya mhusika kama inavyojitokeza katika mkutadha fulani.

**Tashtiti-** Mbinu ya kisanaa ambapo mwandishi hutumia ucheshi kuikosoa jamii.

**Dhamira tegemezi-** Hali ya matumizi ya vitenzi vinavyodhihirisha ombi, mapendekezo, agizo na utohakika katika sentensi wakati wa mazungumzo.

**Uchanganuzi sifa-** Mbinu ya utafiti ambayo huhusisha ufafanuzi wa data kama inavyoonekana katika misingi ya rangi, tabia, jinsia, hadhi, hali au tabia yake.

**Kuwa bila rajua**- Hali ya mzungumzaji kudhihirisha matarajio hasi wakati wa mazungumzo. Mtazamo wa mtu katika mazungumzo ambao unamdhihirishia msikilizaji wake kuwa hatarajii matokeo mazuri ya jambo au tendo fulani.

**Mchakato-** Mkondo au mfumo wa kuzalisha au kuibua hali fulani.Ni mkondo mzima wa matukio au hali katika kuzalisha tabia, hali au matokeo fulani.

## YALIYOMO

**Ungamo** ... ii
**Tabaruku** ... iii
**Shukrani** ... iv
**Iksiri** ... v
**Maelezo ya Istilahi Muhimu kama Zilivyotumika Katika Utafiti** ... vi
**Yaliyomo** ... vii
**SURA YA KWANZA** ... 1
**1.1 Utangulizi** ... 1
1.2 Tamthilia ya *Mbaya Wetu* ... 2
1.3 Tatizo la Utafiti ... 3
1.4 Malengo ya Utafiti ... 4
1.5 Nadharia Tete ... 5
1.6 Umuhimu wa Utafiti ... 5
1.7 Upeo wa Utafiti ... 5
**1.8 Msingi wa Nadharia ya Utafiti** ... 6
1.8.1 Uso Hasi na Chanya ... 7
1.8.2 Vitendo Vinavyotishia Uso ... 8
**1.8.3 Mkakati Ndani ya Rekodi** ... 9
1.8.3.1 Katika Mahusiano ya Mamlaka ... 9
1.8.3.2 Katika Mazingira ya Dharura ... 10
1.8.3.3 Wakati Tendo Linalofanywa Linalenga Kumfaidi Msikilizaji ... 10
1.8.3.4 Wakati Washirika Wana Mahusiano ya Karibu ... 10
**1.8.4 Mkakati Nje ya Rekodi** ... 11
1.8.4.1 Utoaji wa Vidokezo Vielekezi ... 11
1.8.4.2 Usemaji wa Kauli Zenye Utata ... 12
1.8.4.3 Matumizi ya Kejeli yenye Ucheshi ... 12
**1.8.5 Mkakati Hasi wa Upole** ... 12
1.8.5.1 Matumizi ya Vidokezi Vinavyomtayarisha Msikilizaji Kimbele ... 13
1.8.5.2 Matumizi ya Maswali na Kauli za Kimzunguko ... 13
1.8.5.3 Kujidunisha na Kumtukuza Msikilizaji ... 13

1.8.5.4 Matumizi wa Mbinu ya Kujumlisha ... 14
1.8.5.5 Kutabiri Matarajio au Matokeo Hasi ... 14
1.8.5.6 Kudokeza Athari Hasi za Kitendo ... 14
**1.8.6 Mkakati Chanya wa Upole** ... 15
1.8.6.1 Kumtukuza na Kuonyesha Kumjali Msikilizaji ... 15
1.8.6.2 Kujitambulisha na Kundi Moja na Msikilizaji ... 15
1.8.6.3 Kudhihirisha Makubaliano na Kuepuka Kutokubaliana ... 16
1.8.6.4 Kudokeza Matokeo au Athari Chanya ... 16
1.8.6.5 Utoaji Miadi ... 17
**1.9.0 Yaliyoandikwa** ... 17
1.9.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Utafiti ... 17
1.9.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti ... 20
**1.10 Mbinu za Utafiti** ... 24
1.10.1 Uteuzi wa Sampuli ... 24
1.10.2 Mbinu za Kukusanya Data ... 25
1.10.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ... 25
**SURA YA PILI: MATUMIZI YA MIKAKATI YA UPOLE NA WAHUSIKA WAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *MBAYA WETU*** ... **27**
**2.0 Utangulizi** ... **27**
**2.1 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Upole** ... **27**
2.1.1 Kumtambua na Kumshughulikia Msikilizaji ... 28
2.1.2 Kutumia Vitambulisho vya Makundi ... 31
2.1.3 Kutafuta Makubaliano ... 32
2.1.4 Kuteua na Kuchangia Mada Inayomvutia Msikilizaji ... 34
2.1.5 Kutumia Ucheshi ... 36
2.1.6 Kujumuisha Msemaji na Msikilizaji Katika Kitendo ... 37
2.1.7 Kutoa Ahadi au Zawadi ... 39
**2.2 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Upole** ... **40**
2.2.1 Matumizi ya Vitangulizi na Vidokezi ... 41
2.2.2 Kutoa Kauli Zisizohusishwa na Mtu Maalum/Kuepuka Viwakilishi Nafsi ... 43
2.2.3 Kubashiri Matokeo Mabaya ya Kitendo ... 45

2.2.4 Kuonyesha Staha/Heshima Baina ya Msemaji na Msikilizaji ........................................... 48
2.2.5 Kutaja Kitendo Kinachotishia Uso Kama Kanuni ya Jumla................................................ 49
2.2.6 Kupunguza Ulazimishaji wa Kauli ...................................................................................... 50
2.2.7 Kuuliza Maswali ................................................................................................................... 52
**2.3. Matumizi ya Mkakati Nje ya Rekodi ................................................................................. 53**
2.3.1 Matumizi ya Maswali ya Balagha........................................................................................ 53
2.3.2 Matumizi ya Semi ................................................................................................................. 56
2.3.3 Kutoa Maelezo Pungufu katika Usemi ............................................................................... 58
2.3.4 Kuongea kwa Namna ya Mzunguko .................................................................................. 59
2.3.5 Kupuuza au Kubadilisha Mada ya Mazungumzo .............................................................. 61
**2.4 Matumizi ya Mkakati Ndani ya Rekodi................................................................................ 62**
**2.5 Hitimisho.................................................................................................................................. 66**
**SURA YA TATU: MIKAKATI YA UPOLE NA UKUZAJI WA WAHUSIKA WAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *MBAYA WETU* ........................................................................ 67**
**3.0 Utangulizi................................................................................................................................. 67**
3.1 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kuzikuza Sifa za Matari ......................................... 67
3.2 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kuzikuza Sifa za Lila ............................................. 69
3.3 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kuzikuza Sifa zaTemba.......................................... 73
3.4 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kuzikuza Sifa za Mama.......................................... 74
**3.5 Hitimisho.................................................................................................................................. 78**
**SURA YA NNE: HALI ZINAZOYAATHIRI MATUMIZI YA MIKAKATI YA UPOLE YA WAHUSIKA WAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *MBAYA WETU* ............................ 79**
**4.0 Utangulizi................................................................................................................................. 79**
**4.1 Mamlaka ya Mhusika Katika Jamii........................................................................................ 80**
4.1.1Matumizi ya Lugha na Mamlaka ya Mhusika Katika Familia ............................................. 80
4.1.2 Matumizi ya Lugha na Mamlaka ya Mhusika Katika Sheria .............................................. 82
4.1.3 Matumizi ya Lugha na Mamlaka ya Nguvu za Mwili ........................................................ 85
4.1.4 Matumizi ya Lugha na Hali ya Nguvu za Uchumi ............................................................. 86
**4.2 Matumizi ya Lugha Katika Kufanikisha Malengo ya Wahusika...................................... 88**
**4.3 Matumizi ya Lugha na Uhusiano waWahusika Katika Jamii.......................................... 91**
4.3.1 Matumizi ya Lugha na Uhusiano wa Wahusika Katika Familia ........................................ 92

4.3.2 Matumizi ya Lugha na Uhusiano wa Wahusika Kiumri na Kijinsia .................................. 94
4.3.3 Matumizi ya Lugha na Uhusiano wa Wahusika Katika Kazi .............................................. 96
**4.4 Hitimisho ......................................................................................................................... 97**
**SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ....................................................... 99**
**5.0 Utangulizi ........................................................................................................................ 99**
**5.1Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti** ........................................................................ 99
5.2 Changamoto za Utafiti ...................................................................................................... 109
5.3 Mapendekezo .................................................................................................................... 110
**MAREJELEO ......................................................................................................................... i**

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu unashughulikia suala la upole katika fasihi andishi ya Kiswahili kwa kuchambua jinsi ambavyo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanaitumia mikakati ya upole ili kufanikisha mazungumzo yao na wahusika wengine.Matumizi ya nadharia za kiisimu katika uchambuzi wa matini za fasihi limekuwa suala tata kwa muda mrefu. Hata hivyo, kuibuka kwa tapo la wanaisimu-matini katika miaka ya sitini ambao walianza kutumia nadharia za kiisimu kuchanganulia matini za fasihi kumeleta mabadiliko makubwa katika utanzu wa fasihi andishi. Kutokana na hali hii, taaluma ya pragmatiki imekuwa ikitumika kama kiungo muhimu katika kudhihirisha uhusiano uliopo baina ya fasihi na isimu. Hii ina maana kuwa, wanaisimu-matini wanaingalia lugha inayotumika katika matini kama kigezo cha kufafanulia matini husika katika misingi ya dhamira na maudhui. Kwa msingi huu, wanaisimu-matini hujikita katika kujaribu kuonyesha jinsi lugha inavyotumika kuvijenga vipengele mbalimbali vya matini.

Katika kipindi cha miaka ya sabini na themanini, nadharia za kiusemi kama vile Nadharia ya Upole zilianza kutumiwa katika kuchanganua matini za kibunilizi kama vile riwaya. Hii ina maana kuwa, katika miaka ya hapo awali lugha zungumzwa ilikuwa ikiangaliwa kama msingi wa tafiti nyingi zilizohusisha diskosi. Kufikia mwisho wa miaka ya themanini na tisini, wanaisimu-matini kama Biber na Finegan(1986), Swales(1990) na Halliday (1994) walianza kutilia maanani matumizi ya nadharia za kiisimu kuchanganulia ushairi na kupembeza tanzu nyinginezo za fasihi.Hali hii ilitokana na athari za nadharia za uhakiki mpya na uhakiki wa urasimi wa Kirusi ambazo ziliyaathiri mawazo ya watafiti wengi katika kipindi hiki. Hata hivyo, mabadiliko makubwa yameshuhudiwa katika miaka ya hivi karibuni ambapo tanzu nyinginezo za fasihi andishi kama vile riwaya, tamthilia na hadithi fupi zimeanza kuchambuliwa kwa kutumia nadharia za kiisimu.

Nadharia ya Upole ni mojawapo ya nadharia za kiisimu ambazo zimekuwa zikitumiwa kwa kipindi kirefu na wanaisimu- matini hasa wale wa ulaya. Wataalamu hawa wamekuwa wakijikita katika kuchambua diskosi na nyenzo mbalimbali za mawasiliano kama vile magazeti, sinema, makala katika runinga, mahojiano katika vyombo vya habari miongoni mwa diskosi nyinginezo. Katika tafiti hizi, lengo kuu limekuwa kutaka kubainisha ni kwa jinsi gani matumizi

ya lugha ya upole katika diskosi hizi yanachangia katika kudumisha na kuendeleza maingiliano na mlahaka mzuri baina ya washirika wa diskosi hizi.

Kwa mujibu wa Leech (1983:133), lugha hugawika katika makundi mawili makuu kutegemea matumizi yake.Makundi haya ni; lugha zungumzwa na lugha andishi. Leech anadai kuwa, kila mojawapo wa aina hizi mbili za lugha haiwezi ikatenganishwa na nyingine. Aidha Leech anasisitiza kuwa, ulimwengu wa kisasa hauwezi ukaeleweka pasi na kuwepo kwa aina hizi mbili za lugha kwa kuwa lugha hizi mbili hukamilishana na kujalizana. Kwa kifupi, Leech anasisitiza kuwa kila mojawapo ya lugha hizi huwa na dhima yake maalum katika jamii na ni makosa makubwa kwa mojawapo ya lugha hizi kuchukuliwa kuwa bora kuliko nyingine.

Kwa msingi wa uelewa huu, mtafiti anachunguza kipengele cha uhusika katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* ya Ken Walibora (2014) hasa kwa kubainisha jinsi ambavyo wahusika wakuu katika tamthilia hii wanavyoitumia mikakati ya upole katika kufanikisha mazungumzo yao. Katika utafiti huu, mtafiti anaongozwa na kipengele cha mikakati ya upole ambacho ni mojawapo ya mihimili muhimu ya Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987. Aidha,utafiti huu unashughulikia mada hii huku mtafiti akiwa na uelewa kuwa, tamthilia kama zilivyo kazi nyingi za kifasihi ni zao la uhalisia wa kijamii.Mwandishi kama sehemu ya jamii huimulika jamii na kubainisha uhalisia wa jamii husika kwa kuwaumba wahusika wake kwa namna wanavyoakisi sifa za wanajamii kupitia ufundi wa kisanaa.

### 1.2 Tamthilia ya *Mbaya Wetu*

*Mbaya Wetu* ni tamthilia iliyoandikwa na Ken Walibora (2014). Tamthilia hii inatumia mbinu ya tashititi kwa mapana ili kuonyesha athari za udekezwaji wa watoto na wazazi wao na athari za udekezaji huu kwa mhusika mwenyewe, familia yake na jamii kwa ujumla. Ni tamthilia ya kijamii ambayo inaweka wazi utepetevu na ulegevu uliozigubika asasi zetu za jamii kuazia ndoa, mahakama na sheria, familia na siasa. Mwandishi analenga kuibua uhalisia kuwa maovu mengi yanayopatikana katika jamii yana msingi wake katika malezi mabaya kutoka kwa familia, kuwa kuoza kwa jamii kunaanzia na uozo wa familia.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, mwandishi amewaumba wahusika kumi na sita ambao wanatumika kuashiria uhalisia na nafasi mbalimbali zinazoshikiliwa na wanajamii.Wahusika hawa ni pamoja na: Matari, Temba,Mama,Lila,Tonge,Vero,Fiona, Jefule,Bi Mkubwa,Akari I na II, Mtu I, II na III, Bi. Mkubwa na Mjakazi. Wahusika wakuu ni: Matari, Temba, Mama na Lila.

Matari amesawiriwa kwa namna hasi kutoka mwanzo hadi mwisho wa tamthilia. Katika mwisho wa tamthilia hii, ouvu wa Matari unafikia ukingoni baada ya kufungwa kifungo cha miaka ishirini na minne kufuatia shataka la kubaka na kuiba kwa mabavu.Mtafiti anatumia tamthilia hii kuchambua mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika hawa ili kubainisha ambavyo inasaidia katika kuyafanikisha mazungumzo yao na kuiendeleza drama kwa jumla.

### 1.3 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu unachunguza jinsi ambavyo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanaitumia mikakati ya upole katika maingiliano yao na wahusika wengine ili kufanikisha drama, matukio na hadithi kwa ujumla. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu upole na umuhimu wake katika kudumisha mahusiano baina ya msikilizaji na mzungumzaji wakati wa mazungumzo kwa kutumia nadharia ya Brown na Levinson (1987) katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, suala la upole halijachunguzwa kwa kina katika kazi za tamthilia na hasa katika fasihi ya Kiswahili ili kubainisha umuhimu wa matumizi ya upole katika kufanikisha mazungumzo na kuibua athari za kidrama kwa jumla. Hii ina maana kuwa, tafiti nyingi ambazo zimefanywa zimekuwa zikijifunga katika uchambuzi wa utanzu wa fasihi simulizi hasa vipera vya nyimbo na mazungumzo.

Baadhi ya tafiti hizi ni pamoja na utafiti wa Walubengo. A (2010).Walubengo alitumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) katika kutafiti suala la upole katika nyimbo na mawaidha katika sherehe za jando za jamii ya Wabukusu. Mtafiti huyu, alijikita katika kipengele cha mikakati ya kuokoa uso. Mtafiti mwingine aliyetumia nadharia hii ni, Kariithi.F. (2010) aliyeshughulikia mikakati ya upole katika lugha ya vijana na jinsi vijana wanajitambulisha katika makundi kwa kutumia lugha yao.

Utafiti wa Walubengo ulijikita katika vipengele muhimu vya fasihi simulizi ambavyo ni nyimbo na maigizo. Kariithi alijifunga na uchunguzi wa matumizi ya lugha yaani utendaji miongoni mwa kundi la kijamii na jinsi kundi hilo yaani vijana linavyotumia mikakati ya upole katika lugha yao ili kujitambulisha. Utafiti wa Kariithi uliegemea katika taaluma ya isimujamii hasa sajili ya vijana lakini ukaongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) katika kuchunguza matumizi ya lugha ya vijana.

Ni kutokana na kuwepo kwa pengo hili la kutozamiwa kwa suala la upole katika drama ya Kiswahili kwa kina ambapo utafiti huu unapata msingi wake. Katika utafiti huu, mtafiti anachunguza nafasi ya mikakati ya upole katika kufanikisha drama kwa kutumia tamthilia ya *Mbaya Wetu.* Katika kuchunguza suala hili, mtafiti anakusudia kuyapata majibu ya maswali yafutayo: Je, ni kwa nini mazungumzo ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* yanazidi kufanikiwa licha ya kuwepo kwa migogoro mbalimbali miongoni mwa wahusika hawa? Je, matumizi ya mikakati ya upole na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* yana mchango upi katika kuyadumisha mazungumzo yao? Je, mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia hii inachangia vipi katika kuibusha sifa zao? Na je, ni hali zipi zinazoyaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Katika kuchunguza jinsi wahusika wakuu wanavyotumia mikakati ya upole katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* mtafiti anaongozwa na malengo yafuatayo:

1. Kubainisha iwapo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanatumia mikakati ya upole wanapoingiliana na wahusika wengine ili kufanikisha mazungumzo yao.
2. Kuchunguza jinsi mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* inavyochangia katika kuzikuza sifa zao.
3. Kutambua hali zinazoyaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.*

## 1.5 Nadharia Tete

1. Wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanatumia mikakati mbalimbali ya upole ili kufanikisha mazungumzo wanapoingiliana na wahusika wengine.
2. Mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* inachangia katika kuzikuza sifa zao.
3. Hali za jamii kama vile umri, jinsia, mamlaka na malengo ya wahusika zinayaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.*

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unahusu uchambuzi wa mikakati ya upole kama inavyotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* ili kufanikisha mazungumzo yao, kufanikisha drama, na hadithi kwa jumla. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa na mchango kwa wasomi na watafiti wa lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali.Kwanza, kupitia utafiti huu, watafiti wengine katika lugha ya Kiswahili watatiwa motisha na kupata mwelekeo wa kuchambua diskosi na kauli mbalimbali za wahusika katika kazi nyinginezo za fasihi kama vile riwaya, novela na hadithi fupi.

Pili, utafiti huu utawafaa watafiti na wasomi wa lugha ya Kiswahili katika kufahamu na kubainisha jinsi wanajamii mbalimbali hutumia mikakati ya upole, ama ni kutokana na tukio la makusudi au tukio la sadifa. Tatu, utafiti huu utawasaidia wasomi wa Kiswahili na wanajamii kwa ujumla katika kutambua namna aina mbalimbali za miktadha ya kijamii huathiri wanajamii katika kuteua mikakati mbalimbali ya upole wanapoingiliana katika mazungumzo. Kadhalika, katika kiwango cha shule za upili, walimu na wanafunzi watanufaika na utafiti huu kwa mapana. Hii ni kwa vile, wanafunzi hawa watapata maarifa zaidi ya jinsi ya kutambua sifa za wahusika katika matini za fasihi pamoja na mchango wa hali mbalimbali za jamii katika kuathiri matumizi ya lugha ya wahusika hawa.

## 1.7 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu unachunguza jinsi ambavyo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanatumia mikakati ya upole katika kufanikisha mazungumzo yao. Mtafiti anajikita katika taaluma ya isimu-matini katika kuchunguza jinsi wahusika hawa wanafanikiwa kuingiliana na wahusika wengine kupitia lugha licha ya kuwepo kwa hali ya migogoro mbalimbali baina yao.

Mtafiti anaongozwa na mhimili muhimu wa mikakati ya upole kama unavyoelezwa katika Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987).

Kadhalika, katika utafiti huu, mtafiti anajifunga katika kuwashughulikia wahusika wakuu pekee ili kubainisha wanavyoitumia mikakati ya upole katika kufanikisha mazungumzo yao kwa vile: Kwanza, wahusika wakuu wanajitokeza kutoka mwanzo wa tamthilia hadi mwisho. Kwa msingi huu, wahusika hawa wamepewa nafasi kubwa ambayo inawawezesha kuingiliana na takriban wahusika wengine wote tamthiliani. Pili, mtafiti analenga kuchunguza matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika hawa kwa ndani. Hivyo, matumizi ya wahusika wakuu pekee yanampatia nafasi nzuri zaidi ya kuwatafiti kuliko vile ambavyo ingekuwa angewashughulikia wahusika wote tamthiliani.Wahusika wakuu ambao mtafiti anachunguza matumizi yao ya mikakati ya upole ni pamoja na: Matari, Mama, Temba na Lila. Mtafiti amewaacha wahusika wadogo na wajenzi katika utafiti huu kwa vile wanatokea katika miktadha finyu tamthiliani hivyo kauli zao hazitatosheleza malengo ya utafiti wake.

Kando na hayo, utafiti huu unachunguza matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu kupitia lugha zungumzwa pekee. Hii ina maana kuwa, mtafiti anajikita katika kuchunguza jinsi wahusika hawa wanavyojieleza ama kuwaeleza wahusika wengine kupitia matumizi yao ya lugha. Kwa msingi huu, kauli za wahusika hawa ndizo zitakazotiliwa maanani ili kuzianisha katika misingi ya mikakati mbalimbali ya upole.

### 1.8 Msingi wa Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya Upole iliasisiwa na Brown na Levinson (1987). Nadharia hii imesalia kuwa mhimili muhimu katika tafiti nyingi za kisasa kando na kuwa chanzo cha nadharia nyingine zinazohusiana na upole. Baadhi ya wanaisimu ambao wamezijenga kazi zao kutokana na mawazo ya nadharia hii ni pamoja na: Fraser (1990) Scollon na Scollon (1995), Spencer-Oatey (2000) na Watts (2003). Watalamu hawa wameyahakiki mawazo ya Brown na Levinson (1987) kwa kuangalia dhana yao ya uso na mikakati ya upole katika mikabala tofautitofauti. Hata hivyo, wanakubaliana na mawazo ya Brown na Levinson kuhusu dhana ya uso chanya na uso hasi. Aidha, wanayakuza mawazo ya Brown na Levinson kuhusu mikakati mbalimbali ya upole

inayotumiwa na mzungumzaji katika kuokoa uso hasi na uso chanya wa msikilizaji wakati wa mazungumzo.

Brown na Levinson (1987) walitumia mawazo ya dhana ya uso kama ambavyo ilikuwa imeelezwa na Goffman (1967) kuibuni nadharia ya upole ya uso. Kwa mujibu wa Goffman (1967:5), uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na mtazamo ambao wengine huchukulia kuwa ameegemea katika mtagusano fulani. Uso ni dhana bia na ni sura ya kibinafsi inayohusishwa na sifa za kijamii. Aidha, Goffman (1967:9) anasema kuwa, kutunza uso humfanya mtu kuhisi vizuri kwani tunakuwa na uhusiano wa kihisia na uso ambao tunatunza. Kulingana na Goffmana, kupoteza uso kunasababisha kupotea kwa mhimili wa kihisia ambao huhifadhiwa katika hali za kijamii. Kwa kuwa athari za kihisia za kupoteza uso zinaweza kuwa dhabiti, watu mara kwa mara hushiriki katika vitendo vya kuokoa nyuso zao na za wengine katika mazungumzo.

Katika kuuendeleza mjadala wa Goffman kuhusu uso, Brown na Levinson (1987:61) wanaeleza dhana ya uso kama sura ya mtu binafsi ya kijamii ambayo mtu huichukulia kuwa yake. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, kila binadamu ana nyuso mbili, uso chanya na uso hasi. Nyuso hizi mbili zinaelezwa kwa msingi wa matamanio ambayo kila mwanajamii huwa nayo.Aidha, kila mwanajamii hutambua matamanio ambayo mwenzake hutamani yazingatiwe wakati wa mawasiliano. Yule (1996:60), anasema kuwa, istilahi ya upole katika isimu haina maana ya upole kama unavyoeleweka na wanajamii kama tabia ya kijamii ama katika msingi wa utamaduni bali huelezwa kwa kutegemea dhana ya nyuso za washirika.

### 1.8.1 Uso Hasi na Chanya

Katika Nadharia ya Upole, Brown na Levinson (1987:62) waligawa dhana ya uso kuwili lakini kwa namna na hali zinazoingiliana; uso hasi na uso chanya. Walieleza nyuso hizi mbili kwa msingi wa mahitaji au matamanio ambayo kila binadamu huwa nayo na ambayo hufanya kila jitihada kuhakikisha yanathaminiwa. Pia, Brown na Levinson wanaelezea kuwa, wakati ambao tendo la usemi linaenda kinyume na matarajio au matamanio ya uso wa msikilizaji, kunatokea vitendo vinavyotishia kuhasiriwa kwa nyuso chanya na hasi za washirika katika mazungumzo. Katika kundeleza mjadala wa Brown na Levinson, Yule (1996: 61-62), anasema kuwa, uso hasi

huhusisha matamanio ya mtu kuwa huru, kuwa na uhuru wa kutenda na kuwa na uhuru wa kutolazimishwa na wengine. Kwa upande mwingine, mtaalam huyu anaueleza uso chanya kama matamanio ya mtu kukubalika au kushirikishwa, na pia kuthaminiwa na wengine kwa kutambuliwa kama sehemu ya kundi la kijamii.

Brown na Levinson wanaendelea kudai kuwa, kila mzungumzaji huwa na urazini au uelewa wa awali katika akili yake kuwa msikilizaji anaweza akaathiriwa na tendo lake la kiusemi hivyo hujua mchakato huu kutoka mwanzo hadi mwisho.Kwa msingi huu, mzungumzaji huwa na urazini wa kimbele wa kung'amua kuwa mzungumzaji ana nyuso mbili ambazo zinahitaji kutambuliwa. Brown na Levinson wanasema kuwa, mzungumzaji hujitayarisha kwa kubuni mikakati mbalimbali ya upole kabla ya kutekeleza tendo lolote litishialo kuhasiri uso.

### 1.8.2 Vitendo Vinavyotishia Uso

Brown na Levinson (1987:65) wanafafanua kuwa, kuna matendo yanayoweza kutishia au kuzihasiri nyuso za washirika wa mazungumzo ambao ni pamoja na msikilizaji na mzungumzaji. Matendo ambayo yanaweza yakatishia uso hasi wa msikilizaji ni kama vile: kuamrisha, kutoa maagizo, kuonya na kutoa ushauri kwa msikilizaji. Aidha, kuna matendo ambayo yanahasiri uso chanya wa msikilizaji ambayo ni pamoja na: kutusi, kukashifu, kudunisha,vitisho, mada-mwiko hasa zilizokatazwa na utamaduni wa msikilizaji, urejeleaji wa jinsia ya msikilizaji kwa namna hasi, na kumdunisha msikilizaji kihadhi miongoni mwa vitendo vingine.

Kwa upande mwingine, kuna matendo ambayo huhasiri uso hasi wa mzungumzaji kama vile: kuridhia au kukubali maoni na mapendekezo ya msikilizaji, kukubali msamaha kutoka kwa msikilizaji, kukubali ombi la msikilizaji, kutoa miadi au ahadi fulani kwa msikilizaji bila hiari yake, kukubali wito wa msikilizaji, kukubali ushauri wa msikilizaji miongoni mwa vitendo vingine.

Matendo ambayo hutishia uso chanya wa msemaji ni kama vile: kuomba kutendewa jambo fulani na msikilizaji, kuomba msamaha kutoka kwa msikilizaji, kukubali shukrani kutoka kwa msikilizaji, kukiri makosa kwa msikilizaji, kujidunisha mbele ya msikilizaji, kuomba nafasi kutoka kwa msikilizaji miongoni mwa matendo mengine.

Katika kukabiliana na hali au matendo ya kutishia uso, Brown na Levinson wanadai kuwa kuna mikakati minne ambayo hutumiwa wakati wa mazungumzo.Mikakati hii hutumiwa na washirika katika mazungumzo ili kuepuka kudhuru nyuso zao wakati wa kutenda matendo ya kutishia uso. Kulingana na Brown na Levinson (1987: 68), mikakati ya upole hubuniwa ili kuepuka kudhuriwa kwa uso. Wanaueleza uso kama heshima ambayo mtu binafsi huwa nayo na ambayo hutarajia kudumishwa na wengine katika mikitadha ya umma na ya kibinafsi.Mikakati hii ya upole huweza kutumiwa kwa pamoja kutegemea hali na miktadha wanayojikuta kwayo washiriki wa mazungumzo wakati wa mawasiliano. Mikakati hii ni pamoja na:

### 1.8.3 Mkakati Ndani ya Rekodi

Huu ni mkakati ambao hutumika kwa mapana katika mawasiliano ya kila siku kwa vile mazungumzo ya wanajamii huhusisha kauli za moja kwa moja. Mkakati huu hutumiwa na wanajamii hasa wakiwa wanafahamiana au wana uhusiano wa aina fulani. Kulingana na Brown na Levinson (1987:67), mkakati wa upole ndani ya rekodi hufuata kanuni za utaratibu wa mawasiliano kama ambavyo zinaelezwa na Grice (1975). Kwa msingi huu, wakati wa kutumia mkakati huu msikilizaji huzungumza kwa namna ya moja kwa moja, bila utata na kwa namna ambayo ni wazi kabisa. Katika kutumia mkakati huu, msemaji huwa halengi kuhifadhi uso wa msikilizaji ila hulenga kuwasilisha ujumbe fulani. Kutokana na hali hii, mkakati huu huweka msisitizo wake katika uwasilishaji wa ujumbe na wala si katika uhifadhi wa uso. Wanajamii hutumia mkakati huu katika mazingira mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

#### 1.8.3.1 Katika Mahusiano ya Mamlaka

Mkakati huu hutumika katika mazingira ambayo msemaji na msikilizaji wanatenganishwa katika uhusiano na mamlaka au uwezo fulani.Kwa mfano, wakati msemaji ana mamlaka au nguvu zaidi ya msikilizaji hivyo msemaji anaweza akamwamrisha au kumwagiza msikilizaji. Kwa mfano, katika maingiliano baina ya bwana na kitwana au kijakazi; bwana anaweza akamwamrisha mjakazi au kitwana wake kutenda jambo fulani moja kwa moja.Kwa mfano:

1. Bwana: Njoo hapa haraka!
2. Kitwana: Nimeshafika bwana ungetaka nifanyeje.
3. Bwana: Waletee wageni chai mara moja.

Katika muktadha huu, lengo ni kuwasilisha ujumbe bila kuzingatia hali ya uso chanya na hasi wa msikilizaji jambo linalotakana na uhusiano baina ya bwana na kitwana.

Aidha, mkakati huu huweza kutumika katika mazingira ya shuleni ambapo mwalimu huweza kuwaamrisha au kuwaagiza wanafunzi wake kufanya au kuzingatia jambo fulani. Katika muktadha huu, mwalimu hatawaliwi na kaida ya kutaka kuuhifadhi uso wa wanafunzi wake. Kwa mfano mwalimu anaweza akawaelekeza wanafunzi wake hivi:

4. Kufikia jioni vitabu vyote viwe vimefikishwa ofisini mwangu.

Huu ni mkakati wa moja kwa moja ambao unajibainisha kutokana na nafasi za kutawala zinazoshikiliwa na wanajamii.

### 1.8.3.2 Katika Mazingira ya Dharura

Mkakati wa upole ndani ya rekodi pia hujibainisha pale ambapo kuna hali ya dharura ambayo mzungumzaji anamtaka msikilizaji kuizingatia kwa haraka. Msemaji anaweza akamwambia msikilizaji:

5. Chunga pesa zako hapa kuna masinzia wengi.

Lengo la msemaji wa kauli katika mfano 5 ni kujali maslahi ya msikilizaji kwa kumtahadharisha na masinzia hivyo hana haja ya kuzingatia upole kumfahamisha hili.

### 1.8.3.3 Wakati Tendo Linalofanywa Linalenga Kumfaidi Msikilizaji

Kadhalika, mkakati wa upole ndani ya rekodi hutumika pale ambapo tendo ama kauli inayowasilishwa na msemaji hulenga kumfaidi msikilizaji kama vile katika mfano ufuatao:

6. Njoo na kikombe nikutilie chai.

Kwa kuzingatia kauli katika mfano 6, inabainika kuwa suala la upole haujazingatiwa kwa vile dhamira ya kitendo cha msemaji ni kumfaidi msikilizaji. Kwa msingi huu, japo upole haujidhihirishi moja kwa moja inachukuliwa kuwa huu ni mkakati wa upole kwa vile kitendo kinalenga kudumisha na kufurahisha uso chanya wa msikilizaji.

### 1.8.3.4 Wakati Washirika Wana Mahusiano ya Karibu

Mkakati wa upole ndani ya rekodi pia hujibainisha pale ambapo washirika katika mazungumzo wana uhusiano wa karibu. Kwa kawaida, mkakati huu hudhihirika katika mazungumzo baina ya

mahirimu, wanafamilia na marafiki au watu wanaofahamiana kwa mapana. Kwa mfano, marafiki wanaweza wakaamrishana, kuagizana na hata kutumana bila kuzingatia upole kutokana na ukweli kuwa wana uhusiano wa karibu. Kwa mfano rafiki anaweza akamwambia mwenzake:

7. Ukifika dukani uniletee vitabu vitatu vya kuandikia, hakikisha kuwa hutasahau.

Kauli katika mfano 7 haichukuliwi na msikilizaji kama tendo la kutishia uso kwa sababu ya uhusiano wake na msemaji.

**1.8.4 Mkakati Nje ya Rekodi**

Katika kutumia mkakati wa upole nje ya rekodi, msemaji huwa hawasilishi ujumbe wake kwa msikilizaji kwa njia au namna ya moja kwa moja. Kwa msingi huu, mzungumzaji hutumia maneno au kauli zinazodhamiria au kumdokezea msikilizaji lengo au kusudio lake. Mkakati huu humwachia msikilizaji nafasi kubwa ya kujijazia anachokusudia msemaji. Hivyo, huu ni mkakati ambao una misingi yake katika uelewa na ufasili wa maana wa msikilizaji katika kufafanua kinachosemwa.

Brown na Levinson (1987:211) wanaeleza kuwa, mkakati nje ya rekodi unakabiliwa na hatari ya ufasili potovu wa maana na msikilizaji kwa vile huwa si wa moja kwa moja.Vilevile,Wataalam hawa wanafafanua kuwa, mkakati huu huzivunja kanuni za utaratibu wa ushirikiano kama zinavyoelezwa na Grice (1975). Kwa msingi huu, msikilizaji hutarajiwa kuwa na elimu-awali au uelewa wa kile kinacholengwa na msemaji hasa kwa kurejelea kwa kina vidokezo katika kauli ya msemaji.Brown na Levinson (1987:213-227),wanafafanua mbinu mbalimbali zinazotumiwa wakati wa kuokoa uso hasi kwa kutumia mkakati nje ya rekodi ifuatavyo:

**1.8.4.1 Utoaji wa Vidokezo Vielekezi**

Kutoa vidokezo muhimu ambavyo vitamwelekeza msikilizaji malengo ya msemaji ni mojawapo wa mbinu zinazotumika katika utendaji vitendo vya kutishia uso nje ya rekodi. Kwa mfano, badala ya msemaji kusema moja kwa moja kuwa anahisi njaa apewe chakula, anaweza akamdokezea msikilizaji wake kwa kusema:

8. Najihisi mnyonge, sijala tangu jana jioni.

Katika kufasili maana ya kauli hii msikilizaji atatambua kuwa msemaji anaomba chakula.

### 1.8.4.2 Usemaji wa Kauli Zenye Utata

Mkakati huu pia huhusisha utaoji wa kauli ambazo zina utata. Kwa msingi huu, msemaji huzua kauli fulani yenye maana mbalimbali kwa msikilizaji na kumwachia msikilizaji kujijitafutia maana lengwa. Kwa mfano msemaji anaweza akasema:

9. Alama yako ya mtihani haikuridhisha sana muhula huu, inaonekana ulikuwa na shughuli nyingi.

Katika kauli hii, msemaji hataki kusema moja kwa moja kuwa msikilizaji alianguka mtihani na kuwa kuanguka kwake kulitokana na sababu ya kutosoma. Badala yake, anamtafutia kijisababu cha kutopita mtihani.Aidha, msemaji anadai matokeo hayakuwa ya kuridhisha badala ya kudai moja kwa moja alifeli. Mkakati huu unalenga kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji.

### 1.8.4.3 Matumizi ya Kejeli yenye Ucheshi

Kadhalika, mkakati huu hubainika kupitia matumizi ya mbinu ya kejeli lakini kwa namna chanya hali ambayo inaingiliana na mawazo ya Leech (1983:144) kuhusu kinaya na banta. Leech anaeleza kuwa, mzunguzaji anaweza akawasilisha ujumbe hasi kwa msikilizaji kwa kutumia lugha ambayo haidhihirishi uhasi huu kwa njia ya moja kwa moja.Leech pia anaeleza kuwa, kanuni ya banta huzivunja kanuni za ushirikiano kama zinavyoelezwa na Grice (1975). Kwa mfano, mwanafunzi aliyefeli mtihani anaweza akambiwa hakufeli sana ikitiliwa maanani kuwa yeye hufanya vizuri kwenye spoti kuliko masomo. Kejeli itakuwa imebainika katika kauli hii iwapo mwanafunzi huyu si mwanaspoti. Hivyo basi, mkakati huu hutumika katika kuwasilisha kauli zenye dhihaka.

### 1.8.5 Mkakati Hasi wa Upole

Huu ni mkakati ambao hulenga kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji hasa kwa kupunguza makali na hali ambazo zinaweza kutishia uso wa msikilizaji.Matumizi ya mkakati huu hutokana na hali ambapo mzungumzaji anahitaji kitu,msaada, jambo au uhisani kutoka kwa msikilizaji lakini mzungumzaji hataki kumwonyesha msikilizaji kuwa anamlazimisha. Msemaji huelewa fika kuwa, msikilizaji ana haki ya kukataa hivyo hulazimika kutumia mkakati unaodhihirisha upole. Mzungumzaji hufahamu kuwa ombi lake kwa msikilizaji huenda likazua aibu au hali ya hasira hivyo kuepuka kuwasilisha matamanio yake kwa njia ya moja kwa moja. Brown na Levinson

(1987:131), wanaeleza mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika kutekeleza tendo la kutishia uso kupitia mkakati hasi wa upole.

### 1.8.5.1 Matumizi ya Vidokezi Vinavyomtayarisha Msikilizaji Kimbele

Katika kutumia mbinu hii, mzungumzaji hutumia vitangulizi ambavyo vinamdokezea msikilizaji kuwa anachodhamiria kusema si kizuri kwake hivyo kumtayarisha kwa kutumia vidokezo. Katika kufanya hivi, mzungumzaji anaweza akatumia vitangulizi kama:

10. Ashakum si matusi mavazi yako yanaonyesha uchi wako.
11. Pole kwa kusema hili ila tabia yako haiwafurahishi wazazi wako hata kidogo.
12. Naomba msamaha kwa kusema haya, vijana wa kisasa hawana nidhamu hata kidogo.
13. Si nia yangu kusema hili bali nitalisema kwa vile limeshatokea.
14. Niwie radhi kwa kusema hivi wewe ni mwizi.

### 1.8.5.2 Matumizi ya Maswali na Kauli za Kimzunguko

Kadhalika, mkakati huu huhusisha matumizi ya mbinu ya mzunguko inayotambulishwa na kuwepo kwa maneno yanayoashiria dhamira tegemezi. Kwa mfano:

15. Nilikuwa nashangaa iwapo itakuwa vyema kwa sasa tukifumukana kwa vile muda umesonga sana.
16. Sijui kama itawezekana ikiwa utaweza kunikopesha shilingi mia tano kwa sasa.

Pia, huhusisha matumizi ya maswali ya mdokezo kama vile:

17. Sijui iwapo itawezekana unisaidie na shilingi hamsini.
18. Mbona tusipike wali kwa vile tumemaliza kazi.

### 1.8.5.3 Kujidunisha na Kumtukuza Msikilizaji

Aidha, mkakati hasi wa upole huhusisha mzungumzaji kujidunisha na kumtukuza msikilizaji ili kuonyesha tofauti zilizopo baina yake na msikilizaji. Hali hii inaingiliana na mawazo ya Leech (1983:144) kuhusu kanuni za kudumisha mawasiliano hasa ile kanuni ya kujitweza. Katika mbinu hii, msikilizaji hufanywa kujihisi bora au kuwa katika nafasi ya kufanya au kutekeleza wajibu fulani akilinganishwa na mzungumzaji. Kwa msingi huu, mkakati huu hulenga kuendeleza na kukuza uso chanya wa msikilizaji.Kwa mfano:

Kutambua mtu kwa cheo, Bwana, Bi. Mstahiki, mhadhiri, profesa.Pia, kumtayarisha kimbele kwa kumsifu:

19. Najua wewe ni mtu wa shughuli nyingi lakini sasa…
20. Wewe najua huwezi ukashindwa na hesabu ya aina hii kama sisi…
21. Siku hizi nimekuwa mjinga ninasahau ovyo ovyo…unaweza kunikumbusha...

### 1.8.5.4 Matumizi wa Mbinu ya Kujumlisha

Ujumuishaji ni mbinu nyingine ambayo hutumika katika kufanikisha mkakati hasi wa upole. Ujumuishaji huhusisha kanuni ya jumla ambayo huchukulia kuwa kinachosemwa au kuwasilishwa kinahusisha hadhira au kundi nzima la watu badala ya kumwagazia mhusika mlengwa binafsi. Mzungumzaji huchukulia kuwa, katika kujumlisha wahusika wote huwa amekwepa kuuhasiri uso hasi wa mlengwa mahususi na wakati uo huo kuchukulia kuwa anachokisema kimempata mlengwa wake kwa vile anajijua iwapo alidhamiria hivyo.

### 1.8.5.5 Kutabiri Matarajio au Matokeo Hasi

Mkakati hasi wa upole pia huhusisha mbinu ya kuonyesha matarajio au matokeo hasi ya ombi au majibu ya msikilizaji. Hapa msemaji humtayarisha msikilizaji kuyapokea mtokeo hasi na wakati uo huo kumdhihirishia lengo lake japo anafahamu kuwa huenda ikawa hatakuwa na uwezo wa kufanya vile kwa mfano:

22. Najua huna uwezo wa kunisaidia kwa sasa lakini…
23. Sidhani kama una jibu la swali hili lakini wacha nikuulize tu…
24. Naelewa hali yako ya kifedha ya sasa lakini itakuwa vyema ikiwa….

### 1.8.5.6 Kudokeza Athari Hasi za Kitendo

Aidha, mkakati hasi wa upole huhusisha matumizi ya mbinu ya kuonyesha athari mbaya za kitendo fulani badala ya kurejelea kitendo chenyewe. Mbinu hii pia huhusisha matumizi ya kauli za jumla zinazochukuliwa kuwa ukweli bia ambao unakubalika na kila mwanadamu. Kwa mfano mzungumzaji anaweza akatumia maneno kama vile:

25. Kila binadamu anafaa kuwajibika…
26. Ni hatari kwa mwanafunzi kukataa kutii walimu na wazazi wake..
27. Matokeo mabaya katika mitihani ya kitaifa humplekea mtu kukosa nafasi katika chuo kikuu

Aidha, mkakati huu huweza kutumia methali, kauli biu na misemo mingine ambayo hukusudiwa kuwasilisha ujumbe fulani lakini kwa namna isiyo wazi.

### 1.8.6 Mkakati Chanya wa Upole

Mkakati huu hulenga kudumisha uso chanya wa msikilizaji kwa kuepuka kufanya au kusema habari zinazoweza kumuudhi msikilizaji au kuhasiri uso wake chanya.Vilevile, mkakati huu kwa mapana hulenga kuusifu na kuufurahisha uso chanya wa msikilizaji kabla ya kufanya vitendo vya usemi. Jukumu kuu la mzungumzaji huwa ni kumtukuza, kumheshimu na kumrai msikilizaji kiasi cha yeye kujihisi kuwa wa maana na thamani kubwa.

Kadhalika, kupitia matumizi ya mkakati chanya wa upole mzungumzaji hulenga kuibua, kukuza na kuyapalilia mazingira ambayo yatadumisha mahusiano baina ya washiriki wa mazungumzo, hivyo hutawaliwa na utoaji mwingi wa miadi chanya. Mkakati huu huingiliana na mawazo ya Lakoff (1973) kuwa jukumu kuu la washirika katika mchakato mzima wa mawasiliano ni kudumisha mazingira ya uwiano kwa kujaribu kuepuka hali zinazoweza kuyavunja mawasiliano na kuwa, kudumisha mawasiliano ni muhimu kuliko kuzingatia upole. Mkakati huu hutumia mbinu zifuatazo katika kufanikisha lengo la mzungumzaji:

#### 1.8.6.1 Kumtukuza na Kuonyesha Kumjali Msikilizaji

Mbinu hii huhusisha hali ya kumtambua msikilizaji kwa kumshughulikia kwa namna ambayo atahisi kuwa anaenziwa na kuthaminiwa. Hali hii humfanya ahisi vizuri kwa kuufurahisha uso wake chanya. Pia, mzungumzaji anaweza kumtambua msikilizaji kwanza kwa kukisifu kitendo alichokifanya, kuyasifu mavazi yake, kuisifu sura yake, kutambua hadhi yake au hata kusifu mali yake. Kwa mfano mzungumzaji anaweza kusema hivi:

28. *Hongera kwa suti mpya sasa unaweza ukahudhuria mikutano yote bila wasiwasi*..
29. Hiyo tarakilishi yako mpya itakufaa sana katika shughuli zako za utafiti… safari hii hakuna kama wewe…
30. Sisemi kitu kuhusu mtindo wako mpya wa nywele…siuoni na wengi…
31. Ni kitambo sana tangu tushiriki staftahi pamoja…hatuwezi tukapitwa na nafasi hii…

Katika kuambiwa kauli hizi, msikilizaji anahisi kuwa anathaminiwa na kukubalika na msemaji.

#### 1.8.6.2 Kujitambulisha na Kundi Moja na Msikilizaji

Aidha, mkakati huu hudhamiria kumthamini msikilizaji kwa kumtambulisha na kundi au kikundi fulani (hali ya kuwa pamoja) maarufu. Makundi haya yanaweza kuwa na uhusiano katika misingi

ya umri, jinsia, siasa, jamii, utamaduni au matabaka. Majina ya sifa yanayoendana na utambulisho wa kimakundi ni pamoja na: Rafiki yangu/yetu, mwenzangu, mwanachama mwenzangu, ndugu yangu, mwenzetu, kaka yetu, dada yetu, baba yetu miongoni mwa majina mengine.

#### 1.8.6.3 Kudhihirisha Makubaliano na Kuepuka Kutokubaliana

Mkakati huu pia huhusisha uhifadhi wa uso chanya wa msikilizaji na msemaji kwa kuyapalilia mazingira ya makubaliano hasusan kwa kuteua mada ambayo msikilizaji anaijua, anaipenda au inahusiana naye. Mbinu hii huchukulia kuwa, mzungumzaji ana uelewa wa awali wa mambo ambayo msikilizaji anayafahamu na kukubaliana nayo hivyo mzungumzaji huibuka na mada ambayo anaelewa fika kuwa msikilizaji anaifahamu na kukubaliana nayo. Kwa kufanyiwa hivi, msikilizaji huhisi kuwa anakubalika na mchango wake kukubalika pia.

Mkakati huu aidha huhusisha uepukaji wa kauli na mielekeo ambayo inadhihirisha kupinga msikilizaji au kupinga kauli zake. Uepukaji huu unamfanya msikilizaji ahisi kuwa anathaminiwa au anakubalika. Pia, mkakati huu huhusisha kukubaliana na msemaji katika mapendekezo yake na iwapo msikilizaji atayakataa ayakatae kwa namna inayodhihirisha sababu ya kukataa kutekeleza pendekezo lake. Hapa, msikilizaji huepuka kumpinga msemaji kwa njia ya moja kwa moja hasa kwa kuonyesha sababu ya kutowezekana kwa jambo lakini kwa namna ya kukubali kwanza. Kwa mfano msikilizaji anaweza akajibu ombi la mwaliko kama ifuatavyo:

32. **Mhusika A**: Leo utapitia nyumbani kwangu kwa chakula cha mchana.
    **Mhusika B:** Ndio ninaweza japo ninaweza nikashindwa kwa sababu ninasomea mtihani wa kesho asubuhi.

#### 1.8.6.4 Kudokeza Matokeo au Athari Chanya

Kadhalika, mkakati huu huhusisha uwekaji wazi au ubainishaji wa tokeo au jibu la swali la msikilizaji kwa pendekezo lake (mzungumzaji). Katika mbinu msemaji hudhihirisha matumaini kuwa msikilizaji atamfanyia jambo fulani hasa kwa kutumia vishikizo (question tag) mwishoni mwa kauli. Kwa mfano:

33. Leo utanitembelea. Sivyo?
34. Sioni ni kwa nini tusianze safari kwa sasa. Si ni vyema?
35. Kila mtu ameridhika. Au?

Katika kauli zilizopo hapo juu, tayari msemaji amedokeza msimamo wake japo si kwa njia ya moja kwa moja. Msimamo wake unaonekana kushadidiwa na ulazimishaji wake wa kukubalika kwa pendekezo lake hasa kwa kutumia maswali mwishoni mwa kauli. Aidha, msemaji anatumia sentensi zenye kuonyesha dhamira tegemezi (subjunctive mood) katika kauli zake. Msikilizaji ananui kuepuka kuudhi uso chanya wa msikilizaji kwa kutosema mapendekezo yake kwa njia ya moja kwa moja.

### 1.8.6.5 Utoaji Miadi

Mkakati huu pia huhusisha mbinu ya utoaji miadi chanya kwa msikilizaji ili kumfurahisha kama vile kuahidi kumnunulia msikilizaji zawadi. Kwa mfano:

36. Sitakutembelea leo lakini kesho nitakuja nishinde kwako siku nzima.
37. Nikifika dukani nitakununulia nguo maridadi.

Katika mfano 36 msemaji anakataa pendekezo la msikilizaji lakini kwa kutoa ahadi ya kuja kesho hapa anaepuka kuhasiri uso chanya wa msikilizaji. Mfano 37 unadhihirisha matumizi ya upole chanya ili kuokoa uso chanya wa msikilizaji kwa kutoa ahadi ya kununua nguo maridadi.

## 1.9.0 Yaliyoandikwa

### 1.9.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Utafiti

Watalamu wengi wamefanikisha kuibuka, kukua na kuendelea kwa Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson. Baadhi kama vile Grice (1975) na Leech (1983) wameiwekea msingi wa kimawazo nadharia hii ilhali wengine kama vile Spencer (2000) na Watts (2003) wameihakiki na kuiendeleza. Katika sehemu hii, mtafiti anashughulikia mawazo ya wataalam hawa kuhusu mchango wao katika nadharia hii pia katika utafiti huu kwa jumla. Grice (1975) aliuangalia upole kama mkakati wa mazungumzo kuwa, washirika katika mazungumzo huongozwa na kanuni ambazo huhakikisha kuwa utaratibu fulani unazingatiwa katika mawasiliano. Utaratibu huu ndio huwezesha washirika katika mazungumzo kudumisha mawasiliano yao na pia kuyaendeleza. Grice alidai kuwa washirika katika mazungumzo huwa na akili razini ambazo huwawezesha kuzingatia kanuni hizi bila kuvunja mawawasiliano. Kulingana na yeye, mawasiliano yoyote yale huongozwa na utaratibu wa ushirikiano ambao hujumuisha kanuni mbalimbali kama vile: kanuni ya idadi, ukweli, uhusiano na namna. Mawazo ya Grice ni muhimu katika utafiti huu kwa vile yanauwekea msingi wa kinadharia hasa katika kipengele cha

kanuni za utaratibu wa ushirikiano ambacho ndicho msingi wa mawazo ya Nadharia ya Uso ya Brown na Levison kuhusu upole na mikakati ya upole.

Mwanaisimu mwingine ambaye ameshughulikia suala la upole kinadharia ni Lakoff (1973). Lakoff ni mmoja wa wanaisimu wa kwanza kutafiti dhana ya upole na kuibua wazo kuwa upole ni dhana muhimu sana ya mahusiano ambayo inahitaji kutafitiwa. Katika kazi yake ya *what You can Do with Worlds: politiness pragmatic and perfomatives,* Lakoff analiangalia suala la upole katika msingi wa kanuni za upole. Kwa mujibu wa Lakoff, watu wanapozungumza huzingatia seti maalum ya kanuni zinazozuia kuvunjika kwa mawasiliano. Kanuni hizi ni pamoja na; kanuni ya uwazi na ile ya upole. Brown na Levinson (1987) walitumia mawazo ya Lakoff kuikuza nadharia yao ya upole hasa katika kipengele cha mikakati ya upole. Mawazo ya mtaalam huyu yana mchango katika utafiti huu katika kuelezea baadhi ya vipengele vya nadharia ya Upole ya Brown na Levinson.

Leech (1983) ni mwanaisimu mwingine ambaye anaangazia dhana ya upole kwa kuegemea mkabala wa kipragmatiki.Leech, alilenga kuuhakiki mtazamo wa Grice (1975) kuhusu dhana ya upole. Katika kazi yake ya *Principles of politeness* (1983:132), Leech anafasiri dhana ya upole kama aina ya tabia ambayo huwawezesha washiriki katika mazungumzo kuhusika katika mtagusano wa kijamii katika hali ya uwiano na kiupatano. Leech anafafanua kuwa, jambo muhimu zaidi katika mawasiliano ni kudumisha mazingira ambayo yatadumisha mawasiliano husika.Kulingana na yeye, mawasiliano hutawaliwa na kanuni fulani ambazo lazima zizingatiwe. Brown na Levinson (1987) watumia kanuni za mtaalamu huyu hasa kanuni ya mkakati kuibuka na mikakati minne ya upole ambayo huzingatiwa na washirika wakati wa mazungumzo.

Spencer (2000) aliibuka na mtazamo wa udhibiti wa uhusiano katika harakati za kuihakiki nadharia ya Brown na Levison (1987). Kwa mujibu wa Spencer, udhibiti wa uhusiano baina ya mzungumzaji na msikilizaji ndicho chanzo cha kudumisha upole katika mawasiliano.Spencer alidai kuwa, kitu muhimu zaidi katika mawasiliano ni kuzingatia haki za kijamii za msikilizaji pamoja na kuidumisha thamani ya uso wake kijamii.Spencer anazungumzia kuhusu thamani chanya ya uso wa msikilizaji kama mojawapo wa mahitaji muhimu kuzingatiwa katika

mawasiliano. Dai hili linaingiliana na mawazo ya Brown na Levinson (1987) kuhusu uso chanya ambao wanasema kuwa kila mara mzungumzaji hubuni mikakati ya upole kuutunza.

Watts (2003) anahakiki mawazo ya Brown na Levinson (1987) kwa kuuangalia upole katika ngazi mbili kuu ambazo ni upole wa daraja la kwanza na upole wa daraja la pili. Upole wa daraja la kwanza anauhusisha na uelewa wa kawaida wa wanajamii kuhusu upole na vigezo wanavyovitumia kupimia matumizi fulani ya lugha kama yenye upole au yasiyokuwa na upole.Watts anasema kuwa, upole katika daraja la pili ni uelewa wa kiisimu na wanaisimu kuhusu matumizi ya lugha ya upole. Katika upole wa kiwango cha pili, Watts anadai kuwa nadharia za kiisimu ni muhimu katika kuchanganua matumizi ya lugha ili kusema yana upole au la.Aidha, anahusisha upole katika kiwango hiki na lugha zungumzwa na lugha ishara.

Kuhusu dhana ya uso, Watts anaueleza uso kama ujitambulishaji wa mtu kithamani katika jamii. Anaendelea kusema kuwa, uso si kitu kimoja kwa vile hubadilikabadilika kiwakati na kwa kutegemea hali na miktadha ya mazungumzo ambayo washirika hujikuta.Kwa msingi huu, Watts anauona upole kama hali inayotegemea jamii, muktadha na hali za washirika katika mtaguasano wa mazungumzo. Mawazo ya Watts ni muhimu katika utafiti huu kwa vile yanagusia uso ambao pia utafiti wetu unaangazia. Pia, mawazo ya Watts kuhusu upole kutegemea hali za kijamii ni muhimu kwa mtafiti kwa kuwa hii ni mojawapo ya malengo ya mtafiti.

Japo wataalam hawa wanaungalia upole kwa kutumia mikabala tofauti, inajitokeza kuwa wote wanajishughulisha na jinsi wazungumzaji huzalisha mikakati mbalimbali ya kiisimu wanapozungumza kwa kutegemea seti ya kanuni maalum zilizobainishwa.Pia, inajitokeza kuwa, wataalamu hawa wote wanajifunga na mtazamo wa kiufafanuzi na kikaida katika kulikabili suala la upole.Aidha, mikabala yao ni tofauti lakini wanaelekea kukubaliana kuhusu kitu kimoja kuwa upole ni sehemu ya lazima katika mazungumzo. Vilevile, wanaisimu hawa wanakubaliana kuwa seti ya kanuni zinazotumiwa katika kuzingatia upole ni ya kilimwengu na haijifungi na utamaduni maalum.

Katika utafiti huu hata hivyo, mtafiti anaongozwa na mawazo ya Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) kwa vile inahusisha kipengele cha mikakati ya upole ambacho ndicho msingi wa uchambuzi wa tamthilia ya *Mbaya Wetu*.

### 1.9.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti

Kuna watafiti wengi ambao wametumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levison (1987) kuchunguza suala la upole na mikakati yake katika kuchambua matini mbalimbali. Hata hivyo, wengi wa watafiti hawa ambao ni wa nchi za ulaya, wameitumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson katika kuchunguza matumizi ya lugha ya wahusika katika sinema. Kutokana na ukweli kuwa sinema ni sanaa ya kidrama kama ulivyo utanzu wa tamthilia tunazipitia baadhi ya kazi hizi kama sehemu ya madurusu.

Katayoon, A. (2013) alitumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) kuchambua sifa za wahusika katika tamthilia ya Woody Allen, *Death Knocks*. Katika utafiti wake, Katayoon alitumia nadharia hii kubainisha jinsi sifa za wahusika wawili wanaopatikana katika tamthilia hii ambao ni *Death* na *Nat* zinavyojitokeza. Mtafiti huyu alichambua lugha ya wahusika hawa katika miktadha mbambali ya kijamii na kubainisha kuwa waliweza kujibainisha kwa namna mbalimbali kupitia lugha yao. Katika mazungumzo ya wahusika hawa Nat anajitokeza kama mwenye maringo kwa kujigamba mbele ya Death ilhali Death ni myenyekevu. Vilevile, mtafiti huyu alibainisha jinsi wahusika hawa wanavyotumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali kwa kuchunguza lugha yao kwa mfano Death anatumika kukuza maudhui ya mamlaka baada ya kumshinda Nat.

Katika utafiti huu pia, Katayoon anaonyesha kuwa lugha huwa na dhima ya kutambulisha wahusika ambapo katika tamthilia ya *Death Knock* mhusika Death anajitokeza kama mwenye uwezo dhidi ya Nat kupitia lugha yake. Utafiti wa Katayoon unahusiana na wetu kwa kuwa unahusisha kazi ya tamthilia na ulitumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) kuchambua lugha ya wahusika. Kinyume na Katayoon, mtafiti wa utafiti huu anachunguza mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika katika tamthilia ya Kiswahili kwa nia ya kutaka kuwabainisha na kuchunguza hali zinazowapelekea kuitumia mikakati hii.

Mtafiti mwingine ni Hidayati, A. (2014) ambaye alitumia nadharia ya Brown na Levinson (1987) katika kuchunguza mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika sinema ya *A Letter to Juliet*. Katika utafiti wake, Hidayati alilenga kubaini mkakati wa upole uliotumika zaidi na wahusika wakuu katika sinema hii pamoja na kubainisha miktadha ya matumizi ya mikakati ya upole na wahusika hawa. Hidayati alibainisha kuwa, wahusika wanatumia mikakati hasi na chanya ya upole japo mkakati chanya wa upole ulitumika zaidi. Hidayati pia alitambua kuwa sababu kuu ya wahusika hawa kutumia mkakati wa upole kwa mapana ni kutokana na haja ya wao kutaka kuwajali wasikilizaji wao wanapojieleza hivyo kujenga uhusiano.

Hidayati pia alibainisha kuwa, wahusika wakuu walitumia mkakati chanya wa upole zaidi wanapoingiliana na wahusika wasiofahamiana nao na wahusika wanaowazidi kwa umri. Japo Hidayati alitumia nadharia hii kuchunguza mikakati ya upole katika sinema, utafiti wake ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu unahusisha sinema ambayo ni sanaa ya drama. Sinema kama tamthilia huhusisha lugha ya mazungumzo hivyo utafiti wa Hidayati ni muhimu kwa mtafiti wa utafiti huu katika kuchambua namna mikakati ya upole inavyotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.* Aidha, utafiti huu ni muhimu kwa mtafiti katika kuzibainisha hali zinazoyaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*.

Fatkhurozi, A. (2007) alifanya utafiti kuhusu mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika Mia na nyanya yake katika sinema ya *Princess Diaries* kwa kuegemea mkabala wa kiisimujamii. Mtafiti huyu alitafiti matumizi ya lugha ya wahusika hawa katika sinema hii kwa kutumia mtazamo wa Upole wa Scollon na Scollon (1995). Fatkhurozi alitambua kuwa,Mia na nyanya yake walitumia mikakati miwili ya upole. Mkakati wa ushirikishi na mkakati wa uhuru kama wanavyoeleza Scollon na Scollon. Utafiti wa Fatkhurozi unatofautiana na utafiti huu kwa vile yeye anatumia mkabala wa upole wa Scollon na Scollon ilhali utafiti huu unatumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson. Zaidi ya hili, Fatkhurozi alichambua sinema ilhali kazi hii inajifunga katika kuchambua tamthilia. Hata hivyo, utafiti wake unatufaa katika kuelezea jinsi wahusika wa tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanavyojitambulisha kupitia matumizi yao ya lugha.

Mtafiti mwingine ni Mufidatul, U. (2010) ambaye alichunguza jinsi mkakati hasi wa upole unavyotumika na wahusika katika sinema ya *There is Something About Mary*. Mufidatul alitumia Nadharia ya Brown na Levison (1987) na kubaini kuwa wahusika wengi wanatumia mkakati hasi wa upole wanapoingiliana na wengine.

Sari, Y. (2010) naye alichunguza mkakati wa upole unaotumika na wahusika wakuu katika sinema ya *The Other Boleyn Girl* na kubainisha kuwa wahusika wote katika sinema hii wanatumia mikakati yote minne ya upole katika maingiliano yao. Katika utafiti huu, Sari alitambua kuwa, mhusika mkuu Anne anatumia mikakati mbalimbali ya upole kwa madhumuni maalum. Kwa mfano, Anne anatumia mkakati kwenye rekodi anapotaka kumpasha habari za dharura msikilizaji wake. Pia, anatumia mkakati nje ya rekodi anapoelezea kuhusu alivyoukuwa amesalitiwa katika siku za nyuma za maisha yake. Anne pia anatumia mkakati chanya wa upole anapotoa mapendekezo yake ya kuwania taji la malkia wa Uingereza kwa wasikilizaji. Mkakati hasi wa upole anautumia anapotaka kuokoa uso hasi wa msiklizaji.Tafiti za Mufidatul na Sari zinatofautiana na utafiti wetu kwa vile watafiti hawa walichambua utanzu wa sinema ilhali utafiti wetu unahusisha utanzu wa tamthilia. Hata hivyo, tafiti zao ni muhimu kwetu kwa sababu zinahusisha kipengele cha mikakati ya upole ambacho tunakishughulikia pia.

Ratna, I. (2012) alitumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) katika kuchambua mikakati ya upole inayotumiwa na mhusika mkuu Harry Potter katika riwaya ya J.K. Lowling ya *Harry Potter and the Sorcerer's Stone,* katika tasnifu yake ya uzamili. Katika utafiti huu, Ratna anaweka wazi sifa za mhusika huyu kwa kuchambua mikakati ya upole anayoitumia.Utafiti wa Ratna ni muhimu katika kazi hii kwa vile unahusisha uchambuzi wa sifa za wahusika kwa kuchunguza mikakati ya upole inayotumiwa na mhusika mkuu katika riwaya *Harry Potter and the Sorcerer's Stone*. Kinyume na Ratna aliyechambua utanzu wa riwaya, mtafiti anachambua mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika utanzu wa tamthilia.

Hobbs, J. (2003) katika utafiti wake *The Medium is the Message: Politeness Strategies in Men's and Women's voice mail messages* alitumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) kuchanganua lugha ya wanawake na wanaume katika jumbe za simu zilizohifadhiwa katika lugha zungumzwa. Hobbs alibainisha kuwa, lugha ya wanawake ilitawaliwa na matumizi ya

mkakati chanya wa upole ikilinganishwa na ile ya wanaume. Katika uchunguzi wake pia, Hobbs alibainisha kuwa, lugha ya wanawake ilitawaliwa na uombaji wa msamaha na upigaji vijembe walipokuwa wakizungumza na wenzao wa kiume. Hali hii ilikuwa kinyume katika lugha ya wanaume. Hobbs alibaini kuwa hali hii ilitokana na sababu za kijamii kama malezi na utamaduni.

Utafiti wa Hobbs unamsaidia mtafiti katika kutambua na kuelezea sababu za wahusika kutumia mikakati ya upole inayotofautiana katika mazingira mbalimbali.Utafiti wa Hobbs pia unaingiliana na ule wa Fitriayani,Y.(2007), ambaye alichambua mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika katika riwaya ya John Grisman *The Client.* Fitriayan alitambua kuwa japo mikakati yote minne ya upole inatumika, matumizi ya mikakati hii yanaongozwa na masuala mbalimbali ya uhusiano wa kijamii kama:umri, uhusiano, mamlaka na tabaka.

Owino, M. (2011), alichanganua matini teule ya nyimbo za Faustine Munishi kwa kutumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) katika tasnifu yake. Katika utafiti wake, Owino alitumia nadharia hii katika kutafiti mikakati ya upole inayojidhihirisha katika nyimbo mbili za mwimbaji huyu wa nyimbo za kidini. Martha alitambua kuwa, kuna mikakati mbalimbali ya kuokoa uso hasi wa wasikilizaji iliyotumika na mwimbaji huyu ili kudhihirisha upole kwa wasikilizaji wa nyimbo zake.

Utafiti wa Owino una mchango mkubwa katika kazi hii kwa vile unadhihirisha jinsi ambavyo Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) inavyoweza kutumiwa katika kufafanua maana za kauli za mzungumzaji. Japo Owino alijifunga na lugha zungumzwa na uchambuzi wa maana katika nyimbo husika, utafiti wake ni nguzo muhimu katika kuiwekea kazi hii msingi wa kinadharia. Kinyume na Owino anayechunguza utanzu wa fasihi simulizi yaani utanzu wa nyimbo, utafiti huu unaegemea matini andishi yaani tamthilia kwa kutumia nadharia ya Brown na Levinson (1987).

Mwari, R. (2014), alifanya utafiti kuhusu mikakati ya upole katika vipindi vya runinga kwa kujikita na mawaidha ya Bi.Msafwari katika runinga ya *Citizen*. Mwari alibainisha kuwa, suala la upole ni muhimu sana katika mazungumzo kwenye vipindi vya runinga. Mtafiti huyu pia

alitambua kuwa vipindi vya runinga hutakiwa kuyajali mahitaji ya nyuso za wahusika katika mazungumzo husika na vilevile katika kukabiliana na vitisho vya kutishia nyuso za washiriki, wasikilizaji na watazamaji wa vipindi hivi.

Utafiti wa Mwari ni muhimu katika utafiti huu kwa vile, kama ulivyo utafiti wa Owino utafiti wa Mwari unauwekea utafiti huu msingi wa kinadharia. Zaidi ya hayo, Mwari anajihusisha na lugha ya mazungumzo baina ya Bi. Msafwari na Lulu na Kanze sawa na ilivyo lugha ya tamthilia ambayo huhusisha mazungumzo ya wahusika mbalimbali. Kwa msingi huu, uanishaji wa mikakati ya upole uliotumika katika mazungumzo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa vile unasaidia katika kuchambua na kuanisha kauli za wahusika katika tamthilia hii.Mwari hata hivyo, anajihusisha na lugha zungumzwa ilhali utafiti huu unaegemea katika lugha andishi.

## 1.10 Mbinu za Utafiti

### 1.10.1 Uteuzi wa Sampuli

Mtafiti wa utafiti huu anatumia Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) katika kutafiti namna wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanatumia mikakati ya upole katika kufanikisha mazungumzo yao. Aidha, anachunguza jinsi matumizi ya mikakati ya upole na wahusika hawa inavyosaidia katika kuendeleza matukio ya kidrama tamthiliani.Mtafiti anatumia tamthilia hii kama sampuli ya utafiti kwa sababu kuwa, tamthilia huhusisha lugha ya mazungumzo ambapo wahusika husawiriwa wakizungumza kwa njia ya moja kwa moja. Kwa msingi huu, inakuwa ni rahisi kwa mtafiti kuchanganua jinsi mikakati ya upole inavyotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ikilinganishwa na matini zinazohusisha lugha ya kinathari. Pia, usawiri wa wahusika katika tamthilia hutegemea usemi wa moja kwa moja. Hivyo, mtafiti wa utafiti huu ambao unahusisha uchambuzi wa mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu ananufaika na utanzu huu katika kubainisha jinsi mikakati ya upole inavyosaidia katika kuzikuza sifa za wahusika wakuu.

Kazi hii inatumia tamthilia ya *Mbaya Wetu* kama sampuli lengwa ya utafiti kwa sababu kadhaa. Kwanza, kulingana na ufahamu wa mtafiti tamthilia hii haijafanyiwa uhakiki mwingine hadi sasa. Kwa msingi huu, utafiti huu utakuwa wa kwanza na mchango mpya katika fasihi ya Kiswahili. Pili *Mbaya Wetu* ni tamthilia ya kitashtiti ambayo inadhihirisha ufundi na ustadi

mkubwa katika utunzi wake hasa katika usawiri wake wa wahusika. Hii ina maana kuwa, ufundi wa mwandishi katika matumizi ya lugha katika tamthilia hii ni mojawapo ya sababu zinazomfanya mtafiti kuitumia katika utafiti wake. Kutokana na sababu hizi, tamthilia hii inamfaa mtafiti kwa vile anakusudia kuchambua mikakati ya upole katika mazungumzo ya wahusika wakuu.

Mtafiti amewateua wahusika wakuu wa tamthilia ya *Mbaya Wetu* kwa vile wahusika hawa wanajibainisha kuanzia mwanzo hadi mwisho hivyo wamepewa nafasi kubwa ikilinganishwa na wahusika wengineo. Kadhalika, wahusika wakuu katika tamthilia hii wametumika na mwandishi kuibusha na kuyakuza maudhui mbalimbali. Kutokana na sababu hii, wahusika hawa wanatagusana na wahusika wengine tamthiliani kwa mapana katika kuikamilisha tamthilia hii kifani na kidhamira. Wahusika hawa pia wanaathiriwa na hali mbalimbali za jamii kwa mapana ikilinganishwa na wahusika wengine kutokana na upana wa mawanda yao ya mtagusano.Kutokana na hali hii, wahusika hawa ni muhimu sana kwa mtafiti kwa sababu mojawapo ya malengo yake ni kubainisha hali za kijamii zinazoyaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu tamthiliani.

### 1.10.2 Mbinu za Kukusanya Data

Mtafiti alijifunga katika kukusanya data ya utafiti wake maktabani ambako alisoma vitabu, makala na majarida yanayohusiana na mada ya utafiti. Katika kufanya hili, mtafiti alipitia vitabu na majarida yanayohusiana na nadharia za upole pamoja na tahakiki zilizochapishwa kuhusiana na nadharia hizi. Katika utafiti wake maktabani, mtafiti pia alitembelea mtandao kutafiti makala na machapisho ambayo yana mchango katika utafiti wake. Mtafiti aliisoma na kuichambua tamthilia ya *Mbaya Wetu* ili kuipata data ya utafiti wake. Data hii ilikusanywa kwa kuchunguza kauli za wahusika wakuu ili kubainisha mikakati mbalimbali ya upole wanayoitumia.

### 1.10.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Kwa vile huu ni utafiti unahusisha uchanganuzi sifa ambao huhusisha mbinu ya ufafanuzi katika kuchanganua data yake. Mtafiti aliisoma tamthilia ya *Mbaya Wetu* na kunakili kauli za wahusika wakuu zinazodhihirisha matumizi ya mikakati ya upole.Baada ya hatua hii, kauli hizi ziliainishwa kwa msingi wa kategoria za mikakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole,

mkakati wa upole  nje ya rekodi na mkakati hasi wa upole ndani ya rekodi. Baadaye, kauli hizi zilifafanuliwa kwa mujibu wa nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Katika kuzifafanua kauli hizi, mtafiti alibainisha ambavyo wahusika wakuu katika tamthilia hii wanavyoitumia mikakati hii katika kufanikisha mazungumzo yao pamoja na kutathmini mchango wa mikakati hii katika kufanikisha drama.

Katika hatua nyingine, mtafiti aliichanganua mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* ili kubainisha jinsi inavyochangia katika kuzikuza sifa zao. Katika uchanganuzi huu, vipashio muhimu vya kiisimu ambavyo vina mchango katika kuzidhihirisha sifa za wahusika hawa vilichunguzwa. Baadhi ya vipashio hivi vya kiisimu ni pamoja na vitenzi, vivumishi, vihisishi miongoni mwa kategorio zingine za kisarufi.Isitoshe, katika kuzifafanua sifa za wahusika hawa mtafiti anaonyesha jinsi suala nzima la kidrama linavyojibainisha katika matumizi ya mikakati ya upole inayohusika. Mwishowe, mtafiti alijadili hali mbalimbali za jamii zinazoyaathiri matumizi mikakati mbalimbali ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*.

# SURA YA PILI

# MATUMIZI YA MIKAKATI YA UPOLE NA WAHUSIKA WAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *MBAYA WETU*

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti anashughulikia jinsi wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanaitumia mikakati ya upole katika kufanikisha mazungumzo yao na wahusika wengine. Aidha, mtafiti anachunguza jinsi suala nzima la kidrama linabainika kupitia matumizi mbalimbali ya mikakati ya upole kama inavyotumika na wahusika hawa.Katika kuchunguza hili, kazi hii inashughulikia jinsi wahusika wakuu wanaitumia mikakati yote minne ya upole kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Mikakati ya upole ambayo inashughulikiwa katika sehemu hii ni pamoja na, mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole, mkakati nje ya rekodi na mkakati ndani ya rekodi. Aidha, kila mkakati unaonyeshwa na kaida zinazotumiwa kutekeleza vitendo vya kutishia uso kama zinavyoelezwa katika nadharia ya uso.

## 2.1 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Upole

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987:101), Mkakati chanya wa upole hutumika na mzungumzaji kwa msikilizaji kwa nia ya kumwonyesha kuwa anamjali kwa kuushughulikia uso wake chanya. Kwa msingi huu, mzungumzaji huufurahisha uso chanya wa msikilizaji kwa kumjengea mazingira mazuri ya mazungumzo hasa kwa kuonyesha mahusiano mazuri baina yake na msikilizaji.

Mkakati chanya wa upole huweza kudhihirishwa katika mazungumzo ya washirika kupitia matumizi ya mbinu mbalimbali. Baadhi ya mbinu hizi ni pamoja na, kuyajali maslahi ya msikilizaji, kutilia manani mahitaji ya msikilizaji, kuchangia mazungumzo kwa namna ambayo itamvutia msikilizaji, kujitambulisha pamoja na msikilizaji, kuepuka kumpinga msikilizaji, kukubalina na maoni ya msikilizaji, kutumia ucheshi, kumtolea msikilizaji ahadi, kumwonyesha msikilizaji huruma na kumwelewa msikilizaji miongoni mwa mbinu nyingine.

Brown na Levison (1987) wanaeleza kuwa, mkakati huu hutumika katika mazungumzo miongoni mwa marafiki ama watu wenye uhusiano wa karibu kama vile familia au wafanyikazi.

Katika sehemu hii, mtafiti anajadili jinsi mkakati chanya wa upole unabainika katika matumizi ya lugha ya wahusika wakuu ambao ni; Matari, Lila, Mzee Temba na Mama.

### 2.1.1 Kumtambua na Kumshughulikia Msikilizaji

Brown na Levinson (1987:108) wanaeleza kuwa katika mkakati huu mzungumzaji hutekekeleza kitendo cha kutishia uso chanya wa msikilizaji kwa kuzitambua sifa zake na kuonyesha kuwa anamjali. Kwa msingi huu, mzungumzaji huufurahisha uso chanya wa msikilizaji kwa kutumia maneno ya sifa na kauli nyingine ambazo humdokezea msikilizaji kuwa mzungumzaji anamtambua kama mshirika wa mazungumzo husika. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu,* mbinu hii inadhihirika katika mazungumzo ya wahusika wakuu kwa mapana, kwa mfano:

Matari anatambua uso chanya wa walevi katika baa ya Fiona anapozungumza na Mtu I kwa kusema:

38. MtuI: Twakukaribisha Mtukufu Matari…kwa vilili na vigoma.
    Matari: Ahsanteni nduguzanguni.[Kwa Fiona] Wape hawa wote wanywe buzaa ifurike matumboni mwao kuliko gharika ya Nuhu. Mimi nitalipa. uk.72

Katika dayolojia iliyopo hapo juu, Matari anashughulikia uso chanya wa wasikilizaji wake kwa kutumia mkakati chanya wa upole ambao unatambulishwa na kauli *Ahsanteni nduguzanguni.*Kwa kutumia kauli hii, Matari anajenga uhusiano wa karibu na wenzake kwa kuutambua uhusiano uliopo baina yake nao. Uhusiano huu unajengwa kupitia matumizi ya neno *nduguzangun*i linalokusudiwa kuonyesha utambulisho wake kwao. Kadhalika, Matari anaonyesha hali ya kuwajali wasikilizaji wake kwa kusema*: Wape hawa wote wanywe buzaa ifurike matumboni mwao kuliko gharika ya Nuhu.*

Katika kauli hii, Matari anatumia chuku ya buzaa kufurika matumboni mwa walevi ili kusisitiza makusudio yake ya kuyajali maslahi ya walevi hawa. Kwa kufanya hivi pia, Matari anazuia kuibuka kwa mgogoro baina yake na walevi kufuatia kisa anachowasimulia kuhusu alivyofanikiwa kuziiba na kuziuza nguo za maaskari ili apate pesa za kuwanunulia buzaa. Maneno ya Matari aidha yanakusudia kuwazimba macho walevi wasione sifa yake ya wizi bali wamuone kama karimu ambaye amejitolea kuyashughulikia mahitaji yao.

Katika muktadha mwingine Lila anautambua uso chanya wa mamake anapomshawishi ale chakula. Mazungumzo ya Lila na Mama yanajitokeza ifuatavyo:

39. Mama: Hahaha! Mimi leo sili na silali.
Lila: Kula mama. Kula kidogo. Nimekwambia
mama hakuna anayemuua mwanao.uk 60

Katika mfano 39, Mama na Lila wanajikuta katika mvutano mkubwa. Chanzo cha mvutano huu ni kitendo cha Mama cha kukataa kula chakula kwa madai kuwa mwanawe Matari amekamatwa kwa tuhuma ya wizi. Kwa upande mwingine, Lila anawajibika kumshawishi Mama kutuliza mawazo yake kwa kumsihi akile chakula.Kutokana na hali hii, Lila anatumia mkakati chanya wa upole katika kuujenga mwingiliano mzuri baina yake na Mama kwa nia ya kumtuliza. Lila anautambua uso chanya wa Mama kwa kuonyesha kumjali kupitia matumizi ya neno *mama* linaloonyesha uhusiano wake na Mama na wakati uo huo kutumia maneno ya kushawishi kama vile *kula kidogo* na *kula mama*. Kwa kutumia lugha yenye sifa hizi, Lila anadhihirisha jinsi anavyomjali kwa kumhakikishia kuwa mwanawe Matari yuko salama. Pia, Lila anafahamu kuwa hali ya afya ya Mama si nzuri na kukamatwa kwa Matari kumemzidishia huzuni. Kwa msingi huu, Lila anadhihirisha hali ya kumjali mamake kwa kumleta karibu na kumhakikishia mazuri, kwa kufanya hivi anawekea mazungumzo yao msingi imara wa kuyadumisha.

Katika mazungumzo baina ya Matari na Mama, Mama anautambua uso chanya wa Matari kwa kumweleza jinsi yeye na babake wanampenda.Mama anamwambia Matari:

40. Mama: Tangu lini sisi wazee wako tukakosa karo ya kukulipia mtoto wetu? uk.20.

Katika mfano 40, Mama anatumia mkakati chanya wa upole kwa Matari kwa nia ya kumwonyesha kuwa anajaliwa na kuwa yeye ni sehemu ya familia ya Mzee Temba.Upole chanya katika lugha ya Mama unabainika kupitia matumizi ya maneno ya utambulisho; *sisi wazee wako* na *mtoto wetu.* Kupitia maneno haya, Mama anamwonyesha Matari kuwa yeye ni sehemu ya familia ya Mzee Temba na wazazi wake wanamjali zaidi.Kauli ya Mama pia inadhamiria kuupunguza mgogoro unaozuka baina yake na Matari ambaye analalamika kuwa ni yeye pekee katika familia ya Mzee Temba ambaye hajasoma.

Kwingineko katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, Temba anadhihirisha matumizi ya mkakati chanya wa upole kwa kujitambulisha na wasikilizaji wake anapokuwa akizungumza na Lila.

41. Temba*:* Lila u hali gani?
Lila: Njema baba.
Temba: Usisahau kurauka mapema
kesho kwenda sokoni kunidaia
deni kwa yule mwalimu mpangaji
asiyelipa kodi…
Lila: …Lakini baba? uk.23.

Dayolojia iliyopo hapo juu inadhihirisha wahusika Lila na Temba wakitumia mkakati chanya wa upole ili kuokoa nyuso chanya zinazohusika. Temba anamtambua Lila kwa jina kwa kumwita *Lila* na kisha kumwuliza Lila; *Lila u hali gani?* Kwa upande mwingine, Lila anadhihirisha upole chanya kwa kumtambua Temba kama babake kwa kusema; *Njema baba*. Matumizi ya lugha ya wahusika hawa yanadhamiria kuujenga uhusiano baina yao ili kufanikisha mazungumzo yao.

Aidha, Temba anatumia mkakati chanya wa upole kama ambavyo inadhihirishwa na kauli yake ili kumleta Lila karibu amtume kwa mwalimu jambo ambalo anajua kuwa Lila hatalikubali moja kwa moja. Kwa msingi huu, Temba anapunguza mvutano utakaoletwa na kauli yake kwa kuujenga uhusiano na mwanawe kwanza.

Aidha, Mama anashughulikia uso chanya wa Matari kwa kumtambua kama mwanawe na kumhakikishia kuwa yeye ni sehemu ya familia ya Mzee Temba. Mama Anapomwambia Matari hivi:

42. Mama: Matari mwanangu. Hapa ni kwenu. Kula ushibe, ulale usone bila atiati.
Nimi leo nitakula chakula kinitue tumboni atiati.
Njoo. Njoo mwanangu nikupige pambaja kitoto changu. Njoo. uk66

Katika kauli kwenye mfano 42, Mama anatumia maneno kama vile; *Matari mwanangu*, *Hapa ni kwenu* na *njoo mwangu nikupige pambaja.* Matumizi ya maneno haya yanadhamiria kuufurahisha uso chanya wa Matari kwa kumhakikishia kuwa mamake anamthamini, anatambulika kama sehemu ya familia ya Mzee Temba na ana uhuru wa kula, kulala na kufanya atakalo. Matamshi haya pia yanadhamiria kumtuliza Matari kimawazo baada ya kuachiliwa kutoka seli.

### 2.1.2 Kutumia Vitambulisho vya Makundi

Brown na Levinson (1987:102), wanaeleza kuwa, katika kutumia mkakati huu ili kuokoa uso chanya wa msikilizaji, mzungumzaji huonyesha uhusiano wake na msikilizaji kwa kumtambua kama sehemu ya kundi lake. Utambuzi huu huhusisha matumizi ya maneno ya kujenga na kudumisha mahusiano kama vile: ndugu, dadangu, mke wangu, mamangu miongoni mwa majina mengine ya utambulisho. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu,* mbinu hii inadhihirika katika matumizi ya lugha ya wahusika wakuu kwa namna mbalimbali. Kwa mfano:

Matari anatumia kaida hii anapojaribu kupunguza hasira ya Lila baada ya kumwibia pesa kwa kumwita dada na kujihusisha na familia ya Mzee Temba:

> 43. Matari: Yaani mimi mwehu kiasi gani hata nikuibie
> dadangu ilhali mama mgonjwa hali yake taabani? uk 15.
> …siwezi kujitia wazimu kwa kumwibia dadangu mwenyewe. uk16.

Mfano 43 ni kauli ya Matari kwa dadake Lila ambaye anamtuhumu kwa kumwibia pesa zake. Hali ya mgogoro inayosababishwa na kitendo cha wizi cha Matari inamfanya Matari kujitetea na kumtuliza Lila kwa kutumia mkakati chanya wa upole. Matari anajitambulisha na Lila ili kuonyesha uhusiano wao wa damu kwa kutumia neno *dadangu* na kisha kusisitiza hali hii kwa kutumia kauli; *dadangu mwenyewe.* Kwa kumhusisha dadake na yeye, Matari anadhamiria kumwonyesha Lila kuwa hawezi kumwibia pesa kwa sababu wanatoka katika familia moja.Aidha, mkakati huu wa upole unamsaidia Matari kuingiliana na Lila kwa namna nzuri licha ya kuwa wahusika hawa wawili hawana mkabala mzuri.

Katika muktadha mwingine, Temba anatambua uso chanya wa Tonge kwa kutumia kaida ya utambulisho wa kimakundi anapomwomba anawe mikono wale, Temba anasema:

> 44. Temba*:* Nawa tule mwanangu. uk61.

Temba anatumia mkakati katika mfano 44, ili kuusuluhisha mgogoro baina yake na Tonge ambaye amekataa kuitii amri yake ya kufutilia mbali kesi ambayo amemshtaki Matari kwa wizi wa ng'ombe wake. Kwa kutumia neno *mwanangu*, Tonge anahisi kuwa yeye ni sehemu ya familia ya Mzee Temba na anafaa kushiriki katika mazungumzo yanayohusisha familia hii. Kadhalika, Temba anatumia kiwakilishi nafsi -tu- chenye kuleta ujumulishaji kama njia ya kuonyesha kuwa Tonge ni sehemu ya familia hii.

Matumizi ya mbinu ya utambulisho wa makundi kama mkakati wa kuokoa uso chanya wa msikilizaji aidha yanajidhihirisha katika mazungumzo ya Mama anapomkaribisha mumewe nyumbani kutoka sokoni kwa kusema:

45. Mama: Pole kwa safari mume wangu. uk.23.

Katika mfano 45, Mama anaushughulikia uso chanya wa Temba kwa kumwita *mume wangu* ishara kuwa anajihusisha na yeye. Kwa kutumia mkakati huu pia, Mama analenga kumfurahisha mumewe ambaye tayari amekasirishwa na vitendo vya Matari kumwibia vipuli vya magari.Kwa kumtuliza kupitia kauli hii, Temba anajihisi ana mshirika mzuri katika mazungumzo hivyo kumweleza mkewe yaliyokuwa yamejiri.

Kadhalika, Mama anatumia mkakati chanya wa upole katika kusuluhisha mgogoro ambao unajitokeza anapojaribu kumshawishi Tonge kumsamehe kakake Matari.Mama anajaribu kumshawishi Tonge kwa kumtambulisha Tonge na Matari, Mama anamwambia Tonge hivi:

46. Mama: Tonge mwanangu msamehe nduguyo. uk.61

Katika mfano 46, Mama anadhihirisha matumizi ya mkakati hasi wa upole kwa kutumia majina mawili ya utambulisho *mwanangu* na *nduguyo*.Kwa kumwita *mwanangu,* Mama anamleta Tonge karibu na yeye kwa kumpa utambulisho wa familia. Kupitia matumizi ya neno *nduguyo*, Mama anajaribu kuathiri hisia za Tonge ili auone uhusiano wa damu ulipo baina yake na Matari hivyo kuyasahau makosa yake.

### 2.1.3 Kutafuta Makubaliano

Mbinu hii kama sehemu ya kuokoa uso chanya huhusisha kuuhifadhi uso wa msikilizaji kwa kukubaliana na anachokisema na kuepuka kumpinga.Aidha, mbinu hii huhusisha mzungumzaji kuchagua mada ambayo msikilizaji anaielewa. Brown na Levinson (1987:117) wanasema kuwa, kuzungumza kuhusu mada kubalifu kunamwezesha msemaji kutilia mkazo makubaliano yake na msikilizaji na hivyo kutosheleza tamanio la msikilizaji la kuwa katika ukweli au kukubalika katika maoni yake.

Kwa msingi huu, katika kutekeleza mkakati chanya wa upole kupitia kutafuta makubaliano, mzungumzaji hulenga kujua mengi kumhusu msikilizaji.Ufahamu huu humwezesha mzungumzaji kuendelea kuimarisha uhusiano wake na msikilizaji na kujenga uhusiano katika

mazungumzo yao. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wahusika wakuu wanadhihirisha mbinu hii katika maingiliano yao kwa njia mbalimbali.

Kwanza, Matari anapokabiliwa na Lila kwa madai ya kuiba pesa zake, Matari anadhihirisha matumizi ya mkakati chanya wa upole kwa  kukubaliana na kile ambacho Lila anamtaka kukubaliana nacho. Dayolojia ya wahusika hawa inajitokeza ifuatavyo:

47. Lila: Usimuue mama bure kwa vituko vyako
    Matari: Nimesikia dada. uk22

Katika mfano 47, Matari na Lila wanajikuta katika mgogoro mkubwa ambapo Lila anamlaumu Matari kwa kumwibia pesa zake.Matari anaamua kuumaliza mvutano huu kwa kukubaliana na ombi lake la kutomzidishia Mama maradhi kupitia tabia yake ya wizi lakini kwa namna ya kutumia mkakati chanya wa upole.Matari anakubaliana na maneno ya Lila kwa kusema; *Nimesikia dada* hivyo kumhakikishia Lila kukubalika kwa maoni yake.

Aidha, mbinu hii ya mzungumzaji kutafuta makubaliano na msikilizaji ili kuuthamini uso wake chanya inabainika katika matumizi ya lugha ya Lila anapoongea na mamake kuhusu ndoa yake. Katika mazungumzo yanayohusisha wahusika hawa wawili, Lila hafurahishwi na kitendo cha Mama cha kumkumbusha kuhusu ndoa hali ambayo inazua mvutano baina yake na mamake.Hata hivyo, Lila anajaribu kuumaliza mgogoro huu kwa kukubaliana na maoni ya mamake kuhusu ndoa.Dayolojia baina ya wahusika hawa wawili inajitokeza kama ifuatavyo:

48. Mama: Ni mwana wa nani huyo aliyekuja kukuposa?
    Lila: Mama hayo tuyazungumze baadaye.
    Mama: Lakini ujue amri ya umri. Wewe si mtoto tena.
    Utakuja kuchelewa kuolewa, ubaki unahangaika kama usipotahadhari.
    Lila: Sawa mama.
    Mama: Kuishi bila kuolewa na bila kuzaa ni laana tupu.
    Lila: Sawa mama, nimesikia.uk.31-32

Katika dayolojia 48, Lila anakubaliana na mada ya Mama kwa kutumia maneno*; Mama hayo tuyazungumze baadaye.*Katika kauli hii, Lila anamtambua mamake kwa kumwita *mama* na wakati uo huo kumhakikishia Mama kuwa mada yake wataishugulikia baadaye. Japo Lila anampinga Mama, anafanya hili kwa namna inayodhihirisha makubaliano.Katika mfano 48 pia, Lila anakubaliana na Mama kwa kutumia maneno*; Sawa mama na Sawa mama, nimesikia.*Lila anauokoa uso chanya wa Mama kwa kukubaliana naye na kuunga mada yake mkono.

Katika mandhari ya seli, Matari anaushughulikia uso chanya wa Askari I kwa kukubaliana na madai yake kuhusu biashara anayoifanya Fiona pale kijijini ili kuendeleza ushirikiano katika mazungumzo yake na askari huyu. Dayolojia hii inajitokeza hivi:

49. Matari: [kwa askari] Tafadhali mwambie dadangu
Lila aniletee soda na mkate. Ninakufa kwa njaa.
Akikataa mwambie Fiona, yule mwanamke shangingi
wangu aje aniauni.
Askari I: Fiona yupi? Humu kijijini mna Fiona wengi.
Matari: Yule Fiona muuza buzaa.
Askari I: Na chang'aa je?
Matari: Mara nyingine anaiuza chang'aa vilevile…uk.53-54

Kwenye dayolojia 49, Matari anaishia kukubaliana na wazo la Askari I kuwa Fiona anauza chang'aa kwa kusema; *Mara nyingine anaiuza chang'aa vilevile* kama njia ya kuumaliza mgogoro ambao Askari I anausababisha kwa kutaka aelezewe zaidi kumhusu Fiona. Matari anatumia mkakati huu kama njia ya kuafikia kusudio lake la kumtuma Askari I kwa Fiona kwa njia ya kuujenga uhusiano mwema kwanza kwa kukubaliana na chochote askari huyu anakisema.

### 2.1.4 Kuteua na Kuchangia Mada Inayomvutia Msikilizaji

Katika matumizi ya kaida hii kama njia ya kuuhifadhi uso chanya wa msikilizaji, mzungumzaji hujaribu kila awezalo kusema kile ambacho kitamfurahisha msikilizaji wake. Aidha, mzungumzaji hujaribu kubainisha mchango wake katika mada ya msikilizaji. Kwa msingi huu, msikilizaji huepuka kumuudhi msikilizaji wake kwa kumlazimisha kuchangia mada ambayo haimfurahishi ama kutochangia mada yake. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wahusika wakuu wanadhihirisha matumizi ya mkakati chanya wa upole kupitia uibuaji wa mada inayoeleweka na wahusika wengine ama kuchangia katika mada zinazoibuliwa na wasikilizaji wao.

Lila anatumia mbinu uteuzi wa mada ya kuvutia anapozungumza na babake kuhusu sababu yake ya kutokwenda kumdaia kodi kwa mwalimu asiyelipa kodi. Katika mazungumzo baina yake na babake, Lila anajikuta katika mgogoro ambapo Temba anamlaumu kwa kutotimiza amri yake. Lila anajaribu kuumaliza mgogoro huu kwa kuibua mada nyingine. Pia, Lila anamjengea babake taharuki kwa kujitokeza na mada ambayo inayoteka mawazo ya Temba kuhusu makutano yake na Vero.Dayolojia hii inajitokeza hivi:

50. Temba: …kwa nini hukufika?
    Lila: Baba! Samahani sana lakini nimepata mengine njiani.
    Temba: Mengine gani?
    Lila: Tonge.
    Temba: Nini Tonge?
    Lila: Ng'ombe wa ndugu yangu Tonge.
    Temba: Lila. uk 25-26

Dayolojia hii 50 inadhihirisha matumizi ya mbinu ya taharuki ambayo inanuia kumvutia Temba kwenye mada kuhusu wizi wa ng'ombe wa Tonge. Taharuki hii inajengwa kupitia matumizi ya maneno kama vile; *nimepata mengine njiani* na *Ng'ombe wa ndugu yangu Tonge.* Kupitia mbinu hii, Lila anafanikiwa kumfanya Temba alisahau kosa lake hivyo kuyajenga mazingira mazuri ya kuingiliana na yeye.

Aidha, katika mazungumzo haya baina ya Lila na, Temba, Temba anadhihirisha upole chanya kwa Lila kwa kuchangia katika mada ya Lila. Katika dayolojia hii, Lila anamwelezea babake sababu yake ya kutoenda kumdaia deni la kodi kwa mwalimu. Lila anaelezea kisa cha wizi wa ng'ombe wa shemeji yake Vero. Katika kumwonyesha kuwa anafuatilia mazungumzo haya Temba anatumia maneno yanayomthibitishia Lila kuwa anaifuata mada yake.

51. Temba: Kwani kulikoni? Eeh?
    Kisha? uk.26 Halafu? Lahaula! uk27

Katika mfano 51, Temba anatumia maswali kama; *Kwani kulikoni? Eeh? Halafu?* pamoja na kihisishi *lahaula!* kama njia ya kuonyesha kuwa anafuatilia mazungumzo ya Lila.Matumizi ya maneno na maswali haya yanampatia Lila motisha wa kuendelea kusimulia kisa chake kwa vile babake anadhihirisha ushirikiano katika mazungumzo husika.

Matari ni mhusika mwingine ambaye anadhihirisha mkakati chanya wa upole kwa kutumia mbinu hii ya kuchangia mada, Matari anasema:

52. Mtu II: Sote twakuenzi kama mboni ya jicho.
    Ukibadili usibadili mwendo na mavazi,
    bado twakupenda.
    Matari: Marhaba. Basi acha niwafafanulie kitaaluma.
    Mwendo ninaigiza mtu niliyemwona jana kwenye TV ya kakangu… uk 12

Katika mfano 52, Matari anawaelezea walevi katika baa ya Fiona kuhusu kisa cha mhusika wa sinema ya Kinaijeria aliyokuwa ameitazama akiwa kwa kakake Tonge. Matari anayateka

mawazo ya wasikilizaji wake kwa kusema; *Basi acha niwafafanulie kitaaluma.*Kwa kutumia kauli hii, Matari anavuta nadhari ya walevi kusikiliza kisa chake. Kisa hiki pia kinakuwa kama njia ya kuwafanya walevi kumwona na kumkubali Matari kama mmoja wao.

Katika mandhari haya ya baa ya Fiona pia, Matari anasimulia kisa kuhusu jinsi alivyofanikiwa kumwibia dadake elfu sitini alipoacha pochi lake pale kitandani. Matari anasema:

53. Matari: Basi dada kafika jana. Kampandisha mama
kwenye wheelchair kwenda kumwosha bafuni.
Akaacha pochi kitandani kwenye chumba cha mama. uk.14.

Katika mfano 53, Matari anaibua mada inayokusudia kufurahisha nyuso chanya za walevi kwa kuwaelezea jinsi alivyoishia kupata shilingi elfu sitini za kuwanunulia buzaa. Japo kisa chake kinadhamiria kuuficha udhaifu wake, Matari anafanikiwa kuunjenga mlahaka mzuri na walevi kwa kujitambulisha kama mmoja wao.

**2.1.5 Kutumia Ucheshi**

Mbinu hii huhusisha utoaji wa kauli zinazodhihirisha ucheshi na utani kwa wasikilizaji. Ucheshi huu hudhamiria kuimarisha uhusiano na kumfafanulia msikilizaji kuwa mzungumzaji anatambuliwa na mzungumzaji. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, mkakati chanya wa upole kupitia matumizi ya ucheshi unajitokeza ifuatavyo:

Matari anamtahadharisha Fiona dhidi ya kumwita mzee kwa namna ya ucheshi ambayo inaweka bayana uhusiano wao. Matari anasema:

54. Matari: Na usiniite mzee…sawa? Tuelewane…
Mzee gani, sijaoa, sijazaa, sina mvi,
sina bakora na tena si kibogoyo. uk.13.

Katika mfano 54, Matari anadhihirisha utani kupitia maelezo yake kuhusu sababu yake ya kutoitwa mzee kwa namna ya msisitizo; *Mzee gani, sijaoa, sijazaa, sina mvi, sina bakora na tena si kibogoyo.* Matumizi ya maneno yenye kuonyesha utani ni njia ya kuujenga uhusiano mwema na walevi kwa kushiriki katika mada na mijadala yao hivyo kujitambulisha kama mmoja wao.

Katika mfano mwingine tamthiliani, Matari anadhihirisha upole chanya kupitia matumizi ya ucheshi anapokuwa akielezea Mama maneno ya maandiko matakatifu: Dayolojia baina ya Matari na Mama inajitokeza ifuatavyo:

55. Mama: Andiko linasema nini?
    Matari: Linasema aliyekuwa akiiba, asiibe tena.
    Mama: Umeelewa.
    [Kimya]
    Mama: Nakuuliza kama umeelewa hilo…? Au umelewa?
    Matari: [Anaiacha hulka ya kilokole na kuwa mkaidi tena] Si hoja kama nimeelewa au nimelewa; yote mamoja. Najua unachotaka mama. Unataka niseme nimeokoka na kumkubali Yesu na kadhalika.Wataka nikwambie nikwambie leo nimekutana na Yesu njiani nikienda kwa Fiona kugeuza maji au chang'aa? Unafikiri kama Yesu asingalikuwa rafiki Yangu ningekuwa hai?uk.21

Katika mfano 55, Matari anatumia mkakati chanya wa upole unaotambulishwa na matumizi ya ucheshi. Matari anamwambia Mama kuwa anataka aseme kuwa alikutana na Yesu njiani akienda kwa Fiona kugeuza maji kuwa chang'aa*; Wataka nikwambie nikwambie leo nimekutana na Yesu njiani nikienda kwa Fiona kugeuza maji au chang'aa?* Kauli ya Matari inakusudiwa kuibua ucheshi kwa mamake kwa vile Mama anaelewa fika kuwa Matari hawezi kuwa amekutana na Yesu. Aidha, kuna matumizi ya kinaya cha kumweleza Yesu akibadilisha maji kuwa chang'aa. Katika kutumia mkakati huu, Matari anadhamiria kuumaliza mgogoro unaojitokeza baina yake na Mama ambao chanzo chake ni tabia ya Matari yakumwibia Lila.

Katika mfano 55 pia, Matari anatumia ucheshi kukwepa kujibu swali la mamake. Mama anamtaka Matari kusema iwapo ameuelewa ujumbe kutoka kwa maandiko matakatifu lakini Matari anatumia ucheshi kukwepa kufanya hivi na kuibadilisha mada. Vilevile, Matari anamaliza mgogoro baina yake na Mama kwa kusimulia kisa cha jinsi alivyonusuriwa na kachero mmoja aliyetumwa na 'Yesu' alipokuwa karibu kuuwawa na umati kwa kumwibia mama mzee shilingi kumi. Matari anazua ucheshi kwa kuuliza mamake swali; U*nafikiri kama Yesu asingalikuwa rafiki yangu ningekuwa hai?*

### 2.1.6 Kujumuisha Msemaji na Msikilizaji Katika Kitendo

Katika kutumia mkakati huu mzungumzaji hudhamiria kuonyesha ushirikiano baina yake na msikilizaji.Kwa msingi huu, mbinu hii huhusisha matumizi ya viwakilishi nafsi huru *sisi*, *mimi*

*na wewe*, na kiwakilishi nafsi tegemezi *'tu'* ili kumshirikisha mzungumzaji. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu,* mbinu hii inajidhihirisha kupitia mhusika Lila anapomwelezea Vero jinsiMtu I na Mtu II walivyokuwa wakiisengenya familia ya Mzee Temba. Lila anamwambia Vero hivi:

56. Lila: Mimi nilikwambia walisema kila mtu,
hata mimi,mambo ya kweli na urongo. uk.44

Katika, mfano 56, Lila anajihusisha na kitendo cha kusengenywa kwa kutumia maneno; *walisema kila mtu, hata mimi.*Kwa kujiingiza katika kitendo cha kusemwa kama Vero, Lila anafanikiwa kuutunza uso chanya wa Vero kwa kumfanya ahisi vizuri na kumwona Lila kama mshirika wake.Kwa upande mwingine, Lila anafanikiwa kupunguza mgogoro baina yake na Vero ambao unatokana na Lila kumlaumu Vero kwa kushirikiana na watu wa nje kuisengenya familia yao.

Katika mazungumzo ambapoTemba anajaribu kumshawishi Tonge kumsamehe Matari na kuondoa mashtaka dhidi yake, Temba anatumia mbinu hii ya kujumlisha kwa kumwambia Tonge:

57. Temba: Nawa tule mwanangu. uk.61

Katika kauli 57, Temba anajiweka kwenye kitendo cha kula pamoja na Tonge kwa kutumia kiambishi nafsi tegemezi -tu-. Aidha, Temba anasisitiza uhusiano huu kwa kumrejelea Tonge kama *mwanangu*. Kwa kufanya hivi, anashughulikia uso chanya wa Tonge na kumfanya ajihisi yeye ni sehemu moja na baba. Kando na kutekeleza jukumu la kuulinda uso chanya wa Tonge, maneno ya Temba yanadhamiria kuusuluhisha mgogoro baina yake na Tonge ambao unasababishwa na kitendo cha Tonge kukataa kumsamehe Matari.

Katika muktadha mwingine mchezoni, Temba anadhihirisha mbinu hii anapokuwa akizungumza na Tonge. Dayolojia hii inajitokeza kama ifuatavyo:

58. Tonge: Nimesema mwizi mara hii sharti akomeshwe.
Temba: Tonge mwanangu, twende nyumbani mimi
nawe tushauriane kuhusu jambo hili. uk.49.

Katika mfano 58, Tonge anajikuta katika mgogoro baina yake na Tonge kuhusu haja ya Tonge kumsamehe Matari na kumwondolea mashtaka ya wizi wa ng'ombe. Tonge hakubaliani na maoni ya babake hali ambayo inamfanya Temba kutumia mkakati chanya wa upole kama njia ya

kumshswishi. Katika matamshi yake, Temba anajitambulisha na Tonge kwa kusema; *twende nyumbani mimi nawe tushauriane*. Matumizi ya maneno *mimi na wewe* ni dhihirisho kuwa Temba anajihusisha na Tonge kama njia ya kumwonyesha kuwa wanashirikiana katika kushauriana.

### 2.1.7 Kutoa Ahadi au Zawadi

Kulingana na Brown na Levinson (1987:102), Kaida hii huhusisha kuujali uso chanya wa msikilizaji kwa kutoa miadi chanya kwake. Katika kutekeleza hili, msikilizaji hudhamiria kumfanya msikilizaji afurahi na kuhisi anajaliwa hivyo kuendelea kuujenga uhusiano na mzungumzaji. Aidha, mbinu hii inaweza ikahusisha utoaji wa ahadi ya zawadi kwa msikilizaji. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wahusika wakuu wanasawiriwa wakitumia kaida hii kama ifuatavyo:

Kwanza, Matari anatoa ahadi kwa Lila kuwa ingawa hana pesa za kumlipa kwa sasa atamlipa baadaye. Matari anasema:

59. Matari*:* Pesa zako nitakulipa.Saa hii sina. Nipe muda tu. uk.18

Katika mfano 59, Matari anajikuta katika mvutano na Lila ambapo Lila anamlaumu Matari kwa kumwibia pesa zake. Matari anaamua kutafuta maridhiano na dadake kwa kutumia mkakati chanya wa upole.Matari anadhihirisha utoaji wa miadi kwa kutumia kitenzi; *nitakulipa* na kuomba apewe muda zadi kwa kesema; *Nipe muda tu*. Kwa kutumia mkakati huu Matari anafanikiwa kutuliza hasira za Lila na kuyajenga mazingira mazuri ya mawasiliano baina yake na dadake.

Katika mazungumzo baina ya Mama na Lila, Lila anamtuliza mamake anayesononeka kwa sababu ya kukamatwa kwa mwanawe Matari kwa namna ambayo inaweka wazi upole chanya. Lila anamtuliza mamake kwa kumwambia:

60. Lila:Mama usilie Matari yupo salama….Na baba na Tonge
wapo huko wanashauriana kuhusu hatima yake.
Yatakwisha mama. uk 58.

Katika mfano 60, Lila anatumia mkakati chanya wa upole unaodhihirishwa na matumizi ya maneno yanayokusudia kutoa ahadi ya matarajio mazuri; *Matari yupo salama*. Aidha, Lila

anaendelea kutoa ahadi chanya kwa kusema; *Yatakwisha mama* .Kwa kutumia lugha ya aina hii, Lila anampatia mamake matumaini kwa kumhakikishia kuwa mtoto wake yuko salama hivyo kumtuliza na kumfanya ashiriki katika mazungumzo na yeye.

Matumizi ya mkakati chanya wa upole kupitia utoaji wa miadi aidha yanajitokeza katika mazungumzo ya Temba anapokuwa akimfahamisha mkewe kuhusu hali ya Matari.Temba anasema hivi:

61. Temba: Mwanao yuko salama mikononi mwa vyombo vya dola. uk.61.

Katika mazungumzo haya, hali ya mvutano inaibuka pale ambapo Mama anataka kujua ambacho Temba amefanya ili kuhakikisha kuwa mwanawe Matari ameachiliwa.Temba anamhakikishia usalama wa mwanawe kwa kuushughulikia uso chanya wa Mama kwa kumtolea ahadi kuwa Matari yupo salama.Ahadi hii inajidhihirisha kupitia matumizi ya maneno; *Mwanao yuko salama* ambayo ni hakikisho kwa Mama kuwa Matari hajadhuriwa na yeyote.

Kwingineko tamthiliani, Temba anaendelea kutumia mkakati huu anapojaribu kumshawishi Tonge kuiondoa kesi ya Matari inayohusu wizi wa ng'ombe, Temba anasema:

62. Temba: Hebu njoo (Tonge)…Watu wa Jefule wanasema
wako radhi kutoa fidia ya ng'ombe mmoja. uk.62.

Katika mfano 62, Temba anajaribu kuusuluhisha mgogoro baina yake na Tonge kwa kutoa ahadi chanya kuwa ng'ombe aliyeibwa na kuchinjwa atalipwa. Temba anatumia maneno haya; *Watu wa Jefule wanasema wako radhi kutoa fidia ya ng'ombe mmoja*

**2.2 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Upole**

Brown na Levinson (1987:129), wanaeleza kuwa mkakati hasi wa upole hutumiwa ili kuutambua uso hasi wa msikilizaji kwa kuonyesha tofauti iliyopo baina ya msikilizaji na mzungumzaji. Huang (2007:116), anasisitiza mawazo ya Brown na Levinson kwa kusema kuwa, katika kutumia mkakati huu mzungumzaji hana uhuru mkubwa wa kumwingilia msikilizaji ikilinganishwa na mkakati chanya wa upole.Huang anadokeza kuwa, mkakati huu hudhamiria kuondoa ulazimishaji wa kitendo cha kutishia uso kwa msikilizaji.Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* matumizi ya mkakati hasi wa upole na wahusika wakuu kama njia ya kuhifadhi nyuso hasi za wasikilizaji wao yanabainika kupitia mbinu zifuatazo:

### 2.2.1 Matumizi ya Vitangulizi na Vidokezi

Mzungumzaji hulenga kufanikisha mkakati hasi wa upole kwa kutumia vitangulizi na vidokezi ambavyo humtayarisha msikilizaji kuupokea ujumbe wake hata kama ni hasi. Kaida hii hutambulishwa na matumizi ya maneno ya kuomba msamaha pamoja na matumizi ya dhamira tegemezi kama vile: labda, samahani, nafikiri, huenda, -weza miongoni mwa mengine.Matumizi ya vidokezi hivi pia hudhamiria kuonyesha majuto kwa habari ambazo mhusika anataka kuzisema. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* kaida ya matumizi ya vitangulizi na wahusika wakuu inajidhihirisha katika miktadha mbalimbali.Baadhi ya miktadha hii, ni pamoja na:

Kwanza, Lila anapokuwa akimwelezea mama yake sababu ya kukurupuka na kumwacha peke yake anatumia kitangulizi cha kuomba msamaha kabla ya kuelezea sababu yake:

> 63. Lila*:* Samahani mama. Nimefanya kukurupuka hapatu ghafla.
> Sio kupenda kwangu….Samahani mama sio kupenda kwangu
> naomba uniwie radhi. uk.19.

Katika mfano 63, Lila anajaribu kuusuluhisha mvutano unaojitokeza baina yake na Mama kwa kutumia vitangulizi *samahani mama* na *naomba uniwie radhi* vinavyombainishia mama yake kimbele kuwa anakiri kosa lake na hakuwa na uwezo wa kuzua kutokea kwa kosa lake.Aidha, Lila anaonyesha ugumu uliokuwepo katika kuepuka kukurupuka kwake kwa kusema; *Sio kupenda kwangu.*

Vilevile, Lila anadhihirisha matumizi ya mkakati hasi wa upole kupitia matumizi ya vidokezi anapomwambia babake sababu ya kutotimiza agizo lake la kwenda kwa mwalimu.

> 64. Lila*:* Baba! Samahani sana nimepata mengine njiani. uk 25

Lila anamtuliza babake kupitia matumizi ya mkakati hasi wa upole ambao unatambulishwa na matumizi ya maneno; *Baba! Samahani sana*.Katika kauli hii, Lila anatumia mbinu ya mdokezo kuwa alipata mengine ambayo hayasemi, pia anaomba msamaha kwa tendo lake kama njia ya kumdhihirishia babake kuwa hakutimiza agizo lake.Kupitia matumizi ya mkakati huu pia, Lila anadhihirisha hali ya unyenyekevu kwa babake hivyo kuyawekea mazungumzo yao msingi bora wa kuendelea bila kuvunjika licha ya mvutano uliopo.

Katika kumfafanulia Temba kuhusu kukamatwa kwa mwenye bucha kwa tuhuma ya wizi, Lila anamdokezea babake uwezekano wa Matari kuwepo katika wizi ule kwa kusema:

65. Temba: Ati nani mwizi? Aliyepatikana na ng'ombe ndiye mwizi.
Mwenye bucha ndiye mwizi
Lila: Sidhani hivyo baba, mwenye bucha hayupo peke yake.uk.28

Kauli ya Lila inadhihirisha kuwa anampinga babake anayesema kuwa Jefule (mwenye bucha) ndiye mwizi wa ng'ombe lakini hataki kudhihirisha waziwazi jambo hili kwa babake. Badala ya kumpinga babake, Lila anaonyesha hali ya kutokuwa na uhakika na kutoa mkondo mwingine wa mawazo kwa kusema; *Sidhani hivyo baba, mwenye bucha hayupo peke yake.*Hapa Lila anashughulikia uso hasi wa babake kwa kutomwambia moja kwa moja kuwa Matari ndiye aliyempelekea mwenye bucha ng'ombe wa Tonge.

Katika mfano mwingine mchezoni, Mama anatumia vidokezi ili kuulinda uso hasi wa Temba anapobishana naye kuhusu kuchinjwa au kutochinjwa kwa mbuzi kama njia ya kusherehekea kuachiliwa kwa Matari. Mama anajaribu kuumaliza mgogoro huu kwa kutumia mkakati hasi wa upole ambao unatambulishwa na matumizi ya ombi.

66. Temba: Hachinjwi (mbuzi)
Mama: …naomba kitumbua changu msinitilie mchanga.uk.65.

Matumizi ya neno *naomba* kama kitangulizi cha kauli ya Mama kwa Temba kama inavyobainika katika mfano 66 ni njia ya kuomba kuipinga kauli yake lakini kwa namna ambayo inadhihirisha uhifadhi wa uso hasi wa mumewe.Kadhalika, Mama anampinga mumewe kwa kuepuka kumlaumu yeye binafsi badala yake kumhusisha na kikundi kwa kutumia kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi -m- katika *msinitilie*.

Aidha, Temba anadhihirisha matumizi ya mkakati hasi wa upole kwa kutumia vitangulizi. Temba anatekeleza tendo la kutishia uso hasi wa askari ambao wanakuja kumchukua Matari baada ya kumwibia Tonge ng'ombe kwa kusema hivi:

67. Askari II: [Anatishia kumzaba kofi. Nusura Matari aanguke.Anajikusanya
na kusimama mbali kidogo] Unaleta mzaha hapa kwa nini?
Temba: Samahani ofisa. Msilete rabsha hapa nina mgonjwa hapa. uk.31.

Katika dayolojia 67 mgogoro baina ya Temba na Askari II unazuka pale ambapo Askari huyu anajaribu kumzaba kofi Matari kwa kulijibu swali lake kwa mzaha. Temba anaamua kumkosoa

Askari II lakini kwa matumizi ya mkakati hasi wa upole ambao unatambulishwa na matumizi ya maneno; *Samahani ofisa.* Kwa kutumia kauli hii, Temba anadhihirisha kutoridhishwa kwake na kitendo cha askari huyu lakini kwa namna inayonuia kuepusha kuvunjika kwa mazungumzo yao.

Katika mazungumzo mengine, Temba anatumia mkakati huu anapokuwa akibishana na Tonge kuhusu haja yake ya kumwondolea Matari mashtaka ya wizi. Temba anasema:

68. Temba: Naomba tafadhali usinifokee Tonge. uk.47

Katika mfano 68, Mkakati hasi wa upole katika lugha ya Temba yanatambulishwa kupitia matumizi ya maneno; *Naomba tafadhali.* Katika kutumia maneno haya, Temba anaificha hasira yake kwa Tonge hali ambayo inamwezesha kuendelea na juhudi zake za kumshawishi kufanya anachotaka.

**2.2.2 Kutoa Kauli Zisizohusishwa na Mtu Maalum/Kuepuka Viwakilishi Nafsi**

Katika kuutumia mkakati huu Brown na Levinson (1987:131), wanasema kuwa msikilizaji huuhifadhi uso hasi wa msikilizaji kwa kutoa kauli zisizohusishwa na mtu maalum. Kwa msingi huu mzungumzaji huepuka kutumia viwakilishi nafsi vinavyomhusisha msikilizaji wake na kitendo maalum. Kauli za aina hii pia husaidia katika kuokoa uso hasi wa msikilizaji kwa sababu haziathiriwi na hisia.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, Lila anamkosoa Vero kwa kuuhifadhi uso wake hasi kwa kusema:

69. Lila:...naona sote tumeathiriwa na vitimbi vya Matari na sote tumechanganyikiwa. Yaishe haya ati. uk.44.

Katika mfano 69, Lila anatumia mkakati hasi wa upole kwa kumkosoa Vero kwa njia ya kujihusisha na kitendo anachodhamiria kukikosoa. Lila anaepuka kumtaja Vero katika kumkosoa lakini kwa kutumia kiwakilishi nafsi cha nafsi ya kwanza wingi *sote*. Lila anasema; *naona sote tumeathiriwa na vitimbi vya Matari na sote tumechanganyikiwa.* Kwa kujihusisha na kitendo cha kuathirika, Lila anafanikiwa kumkosoa Vero hivyo kuepuka kuendeleza mvutano baina yake na Vero.

Katika mfano mwingine mchezoni, Lila anaepuka kumtaja Matari kama mwizi wa pesa zake kwa njia ya moja kwa moja kwa kuuliza swali ambalo limebeba ujumuishaji ndani yake:

70. Lila*:* Mwizi kazi yake gani kama si kuiba? uk.20.

Kupitia swali katika mfano 70, Lila anadhihirisha hasira yake kupitia matumizi ya swali na kisha kutoa jibu la swali lake. Kwa kutumia mbinu hii, Lila anahakikisha kuwa japo kuna mgogoro baina yake na Matari mazungumzo yao yanaendelea.

Matari pia anatumia mkakati hasi wa upole anapowajumuisha walevi wote katika kumkosoa Mtu II kuhusu maoni yake juu ya mavazi yake.Dayolojia hii inajitokeza kama ifuatavyo:

71. Mtu II: Ndio maanaumebadili mwendo na mavazi…
Sijawahi kukuona unadunda utembeapo kama leo.
Matari: Nikivaa matambara mwanishitumu. Nikivaa nadhifu mwanishutumu.
Nikitembea kwa unyonge mwanishitumu, nikitembea kwa mikogo
mwanishutumu. Mwataka nini? uk.12

Katika mfano 71, Matari anawajumulisha walevi wote badala ya kumwingilia Mtu II kwa njia ya moja kwa moja. Ujumuishaji huu unatambulishwa na matumizi ya kiambishi -mw-.Kiambishi hiki kinarejelea ujumuishaji katika hali ya wingi na kinamsaidia Matari kuepuka matumizi ya kiambishi kiwakilisha cha nafsi ya pili umoja -u- ili kutomkosoa Mtu II kwa namna ya uwazi. Kwa kutumia urejelezi wa aina hii, Matari anafanikiwa kuulinda uso hasi wa Mtu II na wakati uo huo kuzuia kuibua mgogoro ambao utahatarisha uhusiano baina yake na yeye.

Katika sehemu nyingine tamthiliani, Mama anatumia kaida hii katika kuuhifadhi uso hasi wa Matari anapomkosoa kuhusu wizi wake wa kila mara. Mama anasema:

72. Mama*:* ...Hauachi hauachi kwa nini?
…kwa nini kutuaibisha kila uchao mwanangu? uk.20

Matamshi ya Mama katika mfano 72 yanatolewa baada ya kufahamu kuwa Matari amemwibia dadake Lila pesa zake hali ambayo inazua mvutano mkubwa baina yake na Matari. Katika kuutumia mkakati huu, Mama anajihusisha na aibu ya Matari kwa kutumia kiambishi -tu- kinachodhihirisha wingi wa wahusika; *kwa nini ku**tu**aibisha.* Katika kauli yake, Mama anashikilia kuwa japo mwizi ni Matari aibu ya wizi wake ina athari kubwa kwa familia ya Mzee Temba. Aidha, Matari anafanywa kuhisi kuwa wizi wake si tatizo lake peke yake ila linaiathiri

jamii yote. Mama pia anaepuka kumwaibisha Matari kwa kumtaja katika ubinafsi wake kama mwizi hivyo kuuokoa uso wake hasi.

Lila pia anadhihirisha matumizi ya mbinu ya kutumia kauli zisizohusishwa na mtu maalum katika mazungumzo yake na Matari. Katika mazungumzo haya, Lila anamkosoa Matari kwa kumwibia pesa zake na kutaja kitendo hicho kama aibu inayoiathiri familia nzima.

73. Lila…Unatutukanisha sote bure.
Watu wanatucheka kwa sababu ya mkono wako. uk.18.

Katika kauli ; *Unatutukanisha sote* na *Watu wanatucheka,* Lila anajaribu kumshawishi Matari kukomesha vitendo vyake vya wizi kwa kupanua athari ya aibu zinazotokana na wizi wake na kuzihusisha na familia nzima.Kwa kufanya hivi, analinda uso hasi wa Matari hivyo kuepuka kuyavunja mawasiliano yao.

Temba pia anatumia mkakati huu wa kuokoa uso hasi kwa Lila kwa kusema:

74. : Temba: Watoto nyie mtanipandisha kichaa. Kwa nini hukufika? uk25

Katika mfano74, Temba anatumia maneno; *watoto nyie mtanipandisha kichaa*. Temba anazungumza kama vile kauli yake inawarejelea watoto wengi bali anaikusudia kwa mwanawe Lila. Kwa kufanya hivi, Temba anafanikiwa kumkosoa Lila kwa kumjulisha na watoto wengi bila kumwingilia kwa njia ya moja kwa moja.

### 2.2.3 Kubashiri Matokeo Mabaya ya Kitendo

Mbinu hii huhusisha mzungumzaji kumtolea msikilizaji kauli ambayo inamtayarisha kukipokea kitendo cha kutishia uso. Katika kutumia mbinu hii, mzungumzaji humtayarisha msikilizaji kuwa anacholenga kukisema si kizuri, athari zake ni hasi au alitaraji hali fulani kutokea ilivyotokea. Mbinu hii pia huhusisha matumizi ya maneno yanayodhihirisha ubashiri mwingi kama vile: najua, naelewa, naona, inawezekana miongoni mwa maneno na kauli nyingine. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, mbinu hii inajibainisha katika kauli na mazungumzo ya wahusika wakuu kwa mapana, kwa mfano:

Katika mazungumzo baina ya Matari na Mama, Matari anatumia mbinu hii anaposema:

75. Matari*:* Najua unachotaka mama…Najua wataka nikwambie
leo nimekutana na Yesu njiani nikienda kwa Fiona…uk.21

Katika mfano 75, Mama anamtaka Matari kukiri kuwa ameelewa maneno katika maandiko matakatifu ambayo yanamkanya kuiba tena. Katika kuipinga kauli hii, Matari anabashiri matokeo ya kitendo cha Mama kwa kukariri neno *najua*. Katika matumizi haya ya lugha, Matari anamtayarisha Mama yake kimbele kuwa anajua kile anadhamiria. Kwa kufanya hivi, anakataa mapendekezo ya Mama lakini kwa namna ya kutumia mkakati hasi wa upole.Japo Matari anakataa pendekezo la mamake, mazungumzo yao hayavunjiki kwa vile Matari anafanya hivi kwa namna ambayo inahifadhi uso hasi wa mamake.

Katika dayolojia baina ya Lila na Vero katika onyesho la nne, Lila anamdokezea Vero kuhusu haja yake ya kutotaka mabishano kwa kuitanguliza kauli yake kwa maneno ya kumtahadharisha. Lila anasema:

76. Lila: Ni mimi wifi.
Vero: Mbona kunishtua hivi?
Lila: Si makusudi wifi.
Na naomba safari hii tusigombane. uk.41

Katika kauli iliyopo hapo juu, Lila anamtayarisha Vero kuwa huenda hatima ya mazungumzo yao ikawa ni magombano. Lila anafanikiwa kuondoa magombano haya kwa kumtahadharisha Vero kuhusu uwezekano wa wao kugombana kupitia matumizi ya kauli inayodhihirisha ombi; *Na naomba safari hii tusigombane*. Kwa kufanya hivi, Lila anafanikiwa kupunguza mgogoro baina yake na Vero hivyo kuzuia kuvunjika kwa mazungumzo.

Kwingineko tamthiliani, katika dayolojia inayofuata, Lila anatumia mbinu ya ubashiri wa matokeo hasi anapokuwa akizungumza naVero:

77. Lila: Mimi nasema vile wao walivyosema.
Vero: Wewe wasema na kuamini?
Lila: Naona unaanza kunitafuta ushari sasa, sio? uk.44

Katika mfano 77, mgogoro kuhusu sababu ya Vero kushiriki katika mazungumzo yaliyodhamiria kuidumisha familia ya Mzee Temba na Mtu I na Mtu II yanaendelea. Lila anachukua jukumu la kuumaliza mgogoro huu ambao unaonekana kuchukua mkondo mwingine kwa kumtahadharisha Vero kwa kusema; *Naona unaanza kunitafuta ushari sasa,* Lila anajifanya mrijua kwa kubashiri mwelekeo hasi wa mazungumzo yake na Vero hivyo kumkosoa kwa namna inayoashiria upole hasi.

Katika mazungumzo baina ya Lila na mamake kuhusu Matari kupelekwa mjini na kufunguliwa mashtaka ya ubakaji, Lila anatumia mkakati hasi wa upole kwa Mama kwa njia ya kumdokezea uzito wa habari zake kwa kusema:

78. Lila: Najua wewe ni mgonjwa lakini nitakwambia ukweli.uk75

Katika mfano78, Lila analazimika kumfahamisha mamake ukweli wa mambo licha ya kujua kuwa atasononeshwa na habari za kukamatwa kwa mwanawe Matari.Lila anamtayarisha Mama kwa kutumia maneno; *Najua wewe ni mgonjwa* ili kumwashiria mamake kuwa anadhamiria kumfahamisha habari ambazo hazitamfurahisha. Kwa kufanya hivi, Lila anapunguza kiwango cha athari ambazo zitasababishwa na habari zake kwa Mama.

Temba anatumia mbinu hii kudihirisha matumizi ya mkakati hasi wa upole anapokuwa akizungumza na Lila kuhusu wizi wa ng'ombe wa maziwa wa Tonge.  Katika mazungumzo baina ya wahusika hawa wawili, mgogoro kuhusu kuhusika kwa Matari katika wizi unajitokeza. Temba anashikilia kuwa Matari hajahusika huku Lila akibainisha msimamo wake kuhusu kuhusika kwa Matari kwa uwazi. Temba anajaribu kuumaliza mgogoro huu kupitia kumtahadharisha mwanawe Lila dhidi ya kumtuhumu Matari kwa wizi huo kwa kusema:

79.  Temba: Usiwe unaanza kumtuhumu mdogo wako kwa wizi…
Naona macho yako yanaonyesha kuelekeza tuhuma kwa
ndugu yako Matari. uk.28.

Katika mfano 79, Temba anayatambua matokeo hasi ya kauli ya Lila kuhusu wizi wa ng'ombe. Temba anamtayarisha Lila kwa kumwambia kuwa anajua matokeo ya matamshi yake kwa kumwambia; *Naona macho yako yanaonyesha…*Kauli hii pia ni njia ya kumwonya Lila lakini kwa namna ya kuhifadhi uso wake hasi. Kutoka na kauli hii pia, Lila haoni vigumu kuendeleza mazungumzo yake na babake kwa vile kauli ya babake inamtolea mwelekeo.

Katika muktadha mwingine mchezoni, Temba anamwonya askari dhidi ya kutumia gari lake kumpeleka Matari mahakani mjini kwa kusema:

80. Askari I: …Wataka nikwambie mara ngapi nawe?
Labda nyie mtumie gari lenu.
Temba:    Afande, si we wajua hili gari si letu ni langu? uk47.

Temba anamdokezea Askari I kuwa hayuko tayari kulitoa gari lake kumpeleka Matari mahakamani mjini kwa kutumia kauli; *Afande, si we wajua hili gari si letu ni langu?* Katika

kauli hii, Temba anamtayarisha askari kwa matokeo mabaya kuwa ombi lake la msaada wa gari tayari limekataliwa lakini kwa namna ambayo imetilia maanani uso wake hasi.

### 2.2.4 Kuonyesha Staha/Heshima Baina ya Msemaji na Msikilizaji

Mkakati hasi wa upole pia hujibainisha katika matumizi ya lugha wakati ambapo mzungumzaji hudhihirisha tofauti yake na msikilizaji kwa kuonyesha heshima au tofauti ya katika hadhi na mamlaka baina yake na msikilizaji. Kaida hii huingiliana na mawazo ya Leech (1983:132) kuhusu kanuni ya upole ya kujitweza ambapo mzungumzaji hujidunisha na kumsifu msikilizaji. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), kaida hii hudhamiria kuondoa ulazimishaji wa msikilizaji na mzungumzaji kumfanyia jambo fulani.Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu,* kaida hii inabainika katika matumizi ya lugha ya wahusika wakuu katika miktadha kadhaa.

Katika mazungumzo baina ya Matari na walevi katika baa ya Fiona, Matari anatumia mbinu hii anapojidunisha na kuisifu jamaa yake kwa kusema:

81. Mtu I: La! Mzee kwa ajili ya utajiri wenu.
Matari: Lakini chetu si changu.Kila mtu kwetu tajiri isipokuwa mimi. Shamba la baba maddal basari, si kwambii nyumba za kupangisha kwenye kituo cha kibiashara na mjini, matatu…na…kadhalika na kadhalika…. Isitoshe kaka Tonge ana shamba la kupigiwa mfano…Mimi Matari kwa maana ya Mburumatari. Maskini hali yangu…uk 13-14.

Katika maelezo kwenye dondoo 81, Matari anapinga kauli ya Mtu I kuwa yeye ni tajiri kwa kujitenga na familia ya Mzee Temba. Matari anamsifu babake na kaka yake Tonge na kujidunisha, japo hawako pale.Matamshi ya Matari yanaashiria matumizi ya mkakati hasi wa upole hasa kwa wanaozungumza nao.  Matari anarejelea utajiri wa babake kwa kusema; *Shamba la baba maddal basari, si kwambii nyumba za kupangisha kwenye kituo cha kibiashara na mjini, matatu...* Aidha, Matari anajidunisha kwa kusema; *Mimi Matari kwa maana ya mburumatari. Maskini hali yangu.* Kwa tathimini ya ndani ya kauli hii, Matari anahalalisha tabia yake ya kuiba kuwa inatokana na umaskini wake. Walevi wanaishia kumwonea huruma na kumwona kama mshirika wao katika mazungumzo yao.

### 2.2.5 Kutaja Kitendo Kinachotishia Uso Kama Kanuni ya Jumla

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa, mzungumzaji anaweza akashughulikia tendo la kutishia uso hasi wa msikilizaji kwa kutaja kitendo kinachotishia uso kama kanuni ya jumla au ukweli unaojulikana.Kutaja kitendo hicho kama kaida ya jamii kunaokoa uso hasi kwa sababu msikilizaji anachukulia kuwa jambo husika halimhusu yeye pekee bali wanajamii wote. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu,* wahusika wakuu wanatumia kanuni ya jumla katika mazungumzo yao na wengine kwa nia ya kuokoa nyuso zao hasi.

Kwanza, Lila anakataa maoni ya mama kuhusu kuolewa kwa kutumia kanuni ya jumla kuwarejelea wanaume, anasema hivi:

82. Lila: Muhali mama, muhali.Nilikwambia sitaki kuolewa.
Sitaki maisha ya kusumbuliwa na wanaume..Wanau...uk.31.

Katika kauli 82, Lila anamfanya Mama kuamini kuwa sababu yake ya kukataa kuolewa ni kuwa wanaume wote ni wasumbufu; *Sitaki maisha ya kusumbuliwa na wanaume…* Lila anajua uzito uliopo wa kumwambia Mama kuwa hataki kuolewa hivyo anatumia kanuni ya kijumla kumjibu mamake. Kwa kusema hivi, Lila anaepuka kumuudhi Mama kwa kulipinga pendekezo lake kuhusu ndoa, hivyo kuuhifadhi uso wake hasi. Hii inakuwa sehemu ya kudhibiti kuvunjika kwa mawasiliano baina ya wahusika hawa kwa vile wote wanazingatia uhifadhi wa uso hasi wa kila mmoja wao.

Pili, Mama anatumia kanuni ya jumla kumkumbusha Lila kuhusu umuhimu wa kuolewa kwa kutoa kauli zinazothibitisha kanuni ya jumla ambayo inaaminika na wanajamii kuwa ya kweli. Katika mazungumzo yanayotawaliwa na mgogoro mkubwa, Mama anatumia mkakati hasi wa upole kama ifuatavyo:

83. Mama: Lakini ujue amri ya umri. Wewe si mtoto tena…utakuja kuchelewa
kuolewa ubaki kuhangaika kama usipotahadhari. uk.31
Kuishi bila kuolewa na bila kuzaa ni laana tupu. uk32
Ndoa ni kitu cha lazima kwa mwanadamu mwanangu. Kuikataa ni
kushindana na maumbile.Ajabu ya shingo kukataa kulala chini. uk.33

Katika mfano 83, Mama anatumia mkakati hasi wa upole kwa namna ya tahadhari ili kuuhifadhi uso hasi wa Lila. Mama anakihusisha kitendo cha kukataa kuolewa na laana kwa kusema; *Kuishi bila kuolewa na bila kuzaa ni laana tupu.*Pia, anasisitiza kauli yake kwa kuirejelea ndoa kama

kitu cha lazima kwa kusema; *Ndoa ni kitu cha lazima kwa mwanadamu mwanangu*. Japo Mama anamkosoa Lila kwa kuchelewa katika ndoa, Lila hadhuriki kama ambavyo ingekuwa Mama angemwambia aolewe moja kwa moja.Mama anatenda tendo nzito la kutishia uso wa Lila lakini mazungumzo yao hayaathiriwi kwa vile Mama anatenda tendo hili kwa namna inayodhihirisha ushughulikiaji wa uso hasi wa Lila.

Katika muktadha mwingine tamthiliani, Temba anatumia kaida ya kanuni ya jumla kudhihirisha mkakati hasi wa upole anapojaribu kumshawishi Tonge kukubali kumwondolea Matari kesi kwa kusema:

84. Temba*:* ...kama kaibwa ng'ombe kaibwa. Kama kachinjwa ng'ombe kachinjwa.Ungeyachia tu hapo mwanangu. Maji yakimwagika hayazoleki. Tena meno ya mbwa hayaumani.uk.46.

Kwenye mfano 84, Temba anatekeleza tendo la kutishia uso hasi wa Tonge kwa kurejelea ukweli wa jumla kuwa ng'ombe aliyechinjwa hawezi akarejeshwa hai; *Kama kachinjwa ng'ombe kachinjwa.*Aidha, Temba anathibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea methali; maji *yakimwagika hayazoleki*. Katika kumwonyesha haja ya kuitupilia mbali kesi ya Matari, Temba anarejelea kanuni ya jumla kwa kunukuu methali; *meno ya mbwa hayaumani*.Kwa kutumia kauli hizi Temba anafanikiwa kupunguza hali ya mvutano inayotawala mazungumzo baina yake na Tonge kuhusu kesi inayomkabili Matari.

### 2.2.6 Kupunguza Ulazimishaji wa Kauli

Msemaji pia huokoa uso hasi wa msikilizaji kwa kutumia maneno ambayo yanaashiria msikilizaji wake kuwa hamlazimishi kuupokea ujumbe wake.Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.* wahusika wakuu wanathibitisha matumizi ya mbinu hii kwa namna kadhaa kwa mfano:

Matari anapoongea na Lila anamwomba kutosema kwa sauti ili mamake asisikie kuwa anahusishwa na wizi kwa kusema.

85. Lila…Nilipe. Nirejeshee pesa zangu.

Matari:…Basi usiseme kwa sauti mama atasikia.uk18

Katika kauli hii, Matari anatumia neno *basi* kama njia ya kumwonyesha Lila kuwa yeye anatoa ombi wala hamlazimishi Lila kutomwambia mama yake kuhusu kisa cha wizi wa pesa. Kwa kufanya hili, Matari anafanikiwa kuyajenga mazingira mazuri ya mawasiliano kwa vile

anahusisha hiari na maoni ya mwenzake katika kauli yake.Mgogoro ambao unatawala mazungumzo baina ya Lila na Matari na ambao chanzo chake ni Matari unamfanya Matari kutumia mkakati hasi wa upole kama njia ya kumtuliza Lila.

Katika sehemu nyingine tamthiliani, Lila anamwomba Vero kuepuka uzushi kwa kutumia mkakati hasi wa upole unaoweka wazi hali ya uepukaji wa ulazimishaji wa hali ya juu. Lila anamwambia Vero:

86. Vero: Ulikuwa ukifanya nini pale chini ya mti?
Lila: Nimesema mbona tusiepuke kugombana safari hii. uk41

Katika mfano 86, mgogoro baina ya Lila na Vero kuhusu Vero kushiriki mazungumzo yenye kudunisha familia ya Mzee Temba na Mtu I na Mtu II unajibainisha.Maneno ya Lila yanakuwa kama tahadharisho kwa Vero kuwa hataki magombano.Hata hivyo, Lila anayatoa maneno yake kwa namna ambayo inadhihirisha upole hasi kufuatia matumizi ya neno *mbona* ambalo linapunguza hali ya ulazimishaji kwa mwenzake.

Aidha, mazungumzo baina ya Mama na Lila yanatawaliwa na matumizi ya upole hasi, Katika mazungumzo baina ya Lila na Mama, Mama anakasirishwa na kukurupuka ghafla kwa Lila hali ambayo inazua mvutano baina ya wahusika hawa wawili. Mama anamwambia Lila:

87. Mama: Afadhali urejee kule mjini unakofanya kazi kuliko kujifanya waja kuniuguza hali, kumbe wanizidishia machungu. uk19

Katika mfano 87, Mama anatumia neno *afadhali'* kwa makusudi kama njia ya kuukoa uso hasi wa Lila ambao unakabiliwa na tishio la kuhasiriwa na matamshi yake. Badala ya Mama kumfukuza Lila nyumbani kwa kauli ya moja kwa moja anampatia hiari ya kurejea mjini. Mama pia anamwambia Lila sababu ya kumwambia hivi kama njia ya kupunguza uzito wa kauli yake.

Katika muktadha mwingine tamthiliani, Temba anamkumbusha Lila haja ya kuamka mapema keshoe kwenda kumdaia deni kwa njia inayoonyesha matumizi ya mkakati hasi wa upole. Kwa vile Temba anafahamu kitendo hiki huenda kikamkasirisha Lila, anaishia kumwambia Lila hivi:

88. Temba: Usisahau kurauka mapema kesho kwenda sokoni kunidaia deni kwa yule mwalimu mpangaji asiyelipa kodi. Umesikia? uk23

Katika mfano 88, Temba anadai kuwa anamkumbusha Lila kuhusu sababu ya kuamka mapema kwa kutumia neno *usisahau* kwa vile hataki kuonyesha kuwa anamlazimisha kumfanyia hivyo.Ili kuhakikisha Lila ameupata ujumbe wake, Temba anamalizia kwa kuuliza swali; *Umesikia?* Kwa kutumia mkakati huu, Temba anafanya kitendo chake kuonekana kama hiari yake na wala si kulazimishwa hivyo.

### 2.2.7 Kuuliza Maswali

Kaida hii kama njia ya kuuhifadhi uso hasi wa msikilizaji huhusisha mzungumzaji kumwuliza msikilizaji maswali hasa kwa nia ya kutaka kuthibitisha kuwa amekubaliana na kile ambacho kimesemwa. Aghalabu mbinu hii hutambuliwa kwa matumizi ya maneno na vishikizo katika mwisho wa sentensi. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu,* wahusika wakuu wanatumia mkakati huu katika kukabiliana na vitendo vya kutishia uso hasi wa wasikilizaji wao wanapozungumza.Kwa mfano:

Lila anamwuliza Matari swali baada ya Matari kumwomba Lila asiongee kwa sauti kubwa ili Mama asisikie. Lila anamwuliza: *Mbona asisikie?* uk.18. Swali hili linalenga kuuhifadhi uso hasi wa Matari.Kwa kutumia swali hili pia, Lila anamdokezea Matari kuwa ana nia ya kumjulisha mamake ukweli japo haiweki bayana nia yake.

Kwingineko tamthiliani, Mama anatumia mkakati huu anapokuwa akijaribu kumkosoa Matari kwa kumwibia Lila pesa. Mama anapotaka kuhakikisha kuwa Matari ameyasoma maandiko matakatifu na kuyaelewa anamuliza Matari maswali:

89. Mama: Andiko linasema nini?
Umeelewa?
Nauliza umeelewa hilo? uk.21

Katika mfano 89, Mama anatumia maswali; *umeelewa? andiko linasema nini?* kama njia ya kumshirikisha Matari kwenye mazungumzo na kuhakikisha kuwa anayazingatia mazungumzo yao.

Katika mazungumzo baina ya Lila na Vero, mbinu hii inadhihirika pale ambapo Lila anatumia maswali kutaka kuthibitisha kuwa Vero anaelewa kile ambacho anamwuliza. Katika kutimiza

hili, Lila anapomuliza Vero kama ana maoni yoyote kuhusu vitendo vya Matari, anamwuliza kwa namna inayoashiria kuwa tayari ana maoni kuhusu jambo hilo.

90. Vero: Samahani. Siwezi kutoa maoni yangu kuhusu hilo.
    Lila: Lakini una maoni sio? uk43

Katika dayolojia 90, mgogoro baina ya Lila na Vero unabainika ambapo Lila anaonekana kumlazimisha Vero kukubaliana na kauli zake kwa kutumia swali; *Lakini una maoni sio?* mwishoni mwa kauli yake. Hata ingawa hali ni hii, mazungumzo baina ya wahusika hawa yanaendelea kwa vile Lila anaondoa ulazimishaji kwa kutaka kujua maoni ya Vero kwa njia ya swali.

### 2.3 Matumizi ya Mkakati Nje ya Rekodi

#### 2.3.1 Matumizi ya Maswali ya Balagha

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), katika kutumia kaida hii ili kuafikia uhifadhi wa uso hasi wa msikilizaji, mzungumzaji hutumia maswali ya balagha yanayolenga kumwonyesha msikilizaji ukweli wa kile anachokiseama.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu,* mbinu hii imetawala katika matumizi ya lugha ya wahusika wakuu. Kwa mfano, katika kikao cha walevi pale katika baa ya Fiona, Mtu II anamwuliza Matari iwapo hajasikia kuwa kakake Tonge hana uwezo wa kumtia mimba mkewe Vero, Matari anamjibu kwa swali kwa kusema:

91. Mtu II:Hujasikia watu wakisema kakako hawezi,
    amekatika waya ama wasemavyo siku hizi hana network.
    Matari: Sasa hayo ni mambo gani ya kusemwa mbele ya watu? uk.13

Katika mfano 91, Matari anamkosoa Mtu II kwa njia ya swali; *Sasa hayo ni mambo gani ya kusemwa mbele ya watu?* badala ya kumkosoa moja kwa moja. Katika swali hili pia, Matari anamlaumu Mtu II kwa kuyasema mambo ya unyumba mbele ya watu lakini anaiweka lawama yake katika mtindo wa swali.Kwa kufanya hivi, Matari anahifadhi uso hasi wa Mtu II na vilevile nyuso hasi za wahusika wengine katika baa ya Fiona.

Katika mgogoro baina ya Matari na Lila kuhusu Matari kumwibia Lila pesa zake, Matari anaambiwa na Lila ampe pesa zake naye Matari anamjibu kwa swali balagha:

92. Matari:Yaani mimi mwehu kiasi gani hata
nikuibie wewe dadangu ilhali mama ni
mgonjwa hali yake taabani? uk.15

Matumizi ya swali na Matari kama inavyobainika katika mfano 92 yanadhamiria kuhifadhi uso hasi wa Lila kwa kukataa na kupinga madai yake kuwa Matari ndiye mwizi. Matari anajaribu kutumia kauli potoshi yenye kumfunga macho Lila kwa kumwonyesha Lila kuwa hawezi kumwibia kutokana na hali kuwa yeye ni dadake; *nikuibie wewe dadangu* na mamake ni mgonjwa; *mama ni mgonjwa hali yake taabani?* Matari aidha anatumia mkakati huu, kumtuliza Lila ambaye ameghadhabishwa na kitendo cha Matari kumwibia pesa.

Katika mazungumzo haya pia, Matari anadumisha mazingira mazuri ya mawasiliano kwa kukosoa kitendo cha Lila cha kumdai pesa mbele ya umma kwa kutumia swali la balagha ambalo linalenga kuhifadhi uso wake hasi;

93. Matari: Lakini mbona kuja kunidai mbele ya umma mzima.
Huoni unanifedhehesha bure bilashi?
Kwa nini kunizingizia wizi basi? uk.20

Katika mfano 93, Matari anauliza Lila maswali; *Huoni unanifedhehesha bure bilashi?* na *Kwa nini kunizingizia wizi basi?*Kupitia maswali haya, Matari anageuza mkondo wa mazungumzo na kuanza kumlaumu Lila ambaye kwa upande wake anamlaumu Matari kwa kumwibia pesa zake.Hata ingawa hali ni hivyo, Matari  anapunguza makali ya kauli yake kwa kuiweka kama swali.

Lila ni mhusika mwingine ambaye anadhihirisha matumizi ya mkakati wa upole nje ya rekodi kwa kutumia maswali balagha. Katika mazungumzo baina yake na Matari, Lila anamkosoa Matari kwa kumfanya amwache mamake ambaye ni mgonjwa na kwenda kumfuata ulevini kwa kumuliza swali la balagha.

94. Lila…waona vile mama ananigombeza kwa kumwacha ghafla? uk.20

Katika mfano 94, Lila anamlaumu Matari kwa kumuliza swali ili kupunguza athari za tendo lake hivyo kuushughulikia uso wake. Hii ina maana kuwa, hata ingawa Lila anamkosoa Matari mazungumzo yao yanadumishwa kwa vile Lila anatambua uso hasi wa Matari.

Katika muktadha mwingine tamthiliani, Lila anapozungumza na Vero kumfahamisha jinsi ambavyo Mtu I na II walivyokuwa wakiisengenya familia ya Temba, Vero anamuliza Lila kile ambacho Mtu I na II walikuwa wakisema, Lila anamjibu kwa swali la balagha:

95. Vero:…walisema nini? Walisema nini kukuhusu?
Walisema wewe bikira na umri wa miaka arobaini? Sivyo?
Lila: Ulitaka waseme nini? uk44.

Katika dayolojia 95, mgogoro baina ya wahusika hawa wawili unabainika kupitia kauli na maswali ya dhihaka wanayoyatumia.Lila anadhihirisha hasira yake lakini kwa namna ya kutumia swalila la balagha; *Ulitaka waseme nini?* ambalo tayari Vero anajua jibu lake. Japo mazungumzo haya yanakabiliwa na tisho la kuvunjika, Lila anayadhibiti kwa kutumia mkakati wa upole nje ya rekodi kupitia swali la balagha analolitumia.

Katika mazungumzo baina ya Mama na Matari kuhusu sababu ya babake Matari kwenda sokoni, Mama anapalilia msingi mzuri wa mazungumzo baina yake na mwanawe kwa kumhusisha Matari na wizi lakini kwa namna ambayo inabainisha upole hasi.Mama anamwuliza Matari:

96. Mama: Kwa nini babako kenda kununua vipuli? uk19

Katika swali linalobainika katika mfano 96, ni wazi kuwa Mama anafahamu kuwa Matari ndiye mwizi wa vipuli vya gari la Mzee Temba. Hata hivyo, anamdokezea Matari ukweli huu kwa kuficha ukweli wake kwenye swali hili. Kupitia swali hili, Matari anafahamu kuwa yeye ndiye mtuhumiwa mkuu wa wizi wa vipuli japo Mama hajamtaja moja kwa moja. Mama anafanikiwa kudumisha uhusiano na mwanawe kwa kuuhifadhi uso hasi wa Matari kwa kutomwita mwizi moja kwa moja.

Temba ni mhusika mwingine ambaye anatumia mkakati hasi wa upole kudhibiti mazungumzo. Anapokuwa akisimuliwa na Lila kisa cha kuibiwa kwa ng'ombe wa maziwa wa Tonge. Temba anamkosoa Lila anaposema kuwa ng'ombe wa Tonge alikuwa mjamzito kwa kumuliza Lila

97. Temba: Tangu lini ng'ombe akawa mjamzito? uk26

Katika kauli 97, Temba anajua kuwa Lila amekosea lakini badala ya kumkosoa kwa njia ya moja kwa moja anamkosoa kwa swali ambalo pia linajumuisha neno sahihi ambalo Lila anafaa kutumia. Katika kuuliza swali hili, Temba anauhifadhi uso hasi wa Lila ambaye angekasirika na kusitisha mazungumzo yake kama Temba angemkosoa kwa njia ya moja kwa moja.

Katika mazungumzo haya pia, Temba anashangazwa na kitendo cha Vero kuharakisha kumfuata mwizi wa ng'ombe pale sokoni kwa kuliza swali:

98. Temba: Ila kwa sasa nauliza kwa nini mbio zote
hizi naye huyu mkazamwana ni mjamzito? uk 27

Kauli iliyopo hapo juu, inadhihirisha matumizi ya mkakati hasi wa upole na Temba kwa vile anakwepa kumlaumu mkazamwana wake (Vero) kwa njia ya moja kwa moja na wakati uo huo kudhihirishia Lila kuwa yeye ni sehemu ya mazungumzo yake.

### 2.3.2 Matumizi ya Semi

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* mkakati nje ya rekodi unatambulika katika lugha ya wahusika wakuu kwa njia ya matumizi ya semi na methali, kwa mfano, Matari anatumia msemo kumkosoa Mtu II anapotaka Matari kufafanua kama alilala kwa kakake. Matari anasema:

99. Mtu II: [Anadakia mazungumzo] Yaani usiku wa
kuamkia leo umelaza kwa kakako?
Matari: Wacha kuniuliza maswali ya kijinga kama polisi.uk12

Katika kauli ya Matari, mfano 99, hasira ya Matari inabainika lakini kwa namna ambayo inadhihirisha uhifadhi wa uso hasi wa Mtu II. Matari anatumia tamathali za lugha zinazomthibitishia Mtu II kuwa hataki kuulizwa maswali. Upole wa Matari unabainika kwa kutumia kauli; *maswali ya kijinga* pamoja na msemo *kama polisi*. Kupitia misemo hii, Matari anaashiria Mtu II kuwa sio kwamba hataki kulizwa maswali ila anachochukia ni maswali mengi ya kijinga.

Kauli ya Matari pia inaibua ucheshi hali ambayo inaficha ukali wa dhamira ya kauli yenyewe.Aidha, kauli hii inalenga kumfahamisha Mtu II kuwa Matari hataki kuzungumzia mada husika kwa vile inahusu mahusiano yake haramu na Vero. Mkakati huu unakuwa njia ya kudumisha mazungumzo ya Matari na walevi kwa vile anadhibiti hali zinazoweza kutishia kuvunjika kwake.

Katika mazungumzo ya Matari na Mtu II, Matari anamzuia Mtu II kuongea kuhusu mahusiano yake na Vero pale ambapo Mtu II anapomsengenya Tonge kuwa hana uwezo wa kumtia mimba mkewe Vero.Dayolojia inajitokeza ifuatavyo:

100. Mtu II: Hujasikia watu wakisema kakako hawezi,
amekatika waya ama wasemavyo siku hizi hana network.
Matari: Sasa hayo ni mambo gani ya kusema mbele za watu?
Za upenuni hazisemwi njiani ati. uk13

Katika mfano 100, Matari anadhihirisha upole hasi kwa Mtu II kwa kutumia msemo; *Za upenuni hazisemwi njiani ati* kama sababu ya kumzuia Mtu II kuzungumzia mada husika. Katika kutoa kauli hii, Matari ametenda tendo la kutishia uso hasi wa Mtu II kwa kumpinga lakini kwa njia ya kutumia msemo.

Katika muktadha mwingine mchezoni, Matari anaelezea kitendo chake cha kumwibia Lila kwa namna ambayo inadhihirisha matumizi ya mkakati hasi wa kuokoa uso nje ya rekodi kwa wasikilizaji wake ambao ni walevi katika baa ya Fiona.

101. Matari: Mungu ni mkubwa ati. Basi napita hivi nikaona.
Mungu si Athumani.Utajiri nisiouangukia wala kuuamkia.
Riziki kama bahati huitambui ijapo ati.uk 14

Katika mfano 101, Matari anatumia misemo, methali na tashbihi kuwathibitishia wenzake kuwa yeye hakuiba ila alizipata pesa zile kwa kudura na bahati ya Mungu. Kwanza, anatumia methali; *Mungu si Athumani* na kukihalalisha kitendo chake cha wizi. Aidha, Matari anatumia tashbihi; *Riziki kama bahati huitambui ijapo*na kujieleza kama mhusika mwenye bahati.Matari anatumia tamathali hizi za lugha kwa vile anaelewa fika kuwa kitendo chake cha kuiba kitawaudhi wenzake akikieleza kwa njia ya moja kwa moja. Kutokana na hali hii Matari anatekeleza kitendo hiki cha kutishia uso hasi wa wasikilizaji kwa njia ya kukihalalisha kwa methali na misemo.

Katika mazungumzo baina ya Lila na Vero, Lila anaulinda uso hasi wa Vero kwa kutumia misemo kumfahamisha Vero kuwa Mtu I na Mtu II walikuwa wakimsengenya yeye na mumewe.

102. Vero: Walisema nini?
Lila: Mambo ya aibu siwezi kukuambia.
Mbona wewe umewapa pesa?
Vero: Kwani uliona nikiwapa pesa?
Lila: Si kuona tu. Nimeyasikia mazungumzo yenu. Unakubali wakupake
mafuta kwa mgongo wa chupa. Wewe unawaamini hawa unadhani
ukihuzunika wanahuzunika nawe? …Unahadaiwa kwa rangi hali
utamu wa chai sukari. Ila tuachane na hayo. uk42

Katika mazungumzo yaliyo hapo juu, Lila anaonyesha udhaifu wa Vero wa kutoweza kutambua kuwa Mtu I na Mtu II walikuwa wakimchimba bila yeye kufahamu kwa kutumia msemo; *Unakubali wakupake mafuta kwa mgongo wa chupa* unaodhamiria kumfungua macho kuuona ukweli huu.Pia, anatumia methali; *Unahadaiwa kwa rangi hali utamu wa chai sukari* ambayo inalenga kumwelezea Vero kuwa sifa anazopewa na Mtu I na Mtu II ni za uongo.Kwa kutumia mbinu hii, Lila anafanikiwa kupunguza makali ambayo yangekuwepo kama angemwambia Vero kuwa anafurahia mazungumzo ya Mtu I na Mtu II ilhali walikuwa wakimsengenya. Hii ni njia mojawapo ya Lila kumwelimisha shemeji yake Vero lakini kwa njia ya upole na bila kuhatarisha kuyavunja mazungumzo yao.

### 2.3.3 Kutoa Maelezo Pungufu katika Usemi

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa, mkakati nje ya rekodi huhusisha matumizi ya mbinu ya mzungumzaji kutoa maelezo pungufu katika usemi au kauli yake. Kaida hii hudhamiria kupunguza uzito wa tendo la kutishia uso hasi ikiwa tendo lenyewe lina athari kubwa zaidi katika kutishia uso. Katika mbinu hii, msikilizaji hudokezewa kauli na msemaji na kuachwa ajijazie mwenyewe. Wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanatumia mkakati huu kama njia ya kufanikisha mazungumzo ifuatavyo:

Kwanza, Lila anatoa maelezo pungufu kama njia ya kuulinda uso hasi wa Mama anapoulizwa na Mama alikotoka.Mazungumzo baina ya Lila na Mama yanajitokeza ifuatavyo:

103. Mama: Lila umetoka wapi?
Lila: Hapa na pale.
Mama: Hivyo ndivyo kusemaje? uk 58

Katika dayolojia 103, Lila anatumia maelezo pungufu; *Hapa na pale* kama njia ya kuepuka kuuhasiri uso hasi wa Mama. Lila anaelewa fika kuwa mamake anatarjia kuwa ametembea kwingi kamtafuta Matari kama alivyotakiwa. Hata hivyo, Lila hajafaulu katika hili hali ambayo inamfanya Lila kuongea bila kufafanua maelezo yake. Kwa kutoa maelezo pungufu, LiLa anamwachia Mama kujijazia kuwa Lila hajafaulu kumpata Matari badala ya Lila mwenyewe kufanya hivi. Mazungumzo ya wahusika hawa yanafaulu licha ya hali ya mgogoro inayoyatawala kwa sababu Lila anajaribu iwezekanavyo kuulinda uso hasi wa Mama kwa kutoa maelezo pungufu.

Pili, Lila anatumia mbinu hii ya kutoa maelezo pungufu kama mkakati wa kuokoa uso hasi nje ya rekodi  anapokuwa akizungumza na Temba kuhusu uwezekano wa Matari kuwa mshukiwa wa wizi wa ng'ombe wa Tonge. Temba anaposisitiza kuwa Jefule ndiye mwizi Lila anasema hivi:

104. Temba: Ati nani mwizi? Aliyepatikana na ng'ombe ndiye mwizi. Mwenye bucha ndiye.
Lila: Sidhani hivyo baba. Mwenye bucha hayupo peke yake. uk28

Katika dayolojia 104, Lila anakwepa kusema moja kwa moja kuwa Matari ni mshukiwa kwa kuwa walishirikiana na Jefule katika wizi wa ng'ombe kwa kusema*; mwenye bucha hayupo peke yake.*Lila anafahamu kuwa maelezo yake kwa babake ni finyu kuweza kueleweka. Hata hivyo, anatumia lugha ya aina hii kama njia ya kuulinda uso hasi wa babake ambaye atadhuriwa na Lila kwa kumtaja Matari moja kwa moja.Kwa msingi huu, Lila anatumia maelezo pungufu kuokoa uso wa babake na kuepuka kuvunja mazungumzo yao.

**2.3.4 Kuongea kwa Namna ya Mzunguko**

Mkakati huu kama njia ya kuuhifadhi uso hasi wa msikilizaji huhusisha matumizi ya maelezo mengi badala ya kwenda moja kwa moja kwenye mada inayohusika. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wahusika wakuu wanatumia mkakati huu kama njia ya kuepuka kuhasiri nyuso hasi za wasikilizaji wao hivyo kujenga mazingira mazuri ya kufanikisha na kudumisha mawasiliano yao. Lila anatumia maelezo ya mzunguko anapotaka kumfahamisha Mama yake kuhusu sababu yake ya kukurupuka ghafla bila kumjulisha. Badala ya kumwambia kuwa alikuwa akimfuata Matari aliyekuwa amemwibia pesa zake anasema hivi:

105. Lila: Eeh! Hebu mwambie mama ulichonifanyia. Mwambie mwenyewe…Kwa nini basi ukishajua hivyo ukanitenda ulivyonitenda? Mama tazama pochi yangu pale karibu na Biblia [kwa Matari]mwambie mama kwa nini ipo tupu….Hebu basi mwambie mama nimemwacha kukufuatia huko kwa nini? uk.20

Katika mfano 105, Lila anatenda tendo la kutishia uso hasi wa Mama kwa kutumia mkakati hasi wa upole. Anatumia mbinu ya mzunguko kuwasilisha ujumbe kuwa, sababu ya yeye kukurupuka ni kumfuata Matari ambaye amemwibia pesa zake zilizokuwa kwenye pochi. Hata hivyo, kutokana na hali kwamba Mama yuko katika hali mbaya kiafya anatumia maneno mengi kuieleza hali hii. Aidha, kutokana na kutotaka kumwaibisha Matari kwa mamake Lila

analazimika kutumia lugha ya kimzunguko ambayo inamdokezea Mama kuwa kukurupuka kwa Lila kulikuwa na sababu. Katika mazungumzo haya uso hasi wa Mama unaokolewa.

Katika muktadha mwingine tamthiliani, Matari anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi kwa kutoa maelezo ya mzunguko anapojikuta katika mvutano baina yake na Mama. Matari anakosolewa na Mama kwa kumwibia dadake Lila pesa kwa njia ya kuambiwa asome Biblia na kuelezea inachosema. Matari anapoulizwa na mamake kama ameelewa maandiko yanavyosema anatumia mbinu ya mzunguko kulijibu swali la Mama.

106. Mama: Nakuuliza kama umeelewa hilo…? Au umelewa?
Matari: [Anaiacha hulka ya kilokole na kuwa mkaidi tena] Si hoja kama nimeelewa au nimelewa; yote mamoja. Najua unachotaka mama. Unataka niseme nimeokoka na kumkubali Yesu na kadhalika.Wataka nikwambie nikwambie leo nimekutana na Yesu njiani nikienda kwa Fiona kugeuza maji au chang'aa? Unafikiri kama Yesu asingalikuwa rafiki Yangu ningekuwa hai? uk.21

Katika mazungumzo ya mfano 106, Matari anaokoa uso hasi wa Mama kwa kutojibu swali lake moja kwa moja.Badala yake, Matari anasimulia kuhusu Yesu kuwa rafiki yake na jinsi alivyookoka kuuliwa na umma baada ya kumwibia mama mzee shilingi kumi. Matari anatumia maelezo haya kimakusudi ili kukwepa swali aliloulizwa.Aidha, kupitia mbinu hii Matari anafanikisha mazungumzo yake na Mama ambayo yanakabiliwa na tishio la kuvunjika kwa kushughulikia uso hasi wa Mama ambao.

Lila pia anatumia mbinu ya mzunguko katika kutekeleza tendo la kutishia uso wa babake nje ya rekodi. Anapoulizwa na babake sababu ya kutoenda kumchukulia babake kodi ya nyumba kwa mwalimu anatoa maelezo mengi kuhusu jinsi walivyokutana na Vero akielekea sokoni.Lila anamzungusha babake kwa kusema mambo nusunusu:

107. Lila: Baba! Samahani sana lakini nimepata mengine.
Temba: Mengine gani?
Lila: Tonge
Temba: Nini Tonge?
Lila: Ng'ombe wa ndugu yangu Tonge.
Temba: Lila!
Lila: Naam, baba
Temba:…Acha kunizungusha kwa maneno.Wanipeleka huku na huko kama mpira uwanjani kwa nini?uk. 25-26

Katika dayolojia 107, Lila anamzungusha babake kwa sababu ya uzito wa habari ambazo anataka kumfahamisha. Lila hataki kumwambia babake sababu yake ya kutoenda kwa mwalimu kwa njia ya moja kwa moja ila babake anasisitiza kuelezwa mambo kwa njia ya moja kwa moja. Katika kujaribu kuumaliza mjadala huu, Lila anatumia mkakati hasi wa upole kwa kutoa maelezo mengi kuhusu makutano yake na shemeji yake Vero sokoni.

### 2.3.5 Kupuuza au Kubadilisha Mada ya Mazungumzo

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), katika kutekeleza mkakati huu mzungumzaji hubadilisha mada ya mazungumzo ikiwa mada yenyewe inahusisha kiwango cha juu cha kutishia uso wa mzungumzaji. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wahusika wakuu wanahusisha mkakati huu katika mazungumzo yao ili kuepuka kuhasiri nyuso hasi za wasikilizaji wao.

Lila anavunja mkondo wa mazungumzo anapoulizwa na mamake ni mwana wa nani aliyekuja kumwoa kwa kuahirisha mada ya ndoa.

108. Mama: Lila!
Lila: Bee Mama.
Mama: Ni mwana wa nani aliyekuja kukuposa?
Lila: Mama hayo tuyazungumze baadaye. uk31

Katika dayolojia 108, Lila anatumia mkakati huu wa kupuuza mada ya mazungumzo kwa kuiahirisha; *Mama hayo tuyazungumze baadaye.*Katika kufanya hivi, Lila anadhamiria kuokoa uso hasi wa Mama kwa kuikataa mada ya Mama na wakati uo huo kumpatia matumaini ya kuirejelea baadaye. Lila anafanikiwa kuuokoa uso wa mamake kupitia mbinu hii kuliko jinsi ambavyo ingekuwa angempinga Mama kwa njia ya moja kwa moja. Kwa upande mwingine, mada ya Mama inauhasiri uso hasi wa Lila hivyo anaipuuza kimakusudi.

Katika muktadha mwingine katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, Lila anatumia mkakati huu anapokuwa akizungumza na Vero shemeji yake kuhusu jinsi Mtu I na Mtu II walivyokuwa wakisengenya familia yao. Mazungumzo haya yanazua mgogoro mkubwa hali ambayo inapelekea Lila kuyakatiza kwa kuibadilisha mada hiyo na kuingiza mada nyingine:

109. Vero: Lila! Naomba tuheshimiane wifi. We' wajua mwenzio
nimeibiwa ng'ombe kisha waja niumbua kwa
kusema napakwa mafuta kwa mgongo wa chupa?
Lila: Ndiyo, unahadaiwa kwa rangi hali utamu wa chai
ni sukari [kimyaIla tuachane na hayo. Matari

wamempeleka wapi wale askari…mamaamenitimua
nyumbani eti niende nikahakikishe hawamdhuru
mwanawe…uk.42

Katika dondoo 109, Lila anauhifadhi uso hasi wa Vero kwa kuipuuza mada inayowagombanisha na kuingiza mada mbili kwa wakati mmoja na kutaka Vero kuzichangia. Lila anasema; *Ila tuachane na hayo* na kisha kuingiza mada kumhusu Matari kwa kusema*; Matari wamempeleka wapi wale askari.* Lila anasitisha mada ya kwanza kuhusu kusengenywa kwa Vero kwa makusudi baada ya kugundua kuwa Vero hafurahishwi nayo na kuingiza swali kuhusu alikopelekwa Matari ili Vero achangie. Kwa kumuliza Vero swali kuhusu Matari na kumdokezea tendo la Mama la kumfukuza nyumbani anakuwa amesuluhisha mgogoro wake na Vero.

**2.4 Matumizi ya Mkakati Ndani ya Rekodi**

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987: 68)) mkakati ndani ya rekodi haulengi kuhifadhi uso wa msikilizaji bali hudhamiria kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji kwa njia iliyotoshelevu kabisa. Kwa msingi huu, msisitizo mkuu wa mzungumzaji huwa katika kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji kuliko kuhifadhi uso wake. Wakati mzungumzaji anatumia mkakati huu huwa anahakikisha kuwa ujumbe wake ni sahili, wa moja kwa moja na hauna utata wowote.

Mkakati wa upole ndani ya rekodi huingiliana kwa mapana na kanuni za ushirikiano katika mazungumzo kama ambavyo zilielezwa na Grice (1975). Grice alisisitiza kuwa jukumu kuu la mzungumzaji katika mawasiliano ni kuwasilisha ujumbe wake kwa msikilizaji kwa namna iliyowazi kabisa na kwa kusema kile ambacho ni muhimu na chenye mchango katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* mkakati ndani ya rekodi unajidhihirisha katika matumizi ya lugha ya wahusika wakuu japo si kwa mapana.Mkakati huu unabainika ifuatavyo:

Kwanza, Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi anapomwamrisha Fiona kuwauzia buzaa walevi wote katika baa ya Fiona kwa njia ya moja kwa moja kwa kusema hivi:

110. Matari: Fiona hebu wapee buzaa wote hawa nitalipa
mimi….wanywe…yote juu yangu. uk.10

Katika mfano 110, Matari anatumia kauli; *Fiona hebu wapee buzaa wote hawa…* Katika kauli hii, Matari anaonekana kumlazimisha Fiona kuwahudumia walevi kwa buzaa.Hata hivyo, Fiona hachukulii kitendo cha Matari kama cha kutishia uso kwa vile kitendo hiki kinaishia kumfaidi yeye. Maneno ya Matari kuwa; *nitalipa mimi* pamoja na kauli…*yote juu yangu*, yanamthibitishia Fiona kuwa kitendo cha Matari kitailetea biashara yake faida.

Katika muktadha mwingine katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi anapotaka kumlaghai askari ili amruhusu kuonana na Fiona ambaye amekuja kumuona pale kizuizini. Mazungumzo ya Askari I na Matari yanajitokeza kama ifuatavyo:

111. Matari: Afande nataka kwenda kujisaidia.
Askari I: Tumia ndoo.
Matari: Ndoo imejaa.
Askari I: Nani alikuambieni muijaze ndoo haraka?... uk.51

Katika mfano 111, Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi kwa kusema; *nataka kwenda kujisaidia.* Kwa kusema hivi, Matari anachukulia kuwa yuko katika hali ya dharura ambayo inafaa kushughulikiwa kwa haraka hivyo hana haja ya kuonyesha lugha ya upole.

Katika onyesho la nane, Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi anapomkabili Fiona na kumtaka atoe pesa zake alizokuwa ameziacha kwake kabla ya kupelekwa kizuizini. Matari anamwamrisha Fiona kwa njia ya moja kwa moja kwa kumwambia.

112. Matari: [Kwa sauti kubwa] Toa fedha zangu.Toa.
Huwezi kuzibania hela zangu nilizopata
kwa jasho langu mwenyewe. Toa fedha zangu..
Fiona: Wacha kunibaka. Niue tu basi.Niue. Nisaidieni. Jamani nina…
Matari: Toa! Zitoe! Mmm! uk.74

Katika mazungumzo yaliyopo hapo juu, Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi anapotoa amri kwa Fiona, mkakati huu unatambulishwa na matumizi ya kauli; *Toa fedha zangu.Toa.* Matari anayarudiarudia maneno haya kudhihirisha hasira yake kwa Fiona. Matumizi ya mkakati huu pia yanachochewa na dharura ya kutaka kupatiwa pesa zake na Fiona. Aidha, katika muktadha huu, Matari haongozwi na na haja ya kuzingatia upole kwa sababu anatenda kitendo cha uhalifu ambacho ni kumbaka Fiona.

Katika mazungumzo baina ya Lila na Matari katika baa ya Fiona, Lila anatumia mkakati ndani ya rekodi anapomwitisha Matari pesa zake. Lila anamwambia Matari kauli hii:

113. Lila: Mwizi wee! Hebu nipe pesa zangu…Nipe pesa zangu au ukione kilichomfanya sangara kuchomwa moto. uk.15.

Lila anautumia mkakati katika mfano113 ili kutoa tahadhari kwa Matari.Vilevile, kutokana na dharura iliyopo ya kumzuia Matari kuzitumia pesa zake inamlazimu Lila kumwamrisha Matari. Mkakati ndani ya rekodi katika kauli ya Lila unatambulishwa pia na matumizi ya kauli; *Hebu nipe pesa zangu, Nipe pesa zangu*

Kadhalika, katika muktadha mwingine kwenye tamthilia ya *Mbaya Wetu*, Lila anamwamrisha Mjakazi kwenda jikoni kumletea mamake chakula kwa namna ambayo inadhihirisha matumizi ya mkakati wa upole ndani ya rekodi. Lila anamwambia Mjakazi:

114. Lila: Nenda kamletee mama chakula. uk.59

Katika muktadha 114, matumizi ya kauli; *nenda kamletee…*yanaashiria kuwa Lila hadhamirii kuonyesha upole kwa Mjakazi kutokana na uhusiano wao wa mtu na mfanyikazi wake.

Vilevile, Lila anatumia mkakati ndani ya rekodi anapokuwa akimfahamisha mamake kuwa Matari ameshikwa na polisi na kupelekwa mahakamani kwa tuhuma za ubakaji. Lila anamfahamisha mamake habari hizi hivi:

115. Lila: Matari kashikwa na polisi na kupelekwa mahakamani mjini. uk75

Katika dondoo 115, matumizi ya mkakati wa upole ndani ya rekodi yanabainishwa na matumizi ya maneno; *Matari kashikwa na polisi na kupelekwa mahakamani mjini*. Kutokana na dharura iliyopo ya kukamatwa kwa Matari, Lila hana nafasi ya kutumia mkakati wa upole katika mazungumzo baina yake na Mama. Japo anafahamu kuwa hali ya afya ya Mama si nzuri na habari zile zinaweza zikamzidishia maradhi, Lila analazimika kuzisema kwa namna ya moja kwa moja kwa sababu ni za dharura.

Temba pia anadhihirisha matumizi ya mkakati ndani ya rekodi anapokuwa akizungumza na Lila kuhusu wizi wa ng'ombe wa Tonge, Temba anajaribu kumwondoa Matari katika kesi ile na kumlaumu mwenye bucha kwa kumwambia Lila:

116. Temba: Ati nani mwizi? Aliyepatikana na ng'ombe ndiye mwizi.
Mwenye bucha ndiye.uk28

Katika kauli 116, Temba anamtambua Jefule (mmiliki wa bucha) kama mwizi kwa njia ya moja kwa moja kwa kusema; *Mwenye bucha ndiye.* Katika kutumia mkakati huu, Mzee Temba anadhamiria kumwondolea Lila tashwishwi kuwa haiwezekani kuwa Jefule si mwizi. Aidha, Temba anakusudia kumtahadharisha Lila dhidi ya kumhusisha Matari na wizi kwa vile mwizi tayari ametambulika.

Katika sehemu ya mchezo ndani ya mchezo katika onyesho la tisa la tamthilia hii, Mama anadhihirisha matumizi ya mkakati wa upole ndani ya rekodi katika mazungumzo yake. Katika mchezo huu, Mama anachukua jukumu la hakimu na kuanza kutoa hukumu dhidi ya Matari. Mama anamwamrisha askari kuwatia ndani ya seli Fiona na Vero wanapogombana na kupigana ndani ya mahakama. Mama anatoa amri yake kwa polisi kwa kusema:

117. Mama: Niondolee hii ghasia hapa.
Wafungeni ndani ya seli wote hawa.uk79

Katika mfano 117, Mama anadhihirisha mamlaka yake dhidi ya wahusika wengine pale mahakamani kwa kusema; *Niondolee hii ghasia hapa*, kwa kusema hivi Mama hamwombi askari kuwaondoa wanaosababisha ghasia ila anaamrisha. Vilevile, Mama anatumia kitenzi chenye kuonyesha amri kwa kusema; *Wafungeni*. Matumizi haya ya lugha yanaonyesha uwezo aliopewa Mama na muktadha wa mahakamai.

Matumizi ya mkakati ndani ya rekodi pia yanajidhihirisha katika matumizi ya lugha ya Mama katika mazungumzo yake na Lila. Mama anamwamrisha Lila aende jikoni kumwandalia babake yaani Mzee Temba chakula kwa kumwambia hivi:

118. Mama:Nenda ukampikie babako chakula.uk.23

Katika muktadha 118, matumizi ya mkakati ndani ya rekodi yanabainika kupitia matumizi ya kauli; *Nenda ukampikie babako chakula.* Katika kumtuma Lila, Mama halazimiki kutumia upole kutokana na sababu kuwa tendo la Lila la kupika chakula linamfaidi babake pamoja na tofauti zao za kiumri.

## 2.5 Hitimisho

Kulingana na maelezo na mifano ambayo imetolewa katika sura hii, inajitokeza kuwa wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanadhihirisha matumizi ya mikakati yote minne ya upole katika kufanikisha mazungumzo yao na wahusika wengine. Aidha, mjadala katika sura ya pili unaonyesha kuwa, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanaongozwa na lengo la kutaka kufanikisha mazungumzo yao wanapoitumia mikakati ya upole. Kadhalika, inabainika kuwa uteuzi wa mkakati wa upole na mhusika unategemea mambo mengi kama vile; uzito wa tendo la kutishia uso na lengo la ujumbe wa mzungumzaji kwa msikilizaji.

Kadhalika, maelezo katika sura ya pili yanadhihirisha kuwa, katika kufanikisha mazungumzo kwa kutumia mkakati chanya wa upole, wahusika wakuu ambao ni Matari, Lila, Mama na Temba wanatumia mbinu mbalimbali zikiwemo:kumtambua na kumjali msikilizaji, kujitambulisha na msikilizaji, utoaji wa ahadi, kutafuta makubaliano na kuepuka kumpinga msikilizaji miongomi mwa mbinu nyinginezo.

Pia, ni wazi kuwa, kando na matumizi ya mkakati chanya kama njia ya kufanikisha mazungumzo yao, wahusika hawa wanatumia mkakati hasi wa upole. Mkakati huu unabainika katika lugha ya wahusika hawa kupitia matumizi ya mbinu kama vile: matumizi ya vitangulizi vidokezi, matumizi ya kauli ya jumla, kujidunisha na kumtukuza msikilizaji, kuepuka ulazimishaji na kuuliza maswali miongoni mwa mbinu nyingine.

Katika kutekeleza tendo la kutishia uso kwa kutumia mkakati nje ya rekodi, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanatumia mbinu mbalimbali za lugha zikiwemo matumizi ya maswali ya balagha, misemo na tamathali za lugha, matumizi ya mbinu ya kinaya, lugha ya mzunguko, utoaji wa maelezo pungufu, uhamishaji na udondoshi wa mada. Mkakati ndani ya rekodi aidha unabainika katika mazungumzo ya wahusika hawa japo si kwa mapana. Imejitokeza kuwa, matumizi ya mkakati huu na wahusika wakuu yanasababishwa na hali mbalimbali kama vile uhusiano wa wahusika na tofauti za wahusika katika jamii.

# SURA YA TATU

# MIKAKATI YA UPOLE NA UKUZAJI WA WAHUSIKA WAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *MBAYA WETU*

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti anashughulikia mchango wa mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* katika kuzikuza sifa zao.Wahusika hawa ni pamoja na: Matari, Lila, Mama na Temba. Mtafiti anachambua mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika hawa ili kubainisha jinsi sifa zao zinavyojitokeza na jinsi suala nzima la kidrama linabainika katika mazungumzo yao.

## 3.1 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kuzikuza Sifa za Matari

Sifa za Matari katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* zinabainika kupitia matumizi ya mkakati mbalimbali ya upole anapoingiliana na wahusika wengine.Kama mhusika nguli ambaye amesawiriwa kwa namna hasi, mhusika huyu anajikuta katika miktadha ambayo inamlazimu kuzingatia uhifadhi wa nyuso za wapinzani wake. Kwa msingi huu, sifa hasi za Matari zinabainika kupitia mikakati ya upole anayoitumia anapozungumza na wenzake.

Kwanza, Matari anapokabiliwa na dadake Lila kwa kumwibia pesa zake, anatumia mkakati wa upole ambao unaitambulisha sifa yake ya unafiki.

119. Matari: Kwa hakika dada mimi sijaiba chochote.
Ujue pia mimi sina uso wa chuma, nina haya ati .
Siwezi kujitia aibu ya kumwibia dadangu mwenyewe.
Lakini ukitaka kuniua, niue nifilie mbali.
Utadhani ni sifa hizo unazozitafuta, kumbe kashfa tupu,
kashfa itakayokugandia haibanduki hadi siku yako hufa.
Hebu niue dada mpendwa. Niue. Niue, Niuee!uk16

Katika mfano119, Matari anatumia mkakati chanya wa upole unaotambulishwa na matumizi ya kauli; *dadangu mwenyewe.* Katika maneno haya, Matari anajitambulisha na Lila kwa kumwita dadake na kisha kusisitiza uhusiano wao kwa kutumia kivumishi cha pekee *mwenywe.*Matari anatumia mkakati huu kama njia ya kumtuliza Lila ambaye amekasirishwa na kitendo cha Matari cha kumwibia pesa zake. Katika kutumia mkakati huu wa upole Matari anajitambulisha kama mhusika mnafiki.Katika sentensi; *Siwezi kujitia aibu ya kumwibia dadangu mwenyewe* Matari anasisitiza kuwa hajamwibia dadake chochote ilhali ni muda mfupi tu uliopita ambapo

amewaeleza walevi katika baa ya Fiona kuhusu jinsi amemwibia dadake. Kabla ya kuwasili kwa Lila, Matari anaulizwa na Mtu III alikoiba pesa naye akamjibu kuwa amemwibia dadake, dayolojia hii inaenda hivi:

120. Mtu III: Lakini Mzee twambie, leo umemkwapua nani?
Matari: Dadangu Lila. uk 14

Kwa kulinganisha maneno ya Matari katika dondoo 120 na dayolojia ya mhusika huyu katika mfano 119 sifa ya unafiki ya Matari inajibainisha. Kwa msingi huu, mkakati chanya wa upole unaotumiwa na Matari kwa dadake katika mfano 120 unakuwa njia mojawapo ya kuikuza sifa ya unafiki ya mhusika huyu ikilinganishwa na matamshi yake ya hapo awali. Katika dondoo hili, pia sifa ya wizi ya Matari inajitokeza pale anaposema; *Siwezi kujitia aibu ya kumwibia dadangu mwenyewe* kumaanisha kuwa yeye si mwizi wa pesa za dadake. Kauli kuwa *sijaiba chochote* inakinzwa na jibu analomtolea Mtu III katika mfano 120, kuwa amemkwapua dadake.

Katika muktadha mwingine, ukatili wa Matari unajitokeza kupitia matumizi yake ya mkakati wa upole ndani ya rekodi kama inavyodhihirishwa katika mwisho wa tamthilia hii. Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi anapokuwa akimwitisha Fiona pesa zake ambazo alikuwa amemwachia kabla ya kukamatwa kwa tuhuma ya kumwibia Tonge ng'ombe wa maziwa.Katika makabiliano haya Matari anasema hivi:

121. Matari: [Kwa sauti kubwa] Toa fedha zangu. Toa.
Huwezi kuzibania hela zangu nilizotoa
kwa jasho langu mwenywewe. Toa fedha zangu.
Fiona: Wacha kunibaka. Niue tubasi, Niue.Nisaidieni.Jamani nina…uk74

Katika dayolojia 121, Matari anatumia maneno yanayoashiria amri na vitisho; *Toa fedha zangu, Huwezi kuzibania hela zangu* hali inyodhihirisha ukatili wake kwa Fiona.

Katika mandhari ya baa ya Fiona Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi anapokuwa akibishana na Fiona.Katika mgogoro huu, Fiona anamtaka Matari kulipa pesa kwanza kabla ya kuhudumiwa kwa buzaa.Matari anamtahadharisha Fiona dhidi ya kumpunja pesa zake. Katika matamshi ya Matari sifa yake ya vitisho inajibainisha.

122. Matari: [Anamkonyeshea Fiona kidole] Uchunge sana ukinipunja au
kuniibia hizi pesa naweza kukufanya chochote…nitakufanya
lolote na wala hakuna lolote litakalonipata,ushafahamu?Ninaweza
nikakuibia,au nikakugeuza kizuu au hata kukubaka…uk 11

Katika mfano 122, sifa ya vitisho inatambulishwa na matumizi ya maneno kama; *Uchunge sana ukinipunja, naweza kukufanya chochote… nitakufanya lolote na wala hakuna lolote litakalonipata.* Hapa Matari anajaribu kumtahadharisha Fiona dhidi ya kutumia pesa zake vibaya hali ambayo pia inaweka wazi sifa yake ya vitisho.

Katika muktadha mwingine, sifa ya ukarimu ya Matari inabainika anapokuwa akimtaka Fiona kuwahudumia walevi kwa buzaa. Matari anasema:

123. Matari: …Wape buzaa wote walewe hadi waanguke
wake zao na wanaume zao waje wawaokote hapa.uk11

Katika mfano 123, Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi ambao unatambulishwa na matumizi ya maneno; *Wape buzaa wote walewe.* Katika kauli hii, Matari anajitolea kuwanunulia walevi wote katika baa ya Fiona buzaa kiasi ambacho wanataka.Matumizi ya mbinu ya chuku; *walewe hadi wake na wanaume zao waje wawaokote hapa* yanadhihirisha makusudio ya Matari katika kutimiza ahadi yake kwa walevi. Kando na Matari kubainishwa kama karimu, sifa yake ya ubadhirifu inajitokeza katika kauli; *wape buzaa wote walewe hadi waanguke*.Matumizi ya maneno haya ni ishara kuwa Matari yuko tayari kutumia pesa zake kuwanunulia walevi buzaa.

Sifa ya ubadhirifu pia inajitokeza katika muktadha ambapo Matari anaachiliwa kutoka seli na kuwatembelea walevi katika baa ya Fiona. Matari anatumia mkakati chanya wa upole ambao unadhihirisha ubadhirifu wake:

124. Matari: [Kwa Fiona] Fiona, basi wape waheshimiwa buzaa
kiasi chao, nitalipa mimi.uk 78

Katika mfano 124, mkakati chanya wa upole unatambulishwa na matumizi ya neno *waheshimiwa* ambalo Matari analitumia kuwatambua walevi. Kando na matumizi ya mkakati chanya wa upole, Matari anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi ambao unaibainisha sifa yake ya ubadhirifu. Matari anasema; basi *wape waheshimiwa buzaa kiasi chao; nitalipa mimi.*

### 3.2 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kuzikuza Sifa za Lila

Sifa za Lila zinabainika katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* kupitia matumizi yake ya mikakati mbalimbali ya upole anapoingiliana na wahusika wengine. Kwanza, Lila anadhihirisha hasira zake kupitia matumizi ya mkakati wa upole nje ya rekodi na mkakati wa upole ndani ya rekodi

anapomkabili Matari katika baa ya Fiona. Katika muktadha huu, Lila anamwandama Matari kwa Fiona baada ya kukosa pesa zake alizokuwa amezihifadhi kwenye pochi lake. Lila anapomkuta Matari akifurahia buzaa na walevi wenzake anatumia mkakati ndani ya rekodi na mkakati nje ya rekodi katika miktadha kadhaa na kudhihirisha hasira yake.

125. Lila: Mwizi wee! Hebu nipe pesa zangu.
Matari: Pesa gani?
Lila: Nipe pesa zangu au ukione kile kilichomfanya
sangara kuchomwa moto.
Matari: Sikuelewi Lila.
Lila: Acha kujitia hamnazo. Nitakuchanachana.
Matari: Yaani mimi mwehu kiasi gani hata nikuibie wewe
dadangu ilhali mama mgonjwa hali yake taabani?
Kwa nini uniwazia mabaya hivi Lila? Eeh?
Lila:Matari! Acha kunichezea akili…Umesubiri
nende kumwosha mamaukaingia chumbani kuifungua
pochi yangu na kuniibia. Wewe mtu kweli au nduli? uk15-16

Katika kauli 125, hasira za Lila zinabainika kwa uwazi kupitia matumizi yake ya lugha. Kwanza, Lila anadhihirisha hasira hii kwa kumwingilia Matari moja kwa moja bila kuzingatia uhifadhi wa uso wake kwa kusema *mwizi wee! Hebu nipe pesa zangu.*Hapa, mkakati ndani ya rekodi ambao unadhihirishwa na matumizi ya kitenzi *nipe* chenye kuleta dhana ya amri unatuwekea wazi hasira ya Lila.

Katika mfano 125, pia, sifa ya hasira ya Lila inazidi kubainikika kupitia matumizi yake ya mkakati nje ya rekodi ambao unatambulishwa na matumizi ya swali la balagha; *Wewe mtu kweli au nduli?* Kupitia swali hili, Lila anamlinganisha Matari na nduli ishara kuwa amekasirishwa na kitendo chake.Kauli hii pia inaweka wazi mvutano uliopo baina ya wahusika hawa wawili.Kando na hili, matumizi ya tamathali za usemi kama njia ya kusisitiza makusudi yake ni ishara kuwa Lila ni mhusika mwenye hasira. Lila anatumia tamathali anuwai za lugha kwa mfuatano zikiwemo istiari ya sagara kuchomwa moto *Nipe pesa zangu au ukione kile kilichomfanya sangara kuchomwa moto*, chuku *Nitakuchanachana* na sitiari; *Wewe mtu kweli au nduli?* hali ambayo inatuthibitishia kuwa Lila anatawaliwa na hasira.

Kupitia matumizi ya mkakati nje ya rekodi pia sifa ya utambuzi ya Lila inabainika. Lila anatumia msemo; *Acha kunichezea akili*. Kwa kutumia kauli hii, Lila anatambulishwa kama mtambuzi, kuwa ana uwezo wa kutathmini kauli za Matari na kujua ukweli wake.

Kwingineko katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, sifa ya Lila ya majuto inabainika kupitia matumizi yake ya lugha anapokuwa akimwelezea mamake sababu ya yake ya kukurupuka na kumwacha peke yake pale chumbani.Katika mazungumzo baina ya Lila na Mama, Mama analalamika kuwa Lila amekurupuka na kumwacha peke yake pale chumbani. Dayolojia ya wahusika hawa inajitokeza kama ifuatavyo:

126. Mama: Lila umeshindwa kunitunza?
Lila: Sivyo mama, samahani sanaa…
Mama: Kama unataka nife basi niue.
Lila: Samahani mama. Nimefanya kukurupuka
hapa tu ghafla.sio kupenda kwangu.
Mama: Nimeuliza umekurupuka kwa nini?
Mbona yule msichanaanayenituza hajawahi
kukurupuka akaniacha peke yangu?Mbona?
Lila: Samahani mama. Naomba uniwie radhi. uk18-19

Katika mazungumzo kwenye dayolojia 126, Lila anatumia mkakati hasi wa upole ambao unabainisha upole, majuto na msamaha wake kwa mamake.Kupitia matumizi ya maneno; *samahani sanaa…, samahani mama. Naomba uniwie radhi*, *sio kupenda kwangu*, msamaha wa Lila kwa mamake na hali ya majuto anayoipitia kutokana na kitendo chake cha kukurupuka inabainika.

Sifa za Lila za unyenyekevu na upole pia zinajibainisha katika mazungumzo yake na babake yaani Temba wakati Lila anapomfahamisha Temba sababu yake ya kutoenda kwa mwalimu. Katika dayolojia hii, Lila anajitokeza kama mpole, mwenye heshima tena mwenye kujutia makosa yake.

127. Temba: Je, Lila amempata mwalimu yule asiyelipa kodi?
Lila: [anasitasita] Sijampata.
Temba: Eeh? Pamoja na kurauka kote huko ulikorauka?
Lila: Sijafika huko.
Temba: [kwa hamaki] Watoto nyie mtanipandisha
kichaa. Kwa nini hukufika?
Lila: Baba! Samahani sana lakini nimepata mengine njiani. uk25

Katika mfano 127, lugha ya Lila inadhihirisha upole na unyenyekevu kwa babake yaani Temba. Katika kuelezea sababu yake ya kukosa kwenda kwa mwalimu, Lila anadhihirisha msamaha wake kwa kusitasita kulijibu swali la babake na kisha kutoa sababu yake. Licha ya Temba kumkorofisha kwa hamaki, Lila anajibainisha kama mwanamke mpole kwa kutumia mkakati chanya wa upole. Mkakati huu unatambulishwa na matumizi ya neno *baba* kama njia ya kuonyesha uhusiano ama utambulisho wa familia Pia Lila anatumia mkakati hasi wa upole ambao unatambulishwa na kitangulizi *samahani sana* na kipashio cha kukinza *lakini nimepata mengine*. Kwa kutumia mikakati hii miwili Lila anadhihirisha heshima yake kwa babake kama mtoto. Vilevile, Lila anadhihirisha msamaha wake kwa babake kwa kukosa kutimiza jukumu lake kama alivyokuwa ameagizwa kufanya.

Vilevile, matumizi ya makakati wa upole nje ya rekodi kama unavyobainishwa na matumizi ya lugha yenye utata na maelezo pungufu yanaibainisha sifa ya ujanja ya Lila. Lila anasema; *nimepata mengine njiani*. Kipashio hiki cha kisarufi kinatumika na mhusika huyu kikiwa na dhima ya kuijenga taharuki ambayo inamchoche Temba kuzidi kumdadisi Lila kuhusu mambo mengine anayozungumzia. Aidha, kupitia usemaji kwa mapungufu, *Sijampata* na kisha kuongezea*, Sijafika huko* badala ya kutoa sababu yake Lila anafanikiwa kuibadilisha mada kuhusu sababu yake ya kutokwenda kwa mwalimu kudai babake kodi na kumjengea babake taharuki kwa kuibua mada kuhusu wizi wa ng'ombe wa Tonge.

Zaidi ya haya, sifa ya utambuzi ya Lila inabainika kupitia matumzi yake ya mkakati hasi upole kama ambavyo dayolojia ifuatayo baina ya Lila na Temba inadhihirisha:

128. Lila: Sidhani hivyo baba mwenye bucha hayupo peke yake
Temba [Anamtazama kwa tuhuma] Usiwe unaanza
kumtuhumu mdogo wako kwa wizi.
Lila: Baba?
Temba: Naona macho yako yanaonyesha yanaelekeza
tuhuma kwa ndugu yako Matari.
Lila: Naona umetia maneno kinywani mwangu.uk28

Katika mfano 128, Lila anatumia mkakati hasi wa upole ambao unatambulishwa na matumizi ya kauli; *sidhani hivyo baba.* Katika kauli hii, Lila anakwepa kudhihirisha msimamo wake kuhusu kuhusika au kutohusika kwa Matari katika wizi wa ng'ombe. Badala yake, anaonyesha uwezekano wa hali hii kimakusudi.Kando na kuuhifadhi uso hasi wa babake*,* matumizi ya

mkakati huu na Lila yanaibainisha sifa yake ya ufahamu wa mambo, kuwa Lila ana uwezo wa kutambua kuwa babake hataki Matari ahusishwe na wizi. Pia, Lila ana uwezo wa kutambua kuwa Matari anahusika na wizi wa ng'ombe.

Katika mfano 128 pia, sifa ya Lila ya utambuzi inazidi kubainika katika matumizi yake ya mkakati wa upole nje ya rekodi ambao unabainishwa na maelezo pungufu katika kauli; *mwenye bucha hayupo peke yake*. Kwa mujibu wa kauli hii, Lila anaulinda uso hasi wa babake kwa kutomwambia ukweli kuhusu kuhusika kwa Matari katika wizi. Vilevile, uwezo wa Lila wa kuelewa na kutambua ukweli wa mambo unabainika kupitia mkakati huu.Sifa hii pia inamtofautisha Lila na babake.

### 3.3 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kuzikuza Sifa zaTemba

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, Temba amesawiriwa kama mhusika hasi ambaye anashindwa kudhibiti tabia za mwanawe Matari hali ambayo inampelekea Matari kuwa tisho kubwa kwa usalama wa jamii ya tamthiliani. Katika matumizi yake ya lugha, Temba anadhihirisha matumzi ya mikakati mbalimbali ya upole. Kupitia mikakati hii ya upole, sifa mbalimbali za mhusika huyu zinabainika.

Kwanza, Temba anajitokeza kama mwenye kudekeza. Katika matumizi yake ya lugha hasa katika muktadha ambapo anazungumzia vitendo vya mwanawe Matari, Temba anaishia kumtetea kwa kila analolifanya liwe zuri au baya. Ufuatao ni mfano unaodhihirisha sifa ya udekezaji :

129. Temba: Aah! Ni makosa makubwa kumshuku nduguyo kwa mambo kama haya…Upendo wa kidugu ulikwenda wapi siku hizi? Wewe huwezi kujitole mhanga nafsi yako kwa ajilia ya nduguyo? Unamshuku kwa nini? Hebu niitie huyo Matari. uk.28

Katika mfano 129, Temba anamkosoa Lila ambaye anamshuku Matari kwa mwizi wa ng'ombe. Katika dayolojia hii, Lila anashikilia kuwa lazima Matari amehusika katika kisa hiki huku babake akimlaumu kwa kufanya madai haya kwa nduguye. Kwa msingi huu, Temba anatamka maneno haya huku akiyaelekeza kwa Lila kama njia ya kumbadilisha mawazo ili kumtetea Matari badala ya kumlaumu.

Temba anatumia mkakati hasi wa upole unaobainishwa katika dondoo hili na matumizi ya kauli ya jumla *Aah! Ni makosa makubwa kumshuku nduguyo kwa mambo kama haya…Upendo wa kidugu ulikwenda wapi siku hizi?* Katika sentensi hii msimamo wa Temba kuhusu vitendo hasi vya mwanawe unadhihirika.Temba anamchukulia Lila kama msaliti mkubwa wa familia yao kwa vile hamuungi mkono Matari. Kwa Temba maoni ya Lila ni dalili ya kupungua kwa mapenzi yake kwa kakake Matari. Kupitia dondoo hili hivyo Temba anajitokeza kama mzazi mwenye kudekeza hali ambayo imechangia katika kudorora kwa tabia ya mwanawe.

Katika muktadha mwingine, sifa ya Temba ya ukali inajidhihirisha anapokuwa akimzomea Lila ambaye analalamika kwa kutumwa na babake kumdai kodi ya nyumba kwa mwalimu asiyelipa deni ilhali yeye ni mtu mzima anayejitegemea.Temba anamjibu Lila kwa maneno ambayo yanadhihirisha ukali mwingi.

130. Temba: Lila? Usiniletee ufedhuli hapa.
Lila: Baba mbona siku zote nijapo kukutembeleeni hapa
wanituma kwenda kwa wapangaji wako wasiolipa?...
Temba: [Kwa kufoka zaidi] Nimesema usiniletee ufedhuli hapa.
Fanya kama nilivyokwambia au nyumba yangu uione paa.
Ushasikia? Peleka ufedhuli wako huko mjini
au uolewe umpelekee mumeo. uk 24.

Katika kauli hii, Temba anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi kudhihirisha hasira yake kwa Lila. Mkakati huu unabainishwa na matumizi ya maneno kama; *Usiniletee ufedhuli hapa* na matumizi ya kauli; *fanya kama nilivyokwambia*. Katika kutumia mkakati huu, Temba anatumia maneno ambayo yanauweka wazi ukali wake. Aidha, sifa ya ukali inazidi kubainika katika mkakati wa upole ndani ya rekodi anaposema; *Peleka ufedhuli wako huko mjini au uolewe umpelekee mumeo*. Kwa kutumia maneno haya, Temba anadhihirisha hasira yake ambayo inatokana na kukosolewa na mwanawe Lila.

### 3.4 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kuzikuza Sifa za Mama

Kando na kufanikisha mazungumzo baina ya Mama na wahusika wengine, mikakati ya upole kama inavyobainika katika lugha ya Mama inachangia katika kuzibainisha sifa zake.

Kwanza, Mama anatumia mkakati hasi wa upole kumkosoa Lila ambaye amekurupuka na kumwacha peke yake. Dayolojia baina ya Mama na Lila inajitokeza kama ifuatavyo:

131. Mama: Lila! Ee? Umechoka kunitunza?
Lila: Sivyo mama, samahani sana…
Mama: Kama unataka nife basi niue,
Lila: Samahani mama. Nimefanya kukurupuka
hapa ghafla. Sio kupenda kwangu.uk18

Katika mfano 131, Mama anadhihirisha hasira yake kwa Lila kwa njia ya kutumia upole hasi. Kwanza, Mama anatumia mkakati hasi wa upole kwa kumdhihaki Lila. Dhihaka hii inabainika katika kauli ya Mama anapomwambia Lila; *Kama unataka nife basi niue,* Kwa kusema hivi, Mama anaionyesha hasira yake lakini kwa namna ambayo inadhihirisha uhifadhi wa uso hasi wa Lila. Kinachojitokeza hapa ni kuwa, Mama anachukulia kuwa Lila hataki kumshughulikia ndio maana anakurupukakurupuka na kumwacha peke yake.

Pili, Mama anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi kudhihirisha hasira yake kupitia matumizi ya swali la balagha; *Umechoka kunitunza?* Katika muktadha huu*,* Mama anamwuliza Lila swali ambalo tayari anajua jibu lake. Madhumuni ya Mama ya kuuliza swali hili sio kuwa anataka Lila alijibu ila ni njia ya kumkosoa kwa namna ambayo pia inadhihirisha uhifadhi wa uso hasi wa Lila.

Kwingineko katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, sifa za hofu, machungu, na ukataji tamaa zinabainika katika lugha ya Mama anapotoa kauli yake kuhusu tabia ya mwanawe Matari. Mama anasema na Matari kwa lugha inayodhihirisha sifa hizi kama inavyobainika katika mfano huu:

132. Mama: Matari! Afadhali nife niondokane na fedheha hii…
Mwanangu Matari…Hauchi Hauchi kwa nini? Utaiba
mpaka lini? Unaiba kwa nini? Nini usichokuwa nacho?
Kwa nini kutuaibisha kila uchao mwanangu? uk20

Katika mfano 132, Mama anatumia mchanganyiko wa mikakati mbalimbali ya upole katika kudhihirisha athari za tabia ya wizi wa Matari katika maisha yake na familia ya Mzee Temba kwa jumla.Mama anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi anaposema; *Afadhali nife niondokane na fedheha hii*…Mkakati huu unatambulishwa na kuwepo kwa urejeleaji wa tabia ya wizi ya Matari kama fedheha na wakati uo huo kujihusisha nayo kwa kusema afadhali afe ili aondokane nayo. Hapa Mama analenga kusisitiza uzito wa athari za tabia ya Matari katika maisha yake. Katika matumizi ya lugha kwenye mkakati huu, sifa ya kuwa na machungu na fedheha ya Mama inawekwa wazi.

Vilevile, Mama anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi unaobainishwa na matumizi ya maswali ya balagha kudhihirisha hali yake ya kukata tamaa. Maswali haya ambayo ni pamoja na; *Unaiba kwa nini, Nini usichokuwa nacho?* na *Utaiba mpaka lini?* yanatuwekea wazi ukweli kuwa Mama ni mhusika aliyekata tamaa kutokana na tabia ya mwanawe. Aidha, matumizi ya maswali haya tena kwa mfuatano ni dhihirisho kuwa Mama amekata tamaa katika kumrekebisha Matari tabia.

Isitoshe, majuto ya Mama kutokana na kumdekeza mwanawe yanabainika katika lugha yake hasa kupitia matumizi ya makakti wa upole nje ya rekodi ambao unadhihirika kupitia matumizi ya maelezo pungufu; *Hauchi Hauchi kwa nini?* Katika kauli hii, Mama anahifadhi uso hasi wa Matari kwa kutorejelea tabia yake ya wizi kwa namna ya moja kwa moja. Kwa kusema *hauchi,* Mama anajizuia kukitaja ambacho Matari haachi kufanya kimakusudi.

Sifa ya Mama ya kudekeza pia inabainika katika tamthilia hii anapomwuliza Lila maswali ambayo yanatuthibitishia msimamo wake kuhusu kuhusika kwa Matari katika wizi. Kwenye dayolojia yake na Lila, Mama anasema hivi:

133. Mama: Hapana! Haiwezekani!
Mwanangu kuiba na kubaka? Do...La!
Lila: Ukitaka usitake, ukiamini usiamini, mambo ni kama vile.
Mama: Mbona wanakijiji hawakumlinda asikamatwe na polisi? uk76.

Katika dayolojia 133, Mama anatumia mkakati nje ya rekodi kupitia matumizi ya mbinu ya kuwa bila rajua yaani, kutotarajia mazuri. Mama anakana kuhusika kwa Matari katika wizi kwa kusema; *Hapana! Haiwezekani! Mwanangu kuiba na kubaka?* Katika kauli hii, Mama anamtetea mwanawe kuwa haiwezekani akaiba au kubaka hata bila kuchunguza iwapo ameiba au la.

Aidha, Mama anatumia mkakati hasi wa upole kwa Lila kwa kumwuliza; *Mbona wanakijiji hawakumlinda asikamatwe na polisi?* Mama anaelewa kuwa wananchi hawakuwa na uwezo wa kuwazuia polisi kumkamata Matari. Hata hivyo, anachukulia kuwa mtazamo wa wananchi kumhusu Matari ni kama wa hapo awali. Aidha, Mama anamwuliza Lila swali hili japo hana uwezo wa kulijibu ishara kuwa amekata tamaa.

Kando na haya, sifa ya Mama kama mshauri inajitokeza kupitia matumizi yake ya lugha. Kwenye matamshi yake ambayo yanalenga kumshauri Lila kufikiria suala la ndoa, Mama anadhihirisha nafasi yake katika malezi kama inavyodhihirishwa katika kauli hii.

> 134. Mama: Unalia nini? Walia kwa sababu nimesema juu ya ndoa? Una moyo wa bua nini mtoto wewe? Hutaki kuambiwa mambo ya ndoa? Ndoa ni kitu cha lazima kwa mwanadamu mwanangu. kuikataa ni kushindana na maumbile. Ajabu ya shingo kukataa kulala chini. uk33

Katika mfano 134, Mama anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi kumkosoa Lila.Mama anauliza; *Una moyo wa bua nini mtoto wewe? Hutaki kuambiwa mambo ya ndoa?* Katika kauli hii, Mama anamwambia Lila kuwa ana moyo wa bua kumaanisha kuwa ana moyo dhaifu ndio maana analia ovyoovyo. Kupitia matumizi ya msemo huu, sifa ya Mama kama mshauri bora inabainika.

Aidha, kama mzazi, Mama anawajibika kumshauri mwanawe kuhusu haja ya kuolewa ili kuendeleza kizazi, Mama ana haki ya kufanya hivi kwa vile Lila amefikisha umri wa miaka arobaini na bado hajaolewa. Hata hivyo, Mama analazimika kutumia mkakati wa upole nje ya rekodi ambao unatambulishwa na matumizi ya methali; *Ajabu ya shingo kukataa kulala chini*. Katika kauli hii Mama anamshauri Lila kuhusu umuhimu wa ndoa kwa njia ya kumlaumu kwa kukataa kufanya kitu ambacho ni cha lazima.Kwa kutumia methali hii, Mama anadhihirisha upole hasi kwa vile hamwambii moja kwa moja kuwa anaikataa ndoa.

Katika muktadha mwingine tamthiliani, Mama anabainika kama mwenye huruma kupitia matumizi ya mkakati hasi wa upole anapokuwa akizungumza na Lila:

> 135. Mama: Ati hujamwona! Si nilikwambia uende uwaambie wasimpige, wasimwue? [Anaanza kulia] Mwanangu Matari... Mwanangu … Maskini atajifia bado mtoto mdogo. Nilifikiri atanizika mimi muwele kumbe mimi ndiye nitakayemzika mwanangu asiye na hatia. uk.58

Katika mfano 135, Mama anadhihirisha huruma kwa mwanawe kupitia matumzi ya mkakati hasi wa upole; *Maskini atajifia bado mtoto mdogo.* Kwa kuisema kauli hii, sifa ya kuwa na ya Mama inabainika. Aidha, Mama anatumia mkakati hasi wa upole ambao unaibainisha sifa yake ya unafiki*; mwanangu asiye na hatia*. Kwa kutamka kauli hii, Mama anamtetea Matari kwa kudai

hana makosa japo anaelewa kuwa amekuwa akiikosoa tabia yake ya wizi kama ambavyo inathibitika kupitia kauli katika mfano 131; *Utaiba mpaka lini? Unaiba kwa nini?*

### 3.5 Hitimisho

Sura hii inajikita katika kuzijadili sifa za wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* kama zinavyobainika katika mikakati mbalimbali ya upole wanayoitumia katika maingiliano yao na wahusika wengine. Katika kufanya hili, wahusika wote wanne ambao ni pamoja na Matari, Lila, Temba na Mama wanaangaziwa huku sifa zao zikielezwa kama zinavyojitokeza katika matumzi yao ya lugha.Aidha, inajitokeza kuwa maingiliano ya wahusika hawa yanatawaliwa na migogoro mbalimbali ambayo inawafanya kutumia mikakati ya upole ili kuisuluhisha na kuendeleza mazungumzo yao.

# SURA YA NNE

# HALI ZINAZOYAATHIRI MATUMIZI YA MIKAKATI YA UPOLE YA WAHUSIKA WAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *MBAYA WETU*

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti anashughulikia jinsi hali mbalimbali za kijami zinavyoyathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.*Katika kushughulikia suala hili, mtafiti anaonyesha jinsi hali za kijamii kama vile, uhusiano wa mamlaka, uhusiano wa jamii na hali na malengo ya wahusika zinavyoyaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika hawa wanapozungumza. Kando na hili, sehemu hii inashughulikia mchango wa hali hizi katika kufanikisha drama kwa kuibua migogoro mbalimbali kuiendeleza na kuisuluhisha.

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987:73) mzungumzaji anapotekeleza kitendo cha kutishia uso huwa anaongozwa na seti ya kanuni ambazo hubainishwa na uzito wa kitendo cha kutishia uso kinachohusika. Brown na Levinson walieleza kuwa, kuna hali tatu muhimu za kijamii ambazo humwaongoza mzungumzaji katika kuteua mkakati wa upole atakaotumia kuwasilisha ujumbe wake kwa msikilizaji. Hali hizi ni pamoja na, uhusiano katika mamlaka baina yake na msikilizaji, uhusiano katika jamii baina ya mzungumzaji na msikilizaji na hali ya tendo la kutishia uso inayohusika. Madai ya Brown na Levinson pia yanatiliwa nguvu na Kasper (1990) anayedai kuwa kuna mwingiliano mkubwa baina ya matumizi ya mikakati ya upole na masiala ya kijamii kama vile; jinsia, umri, hali za kiuchumi na hadhi au matabaka ya wazungumzaji katika jamii husika.

Yule (1996:59), pia anayatilia nguvu mawazo ya Brown na Levinson kwa kusema kuwa, mtagusano wa kiisimu kwa kawaida huwa ni aina ya mtagusano wa kijamii.Yule anaendelea kudokeza kuwa, ili kuelewa kile kinachosemwa katika mtagusano fulani, lazima masuala ya nje na ndani ambayo yanatawala mahusiano husika yatiliwe maanani. Kulingana na Yule, masuala ya nje huhusisha hadhi mbalimbali zinazoshikiliwa na wanajamii kulingana na mamlaka au umri wa mwanajamii. Kwa upande mwingine, masuala ya ndani huhusisha maingiliano ya kijamii yanayohusisha mtu binafsi kama vile uhusiano wake na wengine.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* mahusiano na maingiliano baina ya wahusika wakuu na wahusika wengine yanadhibitiwa na hali mbalimbali za jamii. Aidha, hali hizi zina mchango mkubwa katika kudhibiti lugha yao. Mahusiano ya wahusika wakuu yanaweza yakaangaliwa katika misingi mbalimbali. Kwanza, kuna mamlaka ambayo yanatokana na nguvu za kutawala walizo nazo wahusika. Pili, kuna mahusiano ya wahusika wakuu katika jamii na mwisho ni malengo ya wahusika hawa wanapojihusisha katika mazungumzo na wahusika wengine. Kando na kuathiri mahusiano katikajamii, hali hizi pia zina jukumu muhimu katika tamthilia hii katika kuikamilisha kazi nzima kidrama

### 4.1 Mamlaka ya Mhusika Katika Jamii

Kulinagana na Brown na levinson (1987:74) mahusiano katika mamlaka baina ya wazungumzaji ni mojawapo ya masuala ambayo hubainisha aina ya mkakati wa upole utakaotumika katika muktadha fulani wa mazungumzo. Kulingana na wataalam hawa, nguvu au mamlaka ya mhusika katika jamii humaaniisha kuwa mmoja wa wahusika katika mchakato wa mazungumzo huwa ana mamlaka au uwezo fulani ulioidhinishwa katika jamii dhidi ya mwingine. Hii ina maana kuwa, mshirika wa mazungumzo huwa na uwezo wa kumdhibiti mwenzake katika jamii wanapoingiliana. Suala la mamlaka linaweza likajidhihirisha katika masuala kama vile: hadhi aliyo nayo mhusika katika jamii, jinsia ya mhusika, hali ya kiuchumi (utajiri), tabaka la mhusika au nguvu za kimwili.Matumizi ya mikakati ya upole na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* yanadhibitiwa pakubwa na mamlaka au cheo cha mhusika katika jamii.

#### 4.1.1Matumizi ya Lugha na Mamlaka ya Mhusika Katika Familia

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* Temba amesawiriwa kama mhusika mkuu ambaye ni kiongozi na msemaji wa familia yake. Kwa msingi huu, Temba amepewa mamlaka katika asasi ya ndoa. Mamlaka na cheo cha mhusika huyu yanachangia pakubwa katika kubainisha mikakati ya upole anayoitumia katika tamthilia nzima.

Kwanza, Mzee Temba anatumia mkakati ndani ya rekodi anapomwamrisha Lila. Katika muktadha huu, Lila analalamika kwa babake kuwa amekuwa akimtumia kama mkusanya kodi wake bila kuzingatia kuwa yeye ni mtu mzima anayejitegemea. Temba anamjibu Lila kwa kutumia mkakati ndani ya rekodi ili kudhihirisha mamlaka yake katika familia hii.

136. Lila: Nitakuwa mkusanya kodi wako mpaka lini? Huoni sasa mimi ni mtu mzima najitegemea na nina ajira ya uhazilimjini, tena ajira ya heshima?
Temba: Lila? Usiniltee ufedhuli hapa…[kwa kufoka zaidi] Nimesema usiniletee ufedhuli hapa. Fanya kama nilivyokwambia au nyumba yangu uione paa.Ushasikia?Peleka ufedhuli wako huko mjini au uolewe umpelekee mumeo.uk 24

Katika mfano 136, Temba anadhihirisha nguvu, mamlaka na cheo chake kama kiongozi wa familia yake kwa kutumia mkakati ndani ya rekodi katika kumkabili Lila ambaye anaonekana kumpinga. Temba anatumia kipashio cha kiisimu *fanya kama nilivyokwambia au nyumba yangu uione paa* kudhihirisha mamlaka yake. Kitenzi *fany*a kinadhihirisha dhana ya amri kuwa Lila hana nafasi ya kukataa amri ya babake au kutoa rai nyingine kuhusu maoni yake. Aidha, mamlaka ya Temba katika mfano huu yanampatia uwezo wa kutumia lugha ya vitisho dhidi ya mtoto wake na kumlazimisha kutii amri yake. Temba anaonyesha nguvu zake kupitia lugha ya vitisho inayojibainisha katika matumizi ya mkakati nje ya rekodi unaotambulishwa na nahau *nyumba yangu uione paa*. Hapa Temba anajitokeza kama aliye na mamlaka ya kusema na kutenda.

Katika muktadha 135, Temba anajitokeza kama anayetumia lugha ya vitisho bila kuzingatia suala la uso kwa vile anazungumza na mtoto wake.Kwa upande mwingine, Lila anaonekana kunywea na kutomjibu babake baada ya matamshi haya dhihirisho kuwa utengano wa mamlaka baina yake na babake haumruhusu kumjibiza babake.Hapa tofauti katika mamlaka zinadhibiti matumizi ya lugha ya wahuska hawa wawili.

Katika muktadha mwingine tamthiliani, mamlaka ya Temba katika familia yanabainika katika matumizi yake ya lugha anapokuwa akiipinga kauli ya Mama kuhusu kuchinjwa kwa mbuzi.Temba anatumia mkakati ndani ya rekodi kwa mkewe kwa kusema:

137. Temba: Hachinjwi mbuzi hapa
Mama: Anachinjwa.
Temba: Hachinjwi.
Mama: Anachinjwa.
Temba: Hachinjwi.
Mama: Naona mwataka kunifisha bure nyie .uk65

Katika mfano 137, Temba anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi kudhihirisha mamlaka yake kwa mkewe kwa kutumia kitenzi *hachinjwi* mara kadhaa. Licha ya mkewe kujaribu kushindana naye kuhusu kuchinjwa kwa mbuzi, juhudi zake zinaishia kutofaulu baada ya Temba kushikilia msimamo wake kuwa mbuzi hatachinjwa. Aidha, katika dondoo 136 matumizi ya mkakati wa upole ndani ya rekodi ni ishara kuwa ana mamlaka dhidi ya mkewe.

Katika mfano 137 pia, wahusika hawa wawili wanajitokeza kama wanaoshindana kuafikia malengo yao. Kila mmoja akishikilia kuafikia makusudio na matamanio yake kwa mwingine. Kwa upande wa Temba, lengo lake ni kufanikisha ujumbe wake kwa Mama kuwa mbuzi hatachinjwa. Lengo hili linatambulishwa na matumizi ya neno *hachinjwi* kwa namna ya kulirudia. Kwa upande mwingine, Mama anashindana kuafikia lengo lake la kumfahamisha Temba kuwa kuna haja ya mbuzi kuchinjwa.Katika muktadha huu pia, sifa ya Temba ya kuwa na misimamo mikali inabainika.

### 4.1.2 Matumizi ya Lugha na Mamlaka ya Mhusika Katika Sheria

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* matumizi ya mikakati ya upole pia yanadhibitiwa na nafasi ya kiutawala anayoshikilia mhusika katika asasi za kijamii. Hali hii inajitokeza katika onyesho la tisa ambalo ndilo onyesho la mwisho na linalohusishwa na mpomoko wa matukio katika tamthilia hii. Katika onyesho hili, mwandishi anadhihirisha jinsi matumizi ya lugha ya wahusika yanavyodhibitiwa na nafasi za utawala za kijamii zinazoshikiliwa na wanajamii kwa kuingiza mbinu ya kisanaa ya mchezo ndani ya mchezo. Katika mchezo huu, wahusika wanabadilisha nafasi zao na kuchukua zingine huku Mama akichukua nafasi ya hakimu naye Lila anachukua nafasi ya kiongozi wa mashtaka.Mandhari pia yanabadilika na kuwa yale ya kortini ambapo kesi ambayo Matariameshitakiwa na Fiona kwa kumbaka inasikizwa.

Katika mchezo ndani ya mchezo, Mama anatumia lugha ambayo inadhihirisha mamlaka makubwa katika sheria kama inavyodhihirishwa katika dayolojia hii:

138. Vero:Tafadhali hakimu usimfunge mwanangu huyu [ anaashiria mimba yake] awe yatima kwa kumfunga babake afilie jela.Naomba umwonee imani mwanangu, umsamehe babake.
Mama: Sikiza. Wewe si sehemu ya mchakato huu wa kisheria. Nyamaza au nikufunge jela. uk77

Katika mfano 138, suala la nguvu za mamlaka katika sheria linajitokeza katika matumizi ya lugha ya Mama pale anapotumia kauli ambayo inaonyesha amri; *Nyamaza au nikufunge jela*. Matumizi ya maneno *nyamaza* na *nikufunge jela* yanaashiria kuwa nafasi ya mhusika huyu katika tamthilia hii imebadilika, kuwa Mama hazungumzi na wahusika wengine kama mkewe Temba bali kama hakimu aliyepewa mamlaka na mahakama. Kando na hili, matumizi ya lugha ya vitisho na mhusika huyu yanaashiria kuwa mhusika huyu hajafungwa na majukumu ya familia au jinsia kama inavyojitokeza katika sehemu zingine tamthiliani. Katika mfano 137 pia, lugha ya Mama inatawaliwa na muktadha wa korti ambao unaidhibiti.

Kwa msingi huu, suala la lugha na utambulisho linajitokeza ambapo lugha inayotumiwa na Mama katika muktadha wa kortini inamtofautisha na lugha anayoitumia katika sehemu zingine anakosawiriwa kama mke wa Temba. Katika mandhari haya ya kortini pia Mama anaendelea kudhihirisha mamlaka yake katika sheria kupitia matumizi ya maneno yanayoweka wazi nguvu na mamlaka kama inavyojitokeza katika mfano huu:

139. Mama*:* Niondolee hii ghasia hapa.Wafungeni ndani ya seli wote hawa.uk76

Katika dondoo 139, Mama anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi kutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa namna mbili. Kwanza, kwa kuwaamrisha askari bila kuwaomba ama kuwataka msamaha. Mama anakwepa kwa makusudi kutumia mkakati hasi wa upole kwa askari kwa sababu ya tofauti katika mamlaka iliyopo baina yake na askari. Pili, kwa kutoa maagizo kuwa Vero na Fiona ambao wanapigana ndani ya mahakama wafungwe. Matumizi ya kauli *wafungeni ndani ya seli wote hawa* ni dhihirisho la ukweli kuwa Mama ana uwezo wa kisheria wa kuwafunga washukiwa tena wote kwa mara moja. Katika muktadha huu pia, Fiona na Vero wanajitokeza kama waliyo chini katika ngazi ya mamlaka wanapolinganishwa na Mama ambaye mamlaka yake yanadhihirishwa na vitenzi vya kuamrisha anavyotumia kama vile *wafunge wote hawa*.

Aidha, matumizi ya mbinu ya mchezo ndani ya mchezo katika tamthilia hii ambapo wahusika wanachukua nafasi na majukumu tofauti yana mchango mkubwa katika kuonyesha sifa za ziada za wahusika ambazo hazijitokezi wakati wahusika hawa wanashikilia nafasi zao za kawaida.

Kwa mfano katika mchezo huu Mama amebainika kama mwenye vitisho, msomi wa sheria na asiyekuwa na huruma.

Katika muktadha mwingine mchezoni, uhusiano wa mamlaka unaonekana kudhibiti mikakati ya upole ya mhusika Matari anapokuwa akizungumza na askari katika mandhari ya seli. Katika muktadha huu, Matari anadhihirisha matumizi ya mkakati hasi wa upole kwa mapana anapoingiliana na askari anayelinda seli. Kauli za Matari kwa Askari I zinajitokeza kama ifuatavyo katika kifungu hiki.

140. Matari: [Anatokeza kichwa kwenye dirisha la seli] Afande! Naomba umwambie baba aniletee mkate na soda, nina njaa sana.

Askari I: [Kwa Matari] alikwisha kwenda zake hayupo. Samahani sana…uk48

141. Matari: Tafadhali mwambie dadangu Lila aniletee soda na mkate.Ninakufa njaa…uk53

142. Matari: Afande unaweza kumpelekea salamu shemeji yangu umwambie aiweke siri, asiifichue.[ Askari I anajitia hamnazo. Anaendeleea kulikariri shairi lake.] uk55

Katika mifano 140, 141 na 142, lugha ya Matari inadhihirisha mabadiliko makubwa ikilinganishwa na lugha anayoitumia anapokuwa katika mandhari ya ulevini akizungumza na walevi. Kinachobainika katika matamshi haya ya Matari ni mikakati chanya na hasi ya upole hali inayodhihirisha kuwa mazingira ya selini yamemvua uwezo na nguvu zake.

Katika dayolojia baina ya Matari na Askari I, Askari I anasawiriwa kuwa na mamlaka makubwa dhidi ya Matari ambaye ni mfungwa. Kwa msingi huu, lugha ya Matari inadhibitiwa na mazingira haya kiasi kwamba inadhihirisha upole mwingi. Matumizi ya maneno kama *Naomba umwambie baba* na Matari katika mfano 140 ni dhihirisho la matumizi ya mkakati hasi wa upole kwa Askari I ambaye katika muktadha huu ana uwezo wa kisheria kwa Matari. Kwa msingi huu, Matari anabidiika kunyenyekea anapomwomba kumtuma kwa babake.Hapa matumizi ya lugha ya Matari yanadhibitiwa na muktdha na kwa kiasi kikubwa uhusiano katika mamlaka baina ya Matari na Akari I.

Aidha katika mfano 140, Matari anatumia mkakati chanya wa upole kwa Askari I kwa kujenga uhusiano mwema naye kwa kutumia kipashio cha kiisimu *afande* ambacho kinaashiria uhusiano wa karibu pamoja na heshima. Kwa kutumia neno hili Matari anatambua tofauti za cheo zilizopo baina yake na Askari I hivyo kuudumisha uso chanya wa mhusika huyu. Katika mfano huu, mwandishi anafanikiwa kuendeleza mhusika Matari kuwa na sifa ya upole na heshima kwa wakubwa wake.

Katika mfano 141, suala la uhusiano baina ya lugha na mamlaka linazidi kujitokeza ambapo Matari anakitambua cheo cha Askari I kwa kutumia mkakati hasi wa upole kwa kutumia neno *tafadhali.* Vilevile, kwa kutumia mkakati wa upole nje ya rekodi unaodhihirishwa na matumizi ya chuku katika kauli yake; *Ninakufa njaa.* Katika muktadha huu, Matari anatambua uso hasi wa Askari I kwa kumwomba na wakati uo huo kusisitiza ombi lake kwa kutumia lugha ya hisia; *Ninakufa njaa*. Matumizi ya vipashio hivi viwili yanadhihirisha jinsi mazingira ya seli yalivyomwathiri Matari na kumvua kiburi chake. Kwa kumchora Matari katika hali hii ya chini, mwandishi anafanikiwa kuonyesha jinsi mazingira yalivyo na msukumo mkubwa katika kuathiri mikakati ya upole inayotumiwa na mhusika.

Matari anatumia mkakati chanya wa upole kwa Askari I katika mfano 142 anapomtambua askari huyu kwa cheo chake tena kwa kumwita *afande*.Pia, Matari anatumia mkakati hasi wa upole kupitia matumizi ya kitangulizi *unaweza* ambacho kinatoa ulazimishaji kwa Askari I kutekeleza analoagizwa na Matari. Matari anatambua nyuso hasi na chanya za mhusika huyu kwa kutumia vipashio hivi viwili vya kiisimu kwa vile anatambua kuwa uhusiano wa mamlaka uliopo baina yake na Askari I unahitaji kutambuliwa kupitia lugha anayoitumia.

### 4.1.3 Matumizi ya Lugha na Mamlaka ya Nguvu za Mwili

Kando na mamlaka ya kisheria wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanadhihirisha uwezo na nguvu zao za kimwili kwa wahusika wengine kupitia lugha yao. Hali hii ya matumizi ya lugha inayoakisi mamlaka ya nguvu za mwili inadhihirishwa kwa uwazi katika tamthilia hii kupitia kwa Matari. Matari anamkabili Fiona kwa vitisho anapofahamishwa na Fiona kuwa anatakiwa kuweka kiasi fulani cha pesa kama *deposit* kabla ya Fiona kuanza kuwahudumia walevi kwa pombe. Matari anasema hivi:

143. Matari:[Akimnyoshea Fiona kidole] Uchunge sana ukinipunja au kuniibia hizi pesa naweza kukufanya chochote…nitakufanya lolote na wala hakuna lolote litakalonipata, ushafahamu? Naweza nikakuibia au nikakugeuza kizuu, au hata kukubaka au nikukate kichwa kitengane na kiwiliwili…Umesikia? uk 11

Katika mfano 143, Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi kumtahadharisha Fiona dhidi ya kumwibia pesa zake. Mkakati huu unatambulishwa na matumizi ya lugha iliyojaa vitisho tena inayoashiria makusudio yake katika kutekeleza anachokimaanisha. Kuwa, Matari hamfichi Fiona chochote. Kinachojitokeza katika mfano 143 ni kuwa, Matari anadhihirisha uwezo wa nguvu zake za mwili kwa Fiona kwa kutumia kauli zinazoashiria uwezo wake tena kwa namna ya kuzikariri, Matari anasema; *naweza kukufanya chochote.*

Kando na kuonyesha uwezo wake wa nguvu za mwili, kauli za Matari katika mfano 143 zinadhihirisha kuwa, Matari hana kizuizi chochote katika kumfanyia Fiona unyama wowote. Matumizi ya maswali kama vile *ushafahamu?* na *umesikia?* kama yanavyojitokeza katika dondoo hili pia ni kibainishi cha nguvu za mwili alizo nazo Matari. Kuwepo kwa matumizi ya maneno kama; *naweza kukuibia* au *nikakugeuza* kizuu au hata *kukubaka* pia ni ishara tosha kuwa lugha ya Matari inaashiria uwezo wake wa nguvu za mwili kwa Fiona katika muktadha huu.

Kando na kutufahamisha mengi kuhusu nguvu za mwili za Matari, kauli hii inatubainishia mengi kuhusu udhaifu wa mwili wa Fiona ambaye anawakilisha jinsia ya kike. Kinachojitokeza katika mfano 143 ni kuwa, Matari anatumia lugha yenye sifa za aina hii kutokana na uelewa wake wa kijamii kuhusu udhaifu wa nguvu za mwili unaohusishwa na wanawake. Hii ina maana kuwa Fiona ana uwezo finyu wa nguvu za mwili kwa Matari kutokana na ukweli kuwa yeye ni mwanamke. Kando na kuibua sifa za Fiona kauli hii inakuwa na mchango mkubwa katika kuibua sifa za ukatili, kiburi na vitisho zinazohusishwa na Matari. Matumizi ya viwakilishi nafsi tegemezi -ni- katika vitenzi, '**ni**takufanya, **ni**kakugeuza, **ni**kukate' miongoni mwa vingine ni thibitisho kuwa Matari ni katili mwenye kiburi kikubwa.

### 4.1.4 Matumizi ya Lugha na Hali ya Nguvu za Uchumi

Kando na nguvu za utawala, na nguvu za mwili wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanadhibitiwa na hali na nguvu za uchumi zinazotawala. Hii ina maana kuwa. matumizi ya

mkakati fulani wa upole na mhusika katika mazingira ya kijamii yanadhibitiwa na tofauti za uwezo wa kiuchumi baina ya mhusika huyu na washirika wenzake katika mchakato wa mazungumzo. Kwa msingi huu, wahusika wakuu ambao wamesawiriwa wakiwa katika nafasi nzuri katika uchumi wanaakisi matumizi ya lugha ambayo yanadhihirisha uwezo wao wa dhidi ya wale walio katika nafasi za chini kiuchumi. Kwa mfano, Matari kama mmoja wa wahusika hawa anadhihirisha nguvu zake za uchumi kwa wahusika wenzake anapokuwa katika baa ya Fiona.Hali hii inabainika katika mifano ifuatayo:

144. Matari: [Kwa furaha kubwa ya ghafla] Ohoo! Sasa naelewa.
Mimi Matari sifi. Kifo hakitawahi kunionja mimi.
Matari bin Temba…kifo? La hasha! …Wape buzaa
wote walewe hadi waanguke wake zao na wanaume
zao waje wawaokote. uk 11

145. Matari: Nikazichukua na kuzizoa nguo zote humo ndani.
Nimeuza pale ng'ambo ndipo nikapata hela kidogo kuja
kuwafurahisha hapa.[Kwa Fiona] Fiona , basi wape
waheshimiwa buzaa kiasi chao nitalipa mimi.uk73

Matamshi ya Matari katika mfano 144 yanathibitisha matumizi ya mkakati ndani ya rekodi ambao unabainishwa na matumizi ya kauli yake kwa Fiona kuwa*; wape buzaa wote*. Katika kauli hii, Matari hakusudii kudhihirisha upole wowote kwa sababu anaelewa kuwa tendo la kuwanunulia walevi wote pombe katika baa ya Fiona ni la faida kwa Fiona na kwa walevi wote katika baa ile. Kwa kusema hivi pia, Matari anachukua gharama ya kitendo hiki kwa kuwaepushia walevi gharama ya kulipia buzaa. Kwa msingi huu, Matari anatumia mkakati huu kwa sababu hali iliyopo inamlazimu.

Vilevile katika mfano 144, Matari anadhihirisha mamlaka yake katika uchumi kwa kutumia mkakati wa upole ndani ya rekodi kupitia matumizi teule ya maneno. Kwanza, mamlaka haya yanabainishwa na kuwepo kwa kauli *wape buzaa wote walewe*… kauli hii inaonyesha uwezo wa katika uchumi kiasi cha kuweza kuwadhibiti walevi wote katika baa ya Fiona.Aidha, Matari anatumia maneno yanayooashiria uwezo wake kiuchumi kwa kutumia mkakati wa upole ndani ya rekodi ambao unatambulishwa na matumizi ya maneno ya kujigamba kama vile: *Mimi Matari sifi, Kifo hakitawahi kunionja mimi,* matumizi ya maneno haya ni dhihirisho la kiburi cha Matari kinachotokana na uwezo wake wa kifedha kwa vile anatokana na familia tajiri. Aidha,

kupitia matumizi ya mkakati huu wa upole kwa walevi, Matari anajitokeza kama aliyetokana na familia kubwa kama anavyosisitiza kwa kutumia maneno; *Matari bin Temba* na kuwa *kifo hakiwezi kikanionja*.

Katika mfano 145, Matari anatumia mkakati chanya wa upole kwa kuzitambua nyuso chanya za wasikilizaji wake ambao ni walevi katika baa ya Fiona kwa kuwaita *waheshimiwa*. Kwa kutumia mkakati huu, Matari anadhihirisha mamlaka aliyo nayo kiuchumi kupitia matumizi ya maneno; *basi wape waheshimiwa buzaa kiasi chao nitalipa mimi*. Kwa kutumia vitenzi *wape nitalipa,* Matari anadhihirisha uwezo wake kiuchumi kuwa ana pesa za kuwanunulia walevi hawa kiasi chochote cha pombe ambacho wanahitaji. Aidha, Matari anatumia kiwakilishi nafsi huru *mimi* kusisitiza uwezo huu pamoja na kuwaonyesha walevi kuwa yuko tayari kugharamia buzaa yao.

Katika kuleta athari za kidrama, matamshi ya Matari yana mchango mkubwa katika kumtambulisha mhusika huyu kihadhi na nafasi yake katika jamii. Kupitia maneno ya Matari kwenye onyesho hili pia, uwezo wake wa kuidhibiti familia yake na wanajamii wengine unajitokeza.

**4.2 Matumizi ya Lugha Katika Kufanikisha Malengo ya Wahusika**

Haja ya kufanikisha malengo ya wahusika ni hali nyingine ambayo inaathiri matumizi ya mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.* Hii ina maana kuwa, haja ya kutaka kufanikisha malengo fulani ya mhusika inakuwa kibainishi cha mkakati wa upole atakaoutumia anapokuwa akizungumza na wenzake.Hali hii inajitokeza katika matumizi ya lugha ya wahusika hawa kama inavyobainika katika mifano ifuatayo*:*

146. Matari: Basi tulieni wanakijiii. Tulieni. Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo. Fiona hebu wapee buzaa wote hawa nitalipa mimi. Wacha wanywe walewe waleuke.Yote juu yangu. Nani anapinga? uk10.

Katika mfano 146, Matari anatumia mkakati chanya wa upole kuwazungumzia walevi katika baa ya Fiona ili kuafikia lengo lake ambalo ni kujitambulisha kwa walevi kama mtu karimu. Matari anavuta nadhari ya wasikilizaji yake kwa kutumia mkakati chanya wa upole kwa kuwatambua kama *wanakijiji* na kuwaomba kwa kuwambia*; Basi tulieni.* Kwa kutumia maneno haya Matari

anadhihirisha upole chanya kwa wasikilizaji wake hivyo kujenga uhusiano mwema kati yake na wao.

Uhusiano unaojengwa na mhusika huyu kupitia kuzitambua nyuso chanya za wasikilizaji wake pia unakuwa msingi wa walevi hawa kumtambua Matari kama rafiki yao wa karibu. Katika dondoo 146 pia, Matari anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi ambao unatambulishwa na matumizi ya methali;*leo ni leo asemaye kesho ni mwongo* kama njia ya kuwatayarisha kumsikiliza, hii pia ni njia ya mhusika huyu kuafikia lengo lake la kuuimarisha umarufu wake miongoni mwa walevi.

Kando na hili, Matari anaendelea kutekeleza lengo lake la kujipendekeza kwa walevi hawa kwa kutumia mkakati chanya wa upole ambao unadhihirishwa na matumizi ya kauli; *wape buzaa wote hawa… nitalipa mimi… yote juu yangu*. Matari anatumia mkakati huu kwa walevi ili kuwafurahisha kwa kuwaonyesha kuwa yuko tayari kugharamia buzaa watakayoinywa. Katika muktadha huu,lengo la Matari ambalo ni kuuficha uovu wake kwa kutafuta uungwaji mkono na walevi linabainika. Lengo hili linakuwa na athari kubwa kwa Matari katika kuathiri mkakati wa upole atakaoutumia katika kuwazungumzia walevi.

Vilevile, katika mfano 146, matumizi ya lugha ya Matari yanadhihirisha lengo lake kupitia matumizi ya mkakati wa upole nje ya rekodi. Mkakati huu unadhihirishwa na matumizi ya swali la balagha; *Nani anapinga?* Matari anatumia swali hili kama njia ya kutimiza lengo lake la kuthibitisha kuwa walevi wote wako nyuma yake pamoja na kudhihirisha mamlaka yake kwa walevi. Kwa msingi huu, lengo la Matari ambalo ni kutathmini mtazamo wa walevi kumhusu linadhihirika katika mikakati ya upole anayoitumia.

Katika mandhari ya seli, matumizi ya lugha ya Temba yanadhihirisha jinsi dharura ya kufanikisha malengo ya mhusika inavyoathiri matumizi yake ya mikakati ya upole.Temba anatumia mseto wa mikakati ya upole kufanikisha lengo lake ambalo ni kumshawishi Tonge kumsamehe Matari. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hii:

147. Temba: Sikiza mwanangu. Usisahau mamako anayeugua. Usije ukamwatua moyo bure kwa uamuzi wako wenye harara. uk.48

Katika mfano 147, lengo la Temba kwa mwanawe Tonge ni bayana kupitia jinsi anavyoteua maneno katika kutekeleza tendo la kutishia uso hasi na chanya wa mwanawe Tonge. Kwanza, Temba anatumia mkakati chanya wa upole ambao unabainika katika kauli hii kwa matumizi ya neno *mwanangu*. Mkakati huu unadhamiria kumleta Tonge karibu na yeye kupitia kuufurahisha uso wake chanya. Pili, Temba anatumia mkakati nje ya rekodi unaodhihirishwa na matumizi ya maneno; *usisahau mamako anayeugua.* Maneno haya yanadhamiria kuziteka hisia za mwanawe. Kando na hili, Ili kuhakikisha kuwa lengo lake linafanikwa Temba pia anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi unaobainishwa katika kauli hii na matumizi ya kauli; *uamuzi wako wenye harara*.

Katika kauli 147 pia, Temba analazimika kutumia mikakati mitatu ya upole kwa pamoja kutokana na dharura iliyopo ya kutaka kuafikia lengo lake ambalo ni kumshawishiTonge kumsamehe Matari.Uzito wa jukumu ambalo liko mbele ya Temba unamfanya kutumia mikakati hii kwa namna ya kujalizana. Temba anafahamu kuwa Tonge yuko tayari kuwasilisha kesi anayomshtaki Matari kwa wizi mahakamani. Kwa msingi huu, Temba anaamua kumshawishi Tonge kwa kumleta karibu kupitia mkakati chanya wa upole. Vilevile, anamkumbusha Tonge kuhusu maradhi ya mamake ili apatwe na hisia za huruma.Mwisho, Temba anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi kwa kulidunisha tendo la Tonge kwa kulieleza kama uamuzi wenye harara. Kwa msingi huu, uzito wa tendo la kutishia uso wa Tonge na haja ya kutaka kumshawishi Tonge zinakuwa kichocheo kikuu cha matumizi ya mikakati mseto ya upole.

Kando na haya, matumizi ya lugha ya Lila yanadhihirisha jinsi haja ya kuafikia malengo ya mhusika inavyoweza kuathiri matumizi yake ya mikakati ya upole.Hali hii inabainika Lila anapozungumza na Mama ili kumfahamisha kuhusu kushikwa kwa Matari. Dayolojia ya Lila na Mama inajitokeza kama ifuatavyo:

148. Mama: Umempata mwanangu?
Lila: Mama! Hata sijui niseme nini?
Mama: Nini?
Lila: Najua wewe ni mgonjwa lakini nitakwambia ukweli.
Mama: Nini Lila? Sema tu mwanangu.
Lila: Matari kashikwa na polisi na kupelekwa mahakamani mjini. uk75.

Katika mfano 148, Lila anatumia mikakati mbalimbali ya upole katika kutekeleza tendo la kutishia uso wa mamake. Kwanza, anatumia mkakati chanya wa upole na mkakati hasi wa upole kwa pamoja ili kuiteka makini ya mamake. Matumizi ya mkakati chanya wa upole yanabainishwa na matumizi ya kipashio cha kiisimu *mama* ambacho kinanuia kumfahamisha Mama kuwa Lila anamtambua kama mzazi wake na sehemu ya familia yao. Pili, Lila anatumia mkakati chanya wa upole na mkakati hasi wa upole ambao unadhihirishwa na matumizi ya swali *sijui nifanye nini?* Swali hili linatumiwa na Lila kwa makusudi ili kumtayarisha Mama kuupokea ujumbe mzito ambao anadhamiria kumfahamisha.

Kando na hili, Lila anatumia mkakati hasi wa upole katika mfano 148 ili kuhakikisha na kuthibitisha kuwa mamake yuko tayari kuipokea taarifa yake. Mkakati huu unatambulishwa na matumizi ya kauli; *najua wewe ni mgonjwa* ambayo inamdhihirishia Mama kuwa Lila anatambua hali yake. Kauli hii pia inamtayarisha Mama kulipokea tendo nzito la kutishia uso. Mwishowe, Lila anatumia mkakati ndani ya rekodi kumfahamisha Mama ukweli kuwa Matari ameshikwa na kupelekwa mahakamani mjini.Kinachojitokeza katika mfano 148 ni kuwa, Lila analazimika kutumia mikakati mitatu kwa pamoja kutokana na haja ya kutaka kufanikisha lengo lake.

### 4.3 Matumizi ya Lugha na Uhusiano waWahusika Katika Jamii

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987) matumizi ya mikakati ya upole na wazungumzaji katika muktadha fulani wa kijamii hubainishwa pakubwa na uhusiano wa kijamii baina ya washirika wanaohusika katika mchakato mzima wa mawasiliano. Wilamova (2005), anasisitiza madai ya Brown na Levinson katika utafiti wake uliohusisha matumizi ya mkakati hasi wa upole katika kazi za kibunilizi. Wilamova anafafanua kuwa uhusiano baina ya washirika katika mchakato mzima wa mazungumzo hutawaliwa na kudhibitiwa pakubwa na mamlaka, hadhi za wanajamii katika jamii, hali inayotawala, uhusiano wa kijamii baina ya wazungumzaji, desturi za kijamii pamoja na amali nyingine muhimu ambazo jamii huzichukulia kama msingi wa utamaduni wake. Lakoff (2005), anashikilia kuwa matumizi ya upole hutegemea hali na muktadha wa mazungumzo unaotawala.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* uhusiano wa kijamii katika kudhibiti matumizi ya lugha ya wahusika wakuu unajitokeza katika viwango mbalimbali vikiwemo vile vya familia, jinsia, hadhi kitabaka, umri miongoni mwa viwango vingine.

### 4.3.1 Matumizi ya Lugha na Uhusiano wa Wahusika Katika Familia

Tamthilia ya *Mbaya Wetu* imejengwa na kuwekewa misingi yake katika asasi ya familia. Kwa sababu hii, wahusika wakuu na matukio yanazunguka katika familia ya Mzee Temba na mkewe. Vilevile, migogoro mingi inayojitokeza ina kiini chake katika maingiliano na mtagusano wa wahusika wa familia hii. Hii ina maana kuwa, mahusiano ya wanajamii wa familia hii yanadhibitiwa pakubwa na uhusiano wao katika familia. Hii ina maana kuwa, mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia hii inadhibitiwa na uhusiano wa mzungumzaji na anayezungumza naye. Hali hii inadhihirika tamthiliani ifuatavyo:

Kwanza, uhusiano baina ya Lila na Mama una mchango mkubwa katika kudhibiti matumizi ya lugha ya Lila anapozungumza na Mama. Katika mazungumzo baina ya wahusika hawa wawili, Lila anadhihirisha matumizi ya mkakati chanya upole pamoja na mkakati hasi wa upole ili kuokoa uso chanya na hasi wa mamake. Ufuatao ni mfano unaodhihirisha hali hii:

149. Mama: Lila! Ee! Umechoka kunitunza?
Lila : Sivyo mama, samahani sana…
Mama: Kama unataka nife basi niue.
Lila: Samahani Mama. Nimefanya
kukurupuka hapa tu ghafla.
sio kupenda kwangu. uk18

Katika mfano 149, Lila anadhihirisha matumizi ya mkakati chanya wa upole na mkakati hasi wa upole kutokana na hali mbili muhimu. Kwanza, Lila anajua amemkosea Mama kwa kukurupuka na kumwacha peke yake. Pili, Lila anatawaliwa na haja ya kudumisha heshima kwa mamake kama mzazi. Kwa msingi huu, uhusiano wa mama na mtoto unakuwa kidhibiti cha matumizi ya lugha ya wahusika hawa. Kimsingi, Lila anajitahidi kuzingatia lugha ya upole inayodhihirishwa na matumizi ya kauli *samahani sana* na *samahani mama* ambazo zinadhihirisha heshima na majuto yake kwa kumtendea mamake.

Pili, uhusiano wa baina ya mume na mkewe unayadhibiti matumizi ya lugha ya Temba na mkewe. Katika mazungumzo baina ya wahusika hawa, Temba na Mama wanahusiana kwa namna ambayo inadhihirisha kiwango cha juu cha matumizi ya mikakati ya upole.Uhusiano wa Temba na mkewe unatawaliwa na mgogoro ambao chanzo chake ni tofauti za mawazo kuhusu tabia za mwanao Matari. Ifuatayo ni dayolojia ambayo inadhihirisha matumizi ya mikakati ya upole baina ya Temba na Mama ambayo pia inadhihirisha nafasi ya uhusiano wa kijamii katika kuyadhibiti matumizi ya mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika.

150. Mama: Pole kwa safari mume wangu.
Temba: Nimepoa. vipi hali yako?
Mama: Haijambo. Umevipata vipuli?
Temba: Vingine vinapatikana vingine
mpaka niviagize toka ng'ambo [Anasonya]
na yote haya kwa sababu ya huyu mwanao mjalaana.
Mama: Wetu. Mwana wetu.uk23

Katika mfano150, lugha ya Mama na Temba inatawaliwa na kudhibitiwa pakubwa na uhusiano wao katika ndoa. Kwanza, lugha ya Mama inadhihirisha matumizi ya mkakati wa upole kwa mapana anapoingilana na mumewe.Upole chanya katika lugha ya Mama unabainishwa na matumizi ya maneno yanayonuia kuufurahisha uso chanya wa Temba kama vile, *pole kwa safari mume wangu* na kisha matumizi ya maswali kama *umevipata vipuli?.* Maneno na maswali haya yanalenga kumthibitishiaTemba kuwa mkewe anayajali maslahi yake. Katika muktadha huu pia, uhusiano wa ndoa baina ya mume na mkewe unamfanya Mama kuwa makini katika matumzi yake ya lugha hivyo, matumizi ya mikakati ya upole yanadhibitiwa na uhusiano wao.

Kando na kuonyesha uhusiano wa ndoa baina ya wahusika hawa, kauli ya Mama ina jukumu la kuweka wazi sifa yake ya uwajibikaji ambayo inadhihirishwa na matumizi yake ya maneno kama vile; *pole kwa safari mume wangu* na maswali ambayo yanadhamiria kuonyesha shauku yake ya kujua hali inayomkabili mumewe. Hapa, Mama anajitokeza kama anayewajibika katika kumjulia hali mmumewe.

Katika kauli 150, Mama pia anamkosoa Temba kwa kutumia lugha ya upole wakati Temba anamhusisha Matari na mamake na kujitenga naye. Katika kumkosoa mumewe, Mama anatumia mkakati chanya wa upole kwa kumhusisiha na kumtambulisha Matari na familia ya Mzee Temba kwa kusema; *Wetu. Mwana wetu*. Mama anatumia kiwakilishi *wetu* mara mbili kama njia ya

kumkumbusha Temba kuwa Matari ni sehemu ya familia yao. Lugha ya Mama inadhihirisha matumizi ya lugha ya upole anapomkosoa Temba ithibati kuwa uhusiano wao katika ndoa una nafasi kubwa katika kuyadhibiti matumizi yao ya lugha.

### 4.3.2 Matumizi ya Lugha na Uhusiano wa Wahusika Kiumri na Kijinsia

Bell (2003), akifafanua jinsi suala la uhusiano wa kijamii linavyoyadhibiti matumizi ya lugha ya wanajamii pamoja na kuathiri mikakati yao ya upole anasema kuwa; Umri kama raslimali ya kitamaduni huathiri pakubwa matumizi ya upole ya wanajamii katika tamaduni zote ulimwenguni na husaidia kuelezea tofauti za kiisimu za matumizi ya lugha. Poulious (2003) anakubaliana na Bell kwa kudai kuwa suala la tofauti za kiumri katika jamii humaanisha kuwa mwanajamii hutarajiwa kuzingatia majukumu, haki na desturi fulani anapoingiliana na wanajamii wenzake kilugha.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* suala la jinsia na lile la umri lina athari kubwa katika kuyadhibiti matumizi ya lugha ya wahusika na mikakati ya upole kwa jumla.Hali hii inajitokeza katika miktadha mbalimbali ambapo wahusika wa jinsia zote mbili wanaingiliana. Ufuatao ni mfano wa jinsi suala la jinsia na umri linayadhibiti matumizi ya lugha ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*.

151. Temba: Ati nani mwizi? Aliyepatikana na ng'ombe
ndiye mwizi. Mwenye bucha ndiye.
Lila: Sidhani hivyo baba. Mwenye bucha hayupo peke yake.
Temba: [Anamtazama Lila kwa tuhuma] Usiwe unaanza
kumtuhumu mdogo wako kwa wizi.
Lila: Baba?
Temba: Naona macho yako yanaonyesha kuelekeza
tuhuma kwa ndugu yako Matari
Lila: Baba, unanitia maneno kinywani.
Temba: Aah! Ni makosa makubwa kumshuku nduguyo
kwa mambo kama haya…uk28

Katika mfano 151, lugha ya Lila inathibitisha matumizi mengi ya upole kwa sababu kadhaa. Kwanza, Lila anafahamu kuwa anaongea na babake ambaye amemzidi katika umri hivyo anafaa kuonyesha heshima. Pili, Lila anafahamu uzito uliopo katika kumfanya babake aamini kuwa Matari ndiye mwizi wa ng'ombe wa maziwa wa Tonge.Hapa uzito wa lengo la ujumbe wake unakuwa suala muhimu sana katika kuathiri matumizi ya lugha ya Lila.

Kwa msingi huu, katika mfano 151 Lila analazimika kutumia mkakati hasi wa upole ambao unadhihirishwa na matumizi ya ya maneno; *sidhani hivyo baba* na matumizi ya swali *baba?* Matumizi haya ya lugha ni idhibati kuwa Lila hataki kumkosoa babake kwa njia ya moja kwa moja kutokana na uhusiano wao ambao ni wa baba na mwanawe. Kando na hili, Lila anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi kumkosoa babake kwa kutumia msemo, *unanitia maneno kinywani.* Katika kauli hii, uhusiano wa familia baina ya Lila na babake pamoja tofauti zao katika umri zinakuwa na athari kubwa katika kudhibiti lugha ambayo Lila anaitumia kwa babake.

Kwa upande wa upili, Temba anatumia lugha inayodhihirisha ukali. Temba anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi ambao unatambulishwa na matumizi ya kauli ya moja kwa moja; *Aliyepatikana na ng'ombe ndiye mwizi.* Katika kauli hii, Temba anamtambua mwenye bucha kama mwizi kwa njia ya moja kwa moja ili kumtenga Matari na wizi huo.Kinachobainika katika mfano 151 ni kuwa, Temba anatumia mkakati ndani ya rekodi kwa mapana kuliko anavyofanya Lila kutokana na tofauti zao za kijinsia na kiumri.

Katika mazungumzo baina ya Lila na vero, matumizi ya lugha ya Lila kwa Vero yanadhihirisha athari kubwa ya umri na jinsia katika kudhibiti na kutawala lugha ya wahusika. Lila anakutana na Vero kujadili athari za tabia ya Matari katika familia yao. Katika mazungumzo yao, Lila anadhihirisha lugha ambayo inadhibitiwi pakubwa na haja ya kuulinda uso hasi wa Vero kutokana na uhusiano wao katika umri, jinsia na familia.

152. Vero: Uwii! [Anamtambua] Ala! Wifi kumbe ni wewe, Woyee?
Lila: Ni mimi wifi.
Vero: Mbona kunishtua hivi?
Lila: Si makusudi wifi. Na naomba safari hii tusigombane.
Vero: Ulikuwa wafanya nini pale chini ya mti?
Lila: Nimesema mbona tusiepuke kugombana mara hii? Kila siku, kila siku mimi nawe ni utesi tu?
Vero: Ahaa! Na'mbie pale chini ya mti ulikuwa ukisubiri kubaka watu?
Lila: Nikichelewa kubakwa.
Vero: We' nawe. Ulikuwa unawaogopa wale wanaume.
Lila: Sio wao, maneno yao. Naona aibu wifi. uk41

Katika, mfano 152, Lila ana uhuru wa kutumia lugha ikizingatiwa kuwa anazungumza na shemeji yake, na pia anamzidi kwa umri. (Lila ana umri wa miaka arobaini ilhali Vero ana umri

wa miaka ishirini na mitano) Kwa kuzingatia mahusiano yao na jinsi ambavyo wamekuwa wakigombana, Lila anachukua jukumu la kumtahadharisha Vero kimbele kuhusu haja yao ya kuzuia mabishano safari hii. Lila anatumia mkakati hasi wa upole ambao unatambulishwa na matumizi ya kauli; *Na naomba safari hii tusigombane* na kisha kurudia tena kauli yake kwa kusema*; Nimesema mbona tusiepuke kugombana mara hii?* Kwa kufanya hivi, Lila anajaribu kudhibiti mkondo wa mazungumzo yao ambayo yako katika hatari ya kuvunjika kutokana na tofauti zao za mawazo kuhusu tabia ya Matari vilevile tofauti zao katika umri.

Fauka ya haya, Lila anatumia mkakati wa upole nje ya rekodi kwa nia ya kumdhihaki Vero ambaye anashirikiana na watu wa nje kuisengenya familia yao kwa kutumia tamathali ya lugha kwa kumwambia Vero; *Nikichelewa kubakwa…na maneno yao*. Katika mfano huu, Lila anahuisha maneno ya Vero na wenzake kama yaliyo na uwezo wa kumbaka kwa kuisengenya familia yao. Katika muktadha huu, uhusiano wa Lila na Vero unayadhibiti matumizi yao ya lugha. Kwa upande mwingine, Lila anajaribu kuudhibiti mvutano baina yake na Vero kupitia matumizi ya mikakati mbalimbali ya upole.

### 4.3.3 Matumizi ya Lugha na Uhusiano wa Wahusika Katika Kazi

Hili ni suala lingine ambalo hudhibiti matumizi ya lugha ya wanajamii wanapoingiliana. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), Uhusiano wa wahusika katika kazi au taaluma huathiri matumizi yao ya lugha. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, uhusiano wa wanajamii hujengeka katika ukweli kuwa wanajamii hushikilia nafasi tofautitofauti za kitaaluma.Kwa mujibu wa tathimini za wanajamii mbalimbali, baadhi ya kazi hutofautiana katika hadhi, zingine hupewa hadhi kuu kuliko zingine. Hii ina maana kuwa, kwa mfano kijakazi anapoingiliana na mwajiri wake atajifunga na matumizi ya lugha ya upole kwa mapana kinyume na mwajiri wake ambaye hatachukulia suala hili kwa uzito. Hali hii pia hujidhihirisha katika mahusiano baina ya mhazili na mkuu wake ambapo mhazili hufungwa na kaida za matumizi ya lugha ya upole kwa mapana kuliko mwajiri wake.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* suala la uhusiano wa katika kazi linajidhihirisha katika matumizi ya lugha ya Mama anapoingiliana na Mjakazi pale nyumbani,kwa mfano:

153. Mjakazi: Mama tafadhali onja kidogo.
Mama: [Anamsubu] Wewe! Usiniletee nuksani
na ilhali mwanangu kapotea.
Mjakazi: Kunywa kidogo tu mama. Kidogo tu...Tafadhali.
Mama: Nimekwambia s'taki! [Mama anamtandika Mjakazi
kofi la shavuni. Punde anaingia Lila
anahemahema na kufuta jasho] uk75

Katika mfano 153, uhusiano wa Mama na Mjakazi ambao ni wa mwajiri na mwajiriwa unadhihirika. Katika matumizi yake ya lugha, Mjakazi anatumia mkakati chanya wa upole ambao unabainishwa na matumizi ya maneno ya kurai kama *tafadhali onja kidogo*, *kunywa kidogo tu mama.* Matumizi haya ya maneno ni dhihirisho kuwa Mjakazi anaonyesha kujali maslahi ya Mama kwa kuufurahisha uso wake chanya. Sababu ya kufanya hivi ni kuonyesha heshima aliyo nayo kwa mwajiri wake kwa kumjengea Mama picha ya mwajiriwa mwenye utu na kujali.

Kwa upande mwingine, lugha ya Mama inatawaliwa na ukali. Ukali huu unadhihirishwa na mkakati ndani ya rekodi unaotambulishwa na kauli ya moja kwa moja; *Nimekwambia s'taki* na na matumizi ya neno; *s'taki*. Katika mfano 150, Mama anabainika kama mwenye mamlaka zaidi akilinganishwa na Mjakazi. Mjakazi anadhihirisha hili kupitia lugha yake upole kwa kusema; *Mama tafadhali onja kidogo.* Hii ina maana kuwa uhusiano wa mwajiri na mwajiriwa unaojitokeza katika lugha ya Mama na Mjakazi unakuwa na mchango mkubwa katika kuyadhibiti matumizi ya lugha ya wahusika hawa.

**4.4 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia hali zinazodhibiti matumizi ya mikakati ya upole na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.* Katika kutekeleza hili, mtafiti amegawa hali hizi katika makundi matatu kama zinavyoelezwa katika Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Hali hizi ni pamoja na; uhusiano wa kijamii, malengo ya mzungumzaji sawa na uzito wa tendo la kutishia uso linalohusika na nguvu au mamlaka aliyo nayo mhusika katika jamii. Aidha, sehemu hii imeonyesha aina mbalimbali za uhusiano wa jamii na jinsi ambavyo zinaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika hawa.

Aidha, mtafiti ameonyesha aina mbalimbali za nguvu za malaka ambazo zinadhibiti na kutawala matumzi ya lugha ya wahusika na matumizi yao ya mikakati ya upole. Aina hizi za mamlaka ni pamoja na, mamlaka ya familia, mamlaka katika sheria, uwezo wa nguvu za mwili na mamlaka katika uchumi. Katika kuonyesha uhusiano wa malengo ya wahusika na matumizi ya mikakati ya upole, imebainika kuwa lengo la mhusika na uzito wa tendo la kutishia uso linalohusika lina mchango wa mkubwa katika kubainisha mkakati wa upole ambao wahusika wanatumia katika mazungumzo yao.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti anashughulia muhtasari na mapendekezo ya utafiti. Katika kufanya hili, mtafiti anajadili, matokeo ya uchunguzi, changamoto za utafiti na vilevile kutoa mapendekezo kuhusiana na tafiti zingine ambazo zinafaa kufanywa kuhusiana na suala la upole katika taaluma ya isimu-matini.

## 5.1 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti alidhamiria kubainisha iwapo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanatumia mikakati ya upole wanapoingiliana na wahusika wengine ili kufanikisha mazungumzo yao. Pia, mtafiti alinuia kuchunguza jinsi mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* inachangia katika kuzikuza sifa zao.Aidha, utafiti huu ulilenga kutambua hali zinazoyaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu.*

Lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kubainisha iwapo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanatumia mikakati ya upole wanapoingiliana na wahusika wengine ili kufanikisha mazungumzo yao limeafikiwa.Wahusika wakuu ambao wanashughulikiwa ni pamoja na: Matari, Lila, Temba na Mama. Kama ambavyo inadhihirishwa katika sura ya pili ya utafiti, wahusika wakuu wanaitumia mikakati yote minne ya upole katika maingiliano yao na wahusika wengine. Mikakati hii ni pamoja na: mikakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole, mkakati wa upole nje ya rekodi na mkakati wa upole ndani ya rekodi.Matumizi ya mkakati chanya wa upole katika lugha ya wahusika hawa yanabainika kupitia njia mbalimbali.

Kwanza wahusika wakuu wanazitambua na kuzishughulikia nyuso chanya za wasikilizaji wao. Mbinu hii inatumika na wahusika katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano Lila anautambua uso chanya wa Mama anapomsihi kama inavyodhihirishwa katika mfano 39; *Kula mama. Kula kidogo.* Lila anamtambua Mama kwa kumwita Mama na pia kudhihirisha hali ya kumjali kwa kumbembeleza ale kidogo.

Kando na kumtambua na kumshughulikia msikilizaji, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanadhihirisha upole chanya katika mazungumzo yao kwa kutumia vitambulisho vya makundi. Kwa mfano katika mfano 45, Mama anautambua uso chanya wa Temba kwa kumwambia: *Pole kwa safari mume wangu.* Katika mfano huu, Mama anatumia kauli *mume wangu* kumtambua Temba kama mume wake.

Wahusika wakuu pia wanashughulikia nyuso chanya za wasikilizaji wao kwa kutafuta makubaliano nao pamoja na kuepuka kuwapinga. Kwa mfano, Lila anakubaliana na Mama anaposhauriwa afikirie kuhusu ndoa kwa kusema; *Sawa mama, nimesikia.* Dayolojia hii inaangaziwa katika mfano 48. Katika dayolojia hii, Lila anadhihirisha upole chanya kwa Mama kwa kuepuka kuipinga kauli yake kuhusu ndoa.

Kando na kutafuta makubaliano, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanadhihirisha upole chanya kwa kuchangia mada zinazoanzishwa na wasikilizaji wao. Kwa mfano, katika mfano 51, Temba anamwuliza Lila maswali kama njia ya kumwonyesha kuwa anaifuatilia mada yake. Temba anauliza; *Kwani kulikoni? Eeh? Kisha?  Halafu? Lahaula!* Maswali haya yanadhamiria kumwonyesha Lila kuwa Temba anataka kujua mengi zaidi kuhusu kisa cha wizi wa ng'ombe wa Tonge hivyo kumpatia motisha ya kuendeleza mazungumzo yake.

Vilevile, mbinu ya ucheshi inatumika na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* katika kushughulikia nyuso chanya za wasikilizaji wao. Kwa mfano, Matari anadhihirisha upole chanya kwa Mama anapokuwa akikosolewa na Mama kwa kumwibia dadake pesa. Mama anapotaka kujua kama Matari ameiacha tabia ya kuiba, Matari anamjibu Mama kwa kuzua ucheshi ambao unabainishwa na jinsi anavyolichezea neno kuokoka. Matari analipatia neno hili maana nyingine ya kunusurika kifo kwa kusema; *Najua unachotaka mama.Unataka niseme nimeokoka na kumkubali Yesu na kadhalika.Wataka nikwambie leo nimekutana na Yesu njiani nikienda kwa Fiona kugeuza maji au chang'aa? Unafikiri kama Yesu asingalikuwa rafiki Yangu ningekuwa hai?* Kupitia matumizi ya mkakati huu, Matari anafanikiwa kumfamnya Mama asahau kuwa alikuwa amemwibia dadake pesa. Mbinu hii pia inadhamiria kuimarisha uhusiano baina ya Matari na mamake kwa kuumaliza mvutano baina ya wahusika hawa wawili.

Wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* pia wanatumia mbinu ya kumjumlisha msemaji na kitendo chenye manufaa kama njia ya kuzihifadhi nyuso chanya za wasikilizaji wao. Kwa mfano, Temba anamhusisha mwanawe na tendo la kula anapokuwa akimshawishi kumsamehe kakake Matari kama inavyoonyeshwa katika mfano 57. Temba anamwambia Tonge; *Nawa tule mwanangu.* Kwa kutumia neno *tule*, Temba anamjulisha Tonge kwa kitendo cha kula na kuonyesha uhusiano wa karibu uliopo baina yake na Tonge.

Vilevile, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanafanikisha mazungumzo yao kwa kutumia mkakati chanya wa upole kupitia matumizi ya kauli zinazoonyesha utoaji ahadi. Kwa mfano, Katika mfano 59, Matari anajitetea kwa Lila anapolaumiwa kwa kumwibia pesa kwa kutoa ahadi ya kuzilipa baadaye.*Pesa zako nitakulipa.Saa hii sina. Nipe muda tu*. Katika mfano huu, Matari anaufurahisha uso chanya wa Lila kwa kutoa ahadi ya kuzilipa pesa alizomwibia. Kwa kutumia mkakati huu, Matari anafanikiwa kuumaliza mgogoro uliopo baina yake na dadake hivyo kuudhibiti mkondo wa mazungumzo yao.

Kando na kuutumia mkakati chanya wa upole, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanashughulikia nyuso hasi za wasikilizaji kama ambavyo inabainishwa katika sura ya pili. Katika sura hii, inabainika kuwa mkakati hasi wa upole unatumika kwa mapana wakati ambapo mhusika anamfahamisha msikilizaji wake tendo la kutishia uso hasi. Pia, mkakati huu unatumika wakati ambapo mhusika anataka kuomba msamaha kwa kumkosea msikilizaji wake. Mkakati huu unabainika katika matumizi ya lugha ya wahusika hawa kwa namna mbalimbali.

Kwanza, wahusika wanatumia vitangulizi ambavyo vinamtayarisha msikilizaji kuupokea ujumbe hasi. Kwa mfano, Lila anautambua uso hasi wa Mama kwa kumwomba msamaha kwa kukurupuka kwake na kumwacha peke yake. Lila anasema hivi katika mfano 63; *Samahani mama. Nimefanya kukurupuka hapa tu ghafla.* Katika mfano huu, Lila anajitetea kwa Mama kwa kumwomba msamaha kabla ya kuelezea sababu yake ya kukurupuka. Kwa kutumia maneno haya, Lila anafanikiwa kumtuliza Mama na kuyajenga mazingira mazuri ya kuingiliana naye.

Pili, wahusika hawa wanashughulikia nyuso hasi za wasikilizaji wao kwa kutoa kauli za jumla ambazo hazihusishwi na mtu maalum. Kwa mfano, Lila anamkosoa Matari kwa kumwibia pesa

kwa kusema hivi katika mfano 70, *Mwizi kazi yake gani kama si kuiba?* Kwa kutumia kauli hii Lila anamkashifu Matari kwa kumwita mwizi lakini kwa namna inayodhihirisha upole hasi. Katika kauli hii pia, Lila anaepuka kumtaja Matari kama mwizi na badala yake kumwuliza swali la jumla.

Kando na matumizi ya kauli za jumla, wahusika hawa wanatumia mkakati wa kubashiri matokeo mabaya ya kitendo chao kama njia ya kuushughulikia uso hasi wa wasikilizaji wao. Kwa mfano, katika mfano 78, Lila anatumia mkakati huu anapokuwa akimwarifu Mama kuhusu kukamatwa kwa Matari. Lila anamwambia Mama, *Najua wewe ni mgonjwa lakini nitakwambia ukweli.* Katika kauli hii, Lila anamjulisha Mama kuhusu uzito wa kitendo chake cha kutishia uso kwa kuutambua uso hasi mwanzo. Lila anamdhihirishia Mama kuwa anaelewa hali yake kwa kutumia neno *Najua* lakini anasisitiza haja ya kuzisema habari zake.Kwa kutumia mkakati huu, Lila anamtayarisha Mama kuzipokea habari za kukamatwa kwa Matari.

Vilevile, wahusika wakuu wanashughulikia uso hasi wa wasikilizaji wao kwa kuonyesha heshima baina yao na wasikilizaji wao.Kwa mfano, Matari anajidunisha mbele ya walevi wenzake katika baa ya Fiona kwa kujilinganisha na jamaa wengine wa familia yao. Matari anawaambia walevi hivi; *Shamba la baba maddal basari, si kwambii nyumba za kupangisha kwenye kituo cha kibiashara na mjini, matatu.* Matari pia anajidunisha kwa kusema; *Mimi Matari kwa maana ya mburumatari. Maskini hali yangu.*Kwa kutumia kauli hii, Matari anajiweka katika kiwango sawa na walevi hivyo kuwafanya wamuone kama mmoja wao. Aidha, Matari anafanikiwa kuihalalisha tabia yake ya wizi kwa walevi kuwa, inatokana na hali yake duni ya maisha.

Pia, wahusika wakuu wanatambua nyuso hasi za wasikilizaji wao kupitia kuvielezea vitendo vya kutishia uso kama kanuni ya jumla au ukweli unaojulikana. Kwa mfano, katika mfano 83, Mama anamshawishi Lila kukubali kuolewa kwa kurejelea ndoa kama tukio la maumbile.Mama anasema hivi, *Ndoa ni kitu cha lazima kwa mwanadamu mwanangu.* Katika kauli hii Mama anadhihirisha upole hasi kwa kuepuka kumwambia Lila aolewe kwa njia ya moja kwa moja.

Vilevile, wahusika wakuu wanatekeleza tendo la kutishia nyuso hasi za wasikilizaji wao kwa kutumia mkakati wa kupunguza ulazimishaji. Kwa mfano, Matari anatumia mkakati huu anapokuwa akimwomba Lila asiongee kuhusu tabia yake ya wizi kwa sauti kubwa. Katika mfano 85, Matari anamwambia… *Basi usiseme kwa sauti mama atasikia.*Katika mfano huu, Matari anamtaka Lila kutosema kwa sauti lakini anatumia maneno *basi usiseme* ambayo yanadhihirisha kuwa hadhamirii kumlazimisha Lila kufanya hivyo.

Kando na kuepuka kulazimisha, wahusika wakuu wanadhihirisha upole hasi kupitia matumizi ya maswali.Wahusika hawa wanatumia maswali haya ama katika kuwakosoa wasikilizaji wao au kuonyesha kutokubaliana nao. Kwa mfano, Lila anadhihirisha hasira yake kwa Matari kwa kujibu swali lake kwa namna ya swali. Katika mfano 85, Matari anamtaka Lila kutosema kwa sauti ili mamake asisikie. Katika kumjibu Matari, Lila anamwuliza swali ambalo linaficha ukali ndani yake. *Mbona asisikie?* Matumizi ya swali hili ni ithibati kuwa Lila hakubaliani na maoni ya Matari bali ameuweka msimamo wake kwa namna inayodhihrisha upole hasi.

Mkakati wa upole nje ya rekodi pia unatumika na wahusika wakuu katika kushughulikia nyuso hasi za wasikilizaji wao. Matumizi ya mkakati huu yanajibainisha kupitia njia mbalimbali. Kwanza, kupitia matumizi ya maswali ya balagha. Kwa mfano, Matari anamkosoa Mtu II kwa kusema kuwa Tonge hana uwezo wa kumtia mimba bibi yake kwa kusema hivi; *Sasa hayo ni mambo gani ya kusemwa mbele ya watu?* Katika swali hili Matari anaipinga kauli ya Mtu II lakini kwa namna ambayo inadhihirisha upole hasi.

Kando na matumizi ya maswali ya balagha, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanadhihirisha upole hasi kupitia matumizi ya tamathali za lugha. Kwa mfano, Matari anamwonya Mtu II dhidi ya kuongea kuhusu ndoa ya Tonge kwa kumwambia; *Za upenuni hazisemwi njiani ati*. (Mfano 100). Katika kauli hii, Matari anarejelea hali ya Tonge ya kutoweza kumtia mimba mkewe kama habari za upenuni ambazo hazifaii kusemwa hadharani. Kwa kusema hivi, Matari anaepuka kumpinga Mtu II kwa njia ya moja kwa moja hivyo kuuhifadhi uso wake hasi.

Vilevile, wahusika wakuu wanafanikisha mazungumzo baina yao na wasikilizaji wao kupitia utoaji wa maelezo pungufu.Kwa mfano, Lila anakataa kumjibu Mama kuhusu alikokuwa kwa kusema; *Hapa na pale.* Katika mfano103, Lila anauhifadhi uso hasi wa Mama kwa kutomweleza kuwa alikuwa akimfuata Matari ambaye amemwibia pesa zake.Lila anafanya hivi ili kuepuka kumkasirisha Mama kwa kumwambia kuwa Matari ni mwizi.

Licha ya kutoa maelezo pungufu, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanahifadhi nyuso hasi za wasikilizaji wao kwa kutoa maelezo ya mzunguko. Mkakati huu unatumika na Lila anapokuwa akimweleza babake kuhusu sababu yake ya kutoenda kwa mwalimu. Katika mfano 107, Lila anatoa maelezo mengi kuhusu makutano yake na Vero sokoni. Lila anatumia mkakati huu kama njia ya kumfanya babake asahau mada ya hapo awali ambayo inahusisha sababu yake ya kutokwenda kwa mwalimu.

Wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* pia wanafanikisha mazungumzo yao na wahusika wengine kwa kuhifadhi nyuso zao hasi kupitia kubadilisha mada ya mazungumzo. Ubadilishaji huu unatokea pale ambapo mada inayohusika haimfurahishi msikilizaji au inatishia kuyavunja mazungumzo. Kwa mfano, Lila anabadili mada ya mazungumzo yake na Mama kuhusu ndoa kwa vile inatishia uso wake. Mama anamfanyia Lila mzaha askari wanapoingia kumkamata Matari kwa kumuliza, *Ni mwana wa nani aliyekuja kukuposa?* Katika kulijibu swali hili, Lila anaiahirisha mada hii kwa kusema, *Mama hayo tuyazungumze baadaye*.

Kama inavyojadiliwa katika sura ya kwanza, mkakati wa upole ndani ya rekodi unapotumika huwa haudhamirii kuhifadhi uso wa msikilizaji bali kuwasilisha ujumbe. Hali hii inajidhihirisha Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* ambapo mkakati huu unatumiwa kwa kiasi kidogo sana ikilinganishwa na mikakati mingine ya upole. Hili si jambo la kustajabisha ikizingatiwa kuwa hii ni kazi ya kidrama ambayo hujengwa katika msingi wa migogoro baina ya wahusika. Kwa sababu ya migogoro hii, wahusika wanajitahidi kuzihifadhi nyuso za wasikilizaji wao ili kuepuka kuyavunja mazungumzo yao.

Japo hali ni hivyo, mkakati huu unadhihirika katika lugha ya wahusika wakuu wanapotaka kupitisha ujumbe wa dharura ama kuonyesha mamlaka yao. Adha, mkakati huu unatumika

wakati tendo la kutishia uso linalofanywa na mhusika lina mfaidi msikilizaji wake. Kuongezea, mkakati wa upole ndani ya rekodi unatumika wakati wahusika wakuu wanataka kudhihirisha hasira yao kwa wasikilizaji wao. Kwa mfano, Matari anatumia mkakati ndani ya rekodi anapokuwa akimtataka Fiona kuzitoa pesa zake. Kama inavyojadiliwa katika mfano 112, Matari anasema; *Toa fedha zangu.* Katika kauli hii, Matari anamwamrisha Fiona kuzitoa pesa zake bila kuonyesha upole wowote kutokana na ukweli kuwa Matari ana mamlaka ya uchumi pamoja na mamlaka ya nguvu za mwili dhidi ya Fiona.

Katika mfano 114, Lila anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi anapomtaka Mjakazi kumletea mamake chakula. Lila anasema hivi; *Nenda kamletee mama chakula.* Katika mfano huu inabainika kuwa, uhusiano wa Lila na Mjakazi ambao ni wa mtu na mfanyikazi wake unamfanya Lila kutozingatia upole katika kuwasilisha ujumbe wake kwa Mjakazi. Mifano mingine kudhihirisha miktadha ya matumizi ya mkakati wa upole ndani ya rekodi na wahusika wakuu imejadiliwa katika sura ya pili.

Kama ambavyo imedhihirishwa katika mjadala huu, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* wanaitumia mikakati mbalimbali ya upole wakati wa mazungumzo yao.Jambo linalobainika hapa ni kuwa, matumizi ya mikakati hii si tukio la sadfa bali ni mbinu ya kuzihifadhi nyuso za wasikilizaji wao.Kama ambavyo inabainika katika sura ya pili, migogoro mbalimbali baina ya wahusika hawa ndicho chanzo cha wahusika hawa kuzingatia upole wanapoingiliana na wasikilizaji wao. Hii ina maana kuwa, kila wakati wahusika wakuu wanahusika katika mivutano, wanajaribu kuzuia kuvunjika kwa mazungumzo haya kwa kuzishughulikia nyuso za wasikilizaji wao. Hali hii ya kutaka kuyafanikisha mazungumzo ya wahusika wakuu ndio msingi mkuu wa kuitumia mikakati mbalimbali ya upole.

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* inachangia katika kuzikuza sifa zao. Lengo hili linajadiliwa katika sura ya tatu. Katika sura hii, inabainika kuwa, kuna uhusiano wa karibu sana baina ya ukuzwaji wa sifa za wahusika wakuu na mikakati ya upole wanayoitumia. Mjadala katika sura ya tatu unathibitisha kuwa, sifa za wahusika wakuu ambao ni Matari, Lila, Temba na Mama zinabainika kutokana na mikakati yote minne ya upole wanayoitumia.

Kwanza, sifa ya matari ya ukatili inabainika kupitia matumizi ya mkakati ndani ya rekodi anapokuwa akimtahadharisha Lila dhidi ya kumwibia pesa zake. Sifa hii inabainika kupitia lugha ya vitisho anayoitumia kama ambavyo inadhihirishwa katika mfano 122, *Uchunge sana ukinipunja au kuniibia hizi pesa naweza kukufanya chochote…nitakufanya lolote na wala hakuna lolote litakalonipata, ushafahamu? Ninaweza nikakuibia,au nikakugeuza kizuu au hata kukubaka*. Katika mfano huu, sifa ya ukatili ya Matari inabainika kwa uwazi kupitia matumizi ya maneno ya vitisho anayoyatamka kwa Fiona. Katika mfano huu pia, Matari anadhihirisha hasira yake kwa Fiona kwa kumwambia achunge sana kuwa anaweza akamfanyia chochote.

Pili, mikakati ya upole kama inavyotumiwa na Lila inachangia katika kuzibainisha sifa zake.Kwa mfano, katika mfano 125 Lila anamwambia Matari, *Acha kunichezea akili.* Katika kauli hii Lila anatambulishwa kama mhusika mtambuzi. Kwa kutumia msemo huu, Lila anabainika kama mhusika mwenye uwezo wa kutambua wakati Matari anamchezea akili. Sifa nyingine za Lila zinabainika katika matumizi yake ya mikakati ya upole kama ambavyo inajadiliwa katika sura ya tatu.

Vilevile, katika sura ya tatu sifa za Temba zinabainika kupitia mikakati ya upole anayoitumia anapoingiliana na wahusika wengine. Kwa mfano, sifa ya hasira ya Temba inabainika wakati anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi pamoja na mkakati wa upole nje ya rekodi kumfokea Lila. Katika mfano 130, Temba anamwambia Lila; *Fanya kama nilivyokwambia au nyumba yangu uione paa.* Katika kauli hii, Temba anamwamrisha Lila kufanya alilolisema baada ya Lila kutaka kumpinga. Hasira ya Temba pia inabainika kupitia matumizi ya lugha ya amri ambayo inatambulishwa na matumizi ya neno *fanya*. Aidha, Temba anatoa vitisho na kuonyesha ukali wake kwa kutumia msemo; *nyumba yangu uione paa.*Katika msemo huu, Temba anamlazimisha Lila kutii amri yake.

Kando na hili, sifa za Mama zinabainika kupitia matumizi yake ya mikakati mbalimbali ya upole. Kwa mfano, katika mfano 133, Mama anajitokeza kama mwenye kudekeza katika malezi. Sifa hii inabainika kupitia matumizi ya mkakati wa upole nje ya rekodi anapokuwa akimtetea Matari kuwa hawezi akaiba. Mama anamwambia Lila; *Hapana! Haiwezekani! Mwanangu kuiba*

*na kubaka?* Katika mfano huu, Mama anajitokeza kama mdekezi kwa kukana chochote kinachosemwa kuhusu tabia ya mwanawe.

Kama ambavyo mifano iliyo hapa juu inabainisha, ni wazi kuwa mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* inachangia katika kuzibainisha sifa za wahusika wakuu. Aidha, kama ambavyo sura ya tatu inaonyesha sifa hasi na chanya za wahusika hawa zinabainika. Kwa mfano, mkakati ndani ya rekodi unatumika kubainisha sifa hasi za wahusika kama vile; sifa ya hasira, ukatili na ukali. Mkakati hasi wa upole unapotumika na mhusika unachangia katika kuzibainisha sifa za majuto, ukataji tama miongoni mwa nyingine. Sifa chanya za wahusika wakuu pia zinabainika kupitia matumizi ya mkakati chanya wa upole.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kutambua hali zinazoyaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*. Lengo hili limejadiliwa katika sura ya nne ya utafiti huu. Matokeo ya lengo hili ni kuwa, wahusika wote wakuu ambao ni pamoja na Matari, Lila, Temba na Mama wanaathiriwa na hali mbalimbali za jamii katika kutumia mikakati ya upole.

Kwanza, kama ambavyo inabainika katika sura ya nne, mamlaka ya mhusika katika ngazi za jamii yanamwathiri pakubwa katika matumizi yake ya mikakati ya upole. Mamlaka haya yanangaziwa katika ngazi tatu muhimu za jamii ambazo ni mamlaka ya mhusika katika familia, mamlaka katika kuudhibiti uchumi na mamlaka yanayotokana na uwezo wa nguvu za mwili.

Katika ngazi ya familia, mamlaka ya Temba kama kiongozi wa familia yanadhihirika anapokuwa akimwamrisha Lila kutekeleza wajibu wake wa kwenda kwa mwalimu kumdaia deni lake. Katika mfano 136, Temba anatahadharisha Lila dhidi ya kukaidi agizo lake kwa kumwambia; *Nimesema usiniletee ufedhuli hapa. Fanya kama nilivyokwambia au nyumba yangu uione paa.Ushasikia?* Mkakati wa upole ndani ya rekodi ambao unatambulishwa na matumizi ya maneno ya amri; *Fanya kama nilivyokwambia*, yanaweka wazi uwezo wa Temba wa kumdhibiti Lila. Hapa, mamlaka ya Temba katika familia yanamfanya kuutumia mkakati wa upole ndani ya rekodi.

Aidha, mjadala katika sura ya nne umeweka wazi ukweli kuwa mamlaka katika ngazi ya sheria yanayadhibiti matumizi ya mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu kwa mapana. Kwa mfano, katika mfano 138, Mama anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi anapokuwa akimtahadharisha Vero dhidi ya kupiga kelele kortini kwa kusema, *Nyamaza au nikufunge jela.* Katika kauli hii, Mama anatumia mkakati huu wa upole kwa vile ana mamlaka makubwa kwa Vero. Kwa msingi huu, matumizi ya mikakati ya upole katika muktadha huu yanaathiriwa na cheo chake.

Katika sura ya nne imebainika kuwa, nguvu za mwili walizo nazo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* zina mchango mkubwa katika kuyaathiri matumizi yao ya mikakati ya upole.Kwa mfano, Matari anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi kwa Fiona katika mfano 143 kwa kumwambia; *Naweza nikakuibia au nikakugeuza kizuu, au hata kukubaka au nikukate kichwa kitengane na kiwiliwili.* Katika mfano huu, Matari anatumia lugha ya vitisho bila kuzingatia suala la upole kwa vile anafahamu kuwa ana uwezo mkubwa wa nguvu za mwili akilinganishwa na Fiona.Katika, muktadha huu, matumizi ya mkakati wa upole yanadhibitiwa na uwezo alio nao Matari kwa Fiona.

Aidha, mjadala katika sura ya nne unadhihirisha kuwa matumizi ya mikakati ya upole kama yanavyobainika katika matumizi ya lugha ya wahusika wakuu yanaathiriwa pakubwa na uwezo wa kiuchumi walio nao wahusika. Kwa mfano, Matari anatumia mkakati wa upole ndani ya rekodi anapokuwa akimfahamisha Fiona kuwahudumia walevi. Katika mfano 144, Matari anamwambia Fiona hivi; *Wape buzaa wote walewe hadi waanguke wake zao na wanaume zao waje wawaokote.* Katika mfano huu, Matari anatumia lugha ambayo haidhamirii kuonyesha upole kwa Fiona kwa sababu ya uwezo wake wa fedha. Hii ina maana kuwa, utajiri wa Matari unampa mamlaka ya kutumia mkakati ndani ya rekodi kwa Fiona.

Malengo ya wahusika wakuu pia yanayaathiri matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*. Kwa mfano, Lila anatumia mkakati hasi wa upole anapokuwa akimfahamisha mamake kuhusu kukamatwa kwa Matari. Katika mfano 148, Lila anamwambia Mama hivi; *Najua wewe ni mgonjwa lakini nitakwambia ukweli.*Katika kauli hii, Lila anatumia maneno*; Najua wewe ni mgonjwa* kwa nia ya kumtayarisha Mama kuupokea

ujumbe mzito kuhusu kukamatwa kwa Matari. Hapa Lila ana lengo la kupasha ujumbe mzito kwa Mama hali ambayo inamlazimu kumwandaa Mama mapema kuupokea kwa kuitambua hali yake ya afya. Hii ina maana kuwa, lengo la Lila la kumfahamisha Mama kuhusu kukamatwa kwa Matari linakuwa kidhibiti cha matumizi yake ya mikakati ya upole.

Kando na malengo ya wahusika, matumizi ya mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wakuu yanaathiriwa na mahusiano yao katika jamii. Hali hii inadhihirishwa katika sura ya nne ambapo inabainika kuwa mahusiano waliyo nayo wahusika yanachangia katika kubainisha mikakati ya upole wanayoitumia katika mazungumzo yao. Kwa kurejelea mfano 150, Mama anadhihirisha upole chanya kwa mumewe Temba anapokuwa akimkaribisha nyumbani kwa kumwambia; *Pole kwa safari mume wangu.*Katika mfano huu, Mama anatumia mkakati chanya wa upole ili kuufurahisha uso chanya wa mumewe. Katika mfano huu, uhusiano baina ya Mama na Temba ambao ni wa mume na mkewe unamfanya Mama kutumia mkakati chanya wa upole ili kudhihirisha heshima yake.

Kwa jumla, matokeo ya uchunguzi huu yanabainisha kuwa malengo yote matatu ya utafiti huu yameafikiwa. Ufanisi huu undhihirishwa katika sura za pili,tatu na nne pamoja na hitimisho letu katika sura ya tano. Katika kutathmini malengo ya utafiti huu, katika kila mojawapo ya sura zilizoshughulikiwa inajitokeza kuwa, mikakati ya upole kama inavyotumika na wahusika hawa ina mchango mkubwa katika kufanikisha maingiliano ya wahusika wakuu. Matumizi ya mikakati hii yana mchango mkubwa katika kuzuia kuvunjika kwa mazungumzo hasa katika miktadha ambapo wahusika hawa wanajikuta katika migogoro baina yao wenyewe au baina yao na wahusika wengine.

### 5.2 Changamoto za Utafiti

Utafiti wetu ulikabiliwa na changamoto kadhaa kuanzia mwanzo hadi mwisho.Kwanza, tatizo la uanishaji wa kauli za wahusika katika kategoria ya mikakati mbalimbali ya upole. Changamoto hii inatokana na ukweli kuwa kauli ya mhusika inaweza ikaangukia katika mkakati zaidi ya mmoja. Katika uchunguzi huu, inabainika kuwa kuna miktadha ambayo kauli ya mhusika inaweza ikaainishwa kama mkakati hasi wa upole na vilevile kama mkakati wa upole nje ya rekodi. Hali hii inatokea pale ambapo kauli ya mhusika inajumuisha maneno yanayodhihirisha

kuwepo kwa mikakati miwili au zaidi ya upole ndani yake.Mtafiti alijaribu kukabiliana na changamoto hii kwa kuzingalia kauli hizi kama zinazojumuisha matumizi ya mikakati mseto ya upole hivyo kuzichambua kama kauli moja inayojumuisha mikakati mingi ya upole ndani yake.

**5.3 Mapendekezo**

Mtafiti anapendekeza tafiti zifuatavyo zifanywe; kwanza utafiti utakaochunguza suala la upole kwa kutumia tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile riwaya na hadithi fupi ili kubainisha jinsi mikakati ya upole inavyotumiwa na wahusika wakuu katika tanzu hizi. Pili, tunapendekeza kuwa watafiti wengine wafanye uchunguzi utakaotumia wahusika wadogo katika kazi za drama ili kubainisha jinsi mikakati ya upole wanayoitumia inasaidia katika kuzibainisha sifa zao. Mtafiti pia anapendekeza kufanywe utafiti utakaobainisha jinsi wahusika wa kiume na kike wanatofautiana katika matumizi yao ya mikakati ya upole katika tamthilia ya Kiswahili. Vilevile, mtafiti mwingine afanye uchunguzi ili kubainisha jinsi mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika inachangia katika kuyakuza maudhui katika tamthilia ya Kiswahili.

## MAREJELEO


Bell, N. (2003) “Politeness in the Speech of Korean ESL Learners.” *Working Papers in Educational Linguistics:*

Brown, P. & Levinson, S. (1987) *Politeness: some universals in language usage*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cutting, J. (2008) *Pragmatics and discourse: A resource book for students*. London: routledge.

Fatkhurozi, A. (2007) “Politeness Strategies Used by Mia and Her Grandma in ‘Princess Diaries’ Film”. Malang: English Letters and Language Department. Unpublished Thesis.

Goffman, E. (1955) “On face-work: An analysis of ritual elements in social interaction”. *Psychiatry: Journal of Interpersonal Relations* 18, 213–231. Reprinted in: Erving Goffman (1967).

Grice, H.P. (1975) “Logic and conversation.” In Peter Cole & Jerry Morgan (eds.) *Syntax and Semantics*, Volume 3: *Speech Acts*, pp. 41–58. New York, NY: Academic Press.

Hoobs, P. (2003) “The Medium is The Message: Politeness Strategies in Men’s and Women’s Voice Mail Message.”*Journal of pragmatics* (35) 243- 262.

Huang, Y. (2006) *Pragmatics*. New York: Oxford University Press.

Ratna, I. (2012) “An Analysis of Politeness Strategies used by Harry Potter in J.K. Rowling’s novel ‘Harry potter and the sorcerer’s stone’ ” Thesis. State Institute for Islamic Studies. Unpublished Thesis.

Kariithi, F. (2010) “Mikakati ya Upole katika Matumizi ya Lugha ya Vijana.” Tasnifu ya Uzamili Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Katayoon, A. (2013) “Character revelation and dialogue interpretation through Politeness theory and Conversation analysis in dramatic discourse: The case of Woody Allen’s Death Knocks.”*Journal of Language and Literature Education, 2*(6), 43-54.

Lakoff, R. (1976) “What You can Do with Worlds: politiness pragmatic and perfomatives” In the Proceedings of Texas Conference on: Perfomatives Pressupositions and Implicature, Rogers R, & Wall, J(Ed).

Leech, G. (1983) *Principles of politeness*. London: Longman.

Mufidatul, U. (2010) “An Analysis of Negative Politeness Found in ‘There is something about Mary’ film.” Malang: English Letters and Language Department, Malang. Unpublished Thesis.

Mwari, R. (2014) “Mikakati ya Upole katika vipindi vya runinga: Mawaidha na Bi.Msafwari katika Runinga ya Citizen.” Tasnifu ya Uzamili Chuo kikuu cha Nairobi.Haijachapishwa.

Owino, M. (2011) “Uchanganuzi wa Matini Teule ya Nyimbo za Faustine Munishi: Mtazamo wa Nadharia ya Upole.” Tasnifu ya Uzamili Chuo kikuu cha Nairobi.Haijachapichwa.

Sari, Y. (2010). “The Politeness Strategies Used by Anne as the Ambitious Main Character in ‘The Other Boleyn Girl’ Movie.” Unpublished Thesis. Malang: English Letters and Language Department, UIN Malang.

Scollon, R and Scollon, S. (1995) *Intercultural Communication*. Cambridge, MA: Blackwell.

Spencer-Oatey, H. (2000) *Culturally Speaking: Managing Rapport through Talk across Cultures.* London:Continuum.

Walibora, K. (2014) *Mbaya Wetu*. Nairobi: Moran Publishers.

Watts, R. (2003) *Politeness.* Cambridge: Cambridge University Press.

Walubengo, A. (2010) “Suala la Upole katika Jando ya Jamii ya Wabukusu.” Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Wilamova, S. (2005) “On the function of hedging devices in negatively polite discourse.” *BRNO Studies in English, 31,* 85-93.

Yule, G. (1996) *Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press.